

AMALI

ZA

MAKKA

Kimeandikwa na:
Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi

Kimetarjumiwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed
Na:
Al-Haj Ramadhani K. Shemahimbo

©Haki ya kunakili imehifadhiwa na:
AL-ITRAH FOUNDATION

ISBN: 978 - 9987 - 17 - 019 - 7

Kimeandikwa na:
Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi

Kimetarjumiwa na:
Alhaji Hemedi Lubumba

Kimehaririwa na:
Ustadh Abdallah Mohamed

Na:
Al-Haj Ramadhani K. Shemahimbo

Kimepangwa katika Kompyuta na:
Al-Itrah Foundation

Toleo la kwanza: Januari, 2014

Nakala: 1000

Kimetolewa na kuchapishwa na:

Alitrah Foundation
S.L.P. - 19701, Dar es Salaam, Tanzania
Simu: +255 22 2110640 / 2127555
Barua Pepe: alitrah@yahoo.com
Tovuti: www.ibn-tv-com
Katika mtandao: www.alitrah.info

ترجمة

أدب الحرمين

أعمال المكة

التأليف

السيد جواد الحسيني آل علي الشهري

من اللغة العربية إلى اللغة السواحلية

YALIYOMO

NENO LA MCHAPISHAJI.....	9
DIBAJI.....	11
Faslu ya Kwanza	13
ADABU ZA SAFARI	13
FASLU YA PILI	19
ADABU ZA ZIARA	19
FASLU YA TATU.....	22
YANAYOHUSU UMRA NA HIJJA	22
Hijja ya Uislamu:	22
Mambo yaliyo wajibu katika Umra ya Tamatui ni matano:	22
Mambo yaliyo wajibu katika Kuhirimia ni matatu:.....	22
Mambo yaliyo wajibu katika Hijja ni kumi na tatu, nayo ni kama ifuatavyo:	23
Mambo yaliyo haramu kwa aliyehirimia ni:	25
Kung'oa mti na mmea wa eneo takatifu (Haram):	26
Mambo yaliyo wajibu katika Umra ya Mufrada ni saba, nayo ni kama ifuatavyo:.....	27
FASLU YA NNE	29
MAMBO YALIYO SUNNAH KATIKA IHRAMU, TAWAFU NA KUTEMBEA BAINA YA SWAFA NA MAR'WA KATIKA UMRA	29
Kuoga:	29
Wakati wa kucaa nguo mbili za Ihram aseme:	30
Kisha asali rakaa mbili au sita Sala ya Ihram, na asome dua hii:	31
Na ni mustahabu kwenye tamko la wajibu la kuitikia (talbiya) aongeze:	33

Adabu za kuingia eneo takatifu la Makka (Haram):.....	34
Wakati wa kuingia eneo takatifu aseme:	34
Na ni mustahabu kwamba asimame mkabala na mlango wa salamu (<i>Babus-Salam</i>), na aseme:.....	35
Na katika riwaya nyiningine ni kwamba asimame kwenye mlango wa msikiti na aseme:	36
Dua Zisomwazo Katika Hali Ya Kutufu:.....	45
Dua baada tu ya kusali Sala ya Tawafu:	51
Ni mustahabu kunywa maji ya Zamzam:.....	51
Adabu za kutembea baina ya Swafa na Mar'wa:	52
Adabu za kupunguza nywele:	63
FASLU YA TANO	64
ADABU ZA IHRAMU YA HIJA, KUSIMAMA ARAFA, MASH'ARUL-HARAM, NA AMALI ZA MINA	64
Adabu za kusimama Arafa:.....	66
Adabu za kusimama al-Mash'ari:.....	77
Adabu za kutupa mawe:.....	81
Adabu za sadaka ya kuchinja:	83
Adabu za kunyoa na kupunguza:	85
Adabu za kurudi Makka kwenda kutekeleza matendo matano: 85	
Adabu za mawe matatu baada ya kurejea Mina:	87
Mambo yaliyo mustahabu huko Mina na Msikiti wa Khayfa:..	88
Mambo yaliyo mustahabu wakati wa kurudi Makka:.....	89
Amali na mambo yaliyo mustahabu kufanywa huko Makka:... 90	
Ubora wa maeneo matakatifu ndani ya Msikiti Mtukufu:	92
Mambo yaliyo mustahabu wakati wa kuingia Ka'ba Tukufu: 101	
FASLU YA SITA	110
KUYAZURU MAKABURI HUKO MAKKA	110

Ziyara ya Abdu Manafi, babu yake Mtume (s.a.w.w.):	111
Ziyara ya Abdul-Mutalib babu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):	112
Ziyara ya Abu Talib ami yake Mtume (s.a.w.w.):.....	115
Ziyara ya mama wa Mtume, Amina binti Wahb:	116
Ziyara ya Bibi Khadija Mama wa waumini:	117
Ziyara ya Ismail na Manabii wengine katika Uzio wa Ismail:	118
FASLU YA SABA	122
MAENEKO MATAKATIFU HUKO MAKKA TUKUFU	122
Dua isomwayo katika Mlima Thawru:	122
Dua ya mahali alipozaliwa Mtukufu Mtume:	123
Dua ya mahali ambapo mwezi ulipasuka:	125
Dua ya kwenye mlima wa Abu Qubaysi:	126
Dua ya nyumbani kwa Bibi Khadija (a.s.):.....	127
Kuiaga Ka'ba Tukufu:	127
Fadhila za kuzikwa katika moja ya Maeneo mawili Matakatifu (Haramaini):.....	133
Amali za mkesha wa Arafa:	134
Amali za siku ya Arafa:	154
Dua ya Imam Husain (a.s.) siku ya Arafa:.....	155
Sema mwishoni mwa mchana wa siku ya Arafa:.....	205
Ziyaratul-Jami'a:	206
Fadhila za kumzuru Husain (a.s.):.....	210
Ziyara ya Husein siku ya Arafa:.....	211
Siku ya mwezi kumi:	225
Ziyara ya Aminullah.....	226
DUA YA KUMAYL BIN ZIYAD	230

DUA ASHARATI	250
Ziyara ya Imam wa Zama hizi:	265
DUA AL-'AHAD.....	267
DUA YA ASUBUHI YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.)...	272

NENO LA MCHAPISHAJI

Kitabu kilichoko mikononi mwako ni tarjuma ya kitabu cha Kiarabu kiitwacho *Adabu 'l-Haramain* kilichoandikwa na Sayyid Jawad al-Husaini Aali Ali ash-Shahrudi. Sisi tumekiita, *Amali za Makka*.

Kitabu hiki kinaelezea mambo ya kuzingatiwa kuanzia wakati mtu anapoanza safari kwa ajili ya kuhiji na kufanya ziara (ziyara) katika mji mtukufu wa Makka (yaani adabu za ziara)

Kila safari ina taratibu zake na madhumuni yake. Kwa hiyo, msafiri hutakiwa kuzingatia utaratibu wa safari hiyo ili kufanikisha madhumuni yake. Kuhiji na kuzuru maziarata matakatifu kuna utaratibu na kanuni zake zilizowekwa kisheria, hivyo, mtu anapokwenda mji wowote mtukufu kwa ajili ya Ziara lazima ayazingatie hayo ili afanikishe madhumuni ya safari yake hiyo muhimu.

Katika kitabu hiki mwandishi ameellezea kwa lugha fasaha hatua kwa hatua kuanzia mtu kuondoka kwenda kuhiji na kufanya ziara katika mji mtukufu wa Makka mpaka anapomaliza hija na ziara yake na kurudi nyumbani. Mwandishi ameshughulikia kwa kina adabu na amali za kufanya kwa mwenye kuzuru Makka tukufu. Hata hivyo, ni matarajio yetu kwamba ataendelea kutufahamisha kuhusu adabu na amali za kufanya katika miji mingine mitukufu insha' Allah.

Kutokana na ukweli huo, Taasisi yetu ya Al-Itrah Foundation imeamua kukichapisha kitabu hiki kwa lugha ya Kiswahili kwa madhumuni yake yaleyale ya kuwahudumia Waislamu, hususan wazungumzaji wa Kiswahili.

Tunamshukuru Ndugu yetu Alhaji Hemedi Lubumba kwa kukubali jukumu hili la kukitarjumi kitabu hiki. Vilevile tunawashukuru wale wote walioshiriki kwa njia moja au nyingine hadi kufanikisha kuchapishwa kwake.

Ni matumaini yetu kwamba kitabu hiki kitakuwa ni chenye manufaa sana kwa wale wote wanaokusudia kuhiji na kufanya ziara kwa sasa na baadaye insha' Allah

Mchapishaji:

Al-Itrah Foundation

DIBAJI

Hijja ni fursa ya Umma wa Kiislamu kufikia hali ya Kiibrahim katika sekta ya kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiroho. Mwenyezi Mungu amesema: "**Hakika Nyumba ya kwanza waliyowekewa watu ni ile iliyoko Makka yenye kubarikiwa na mwongozo kwa walimwengu.**" (Sura Aali Imran: 96).

Watu wamezoea zaidi kutimiza Hijja zao kwa mwonekano wa nje katika siku za mkuatano huu wa kimungu ambao huwaleta pamoja waislamu toka pande zote za dunia bila kujali rangi zao, makabila wala mataifa na tamaduni za asili. Kwa kuwa Hijja ni mkusanyiko wa kiroho wenye kulenga kuchanua na kustawi katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu, ni vizuri mahujaji wetu wakaelewa kwamba ibada hii ni kama ibada nyingine katika kuilea jamii katika sekta zote za maisha ya kisiasa, kitamaduni na kijamii, na hivyo ni lazima tuitumie fursa hii kama Bunge la Waislamu la kimataifa na Baraza kuu la Waislamu duniani kupanga mikakati yao ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ili kwamba lengo la Ibrahim (a.s.) lidhihirike ndani ya maisha yetu ya kila siku.

Ni juu ya Waislamu ambao hubeba ujumbe wa Mungu Mwenyezi, kufaidika kisiasa na kijamii na maudhui ya Hijja, na kamwe wasiridhike na mwonekano wa nje. Lakini ni lazima watambue kwamba ibada ya kisiasa na kijamii ya Hijja inaweza kupatikana iwapo tu tutatimiza na kufikia ibada ya kimaadili na kiroho.

Mji wa jihadi ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) ni kituo muhimu ambacho chapaswa kuheshimiwa kwa mahujaji kukipa kipaumbele. Makka na eneo la makaburi matukufu ni kioo cha msingi wa matukio makubwa ya

harakati za Manabii, Uislamu na ujumbe wa Mtume Muhammad (s.a.w.w.), nalo ni eneo ambalo walifika hapo Manabii wa Mwenyezi Mungu na Jibril. Sehemu hii yatukumbusha matatizo na mazito aliyovumilia Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) katika njia ya kuusimamisha Uislamu na kuulea ubinadamu kwa muda mfupi wenyе mafanikio makubwa. Hakika uwepo wa mahujaji kwenye makaburi matukufu na maeneo matakatifu ukichukuliwa kwa mazingatio, unaonyesha wajibu mkubwa walionao katika kulinda mafanikio makubwa ya Uislamu, kwani ni mara ngapi Mtume (s.a.w.w.) kavumilia machungu na matatizo mazito kwa ajili ya haki, ni mara ngapi Maimam (a.s.) waliteseka kwa ugeni, kiu na njaa kwa ajili ya kuondoa batili. Hakika walismama kidete na imara wala hawakuyumbishwa na tuhuma na vitimbi vyaa watu mfano wa Abu Jahl, Abu Lahab, Abu Sufyan, Muawiya na hata Yazid.

Wakati wakipambana na ushetani huu na vitimbi vyao ni wakati huohuo waliendelea na harakati zao katika kuinua na kustawisha roho zao kwa Sala, Saumu, Zaka, Sadaka, Dua na tabia njema, yaani kwa ibada zote, ili kwamba ibada hizo zidhihiri katika ustawi wa uchumi wao, elimu zao, sayansi yao, teknolojia zao, utabibu wao, viwanda vyao, kilimo chao, ufugaji wao, utamaduni wao, idara zao, dola yao, uongozi wao, utawala wao, ulinzi wao, jamii zao na sekta zao zote za maisha yao, hivyo ni wajibu juu ya mahujaji kutambua falsafa ya Hijja na malengo yake ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni ili kwamba iwe ni Hijja halisi ya Ibrahim na si Hijja ya utalii, rekodi na kumbukumbu.

Faslu ya Kwanza

ADABU ZA SAFARI

Dua na adabu za safari ni nyingi, nasi hapa tutataja baadhi tu kati ya hizo:

1. **Istikhara:** Miongoni mwa adabu za safari na mambo yaliyo mustahabu kwa ajili ya safari sawa iwe ni ya Hijja au nyingineyo, ni kufanya Istikhara, na makusudio ya Istikhara ni dua na kuomba kheri kutoka kwa Mwenyezi Mungu katika kutenda jambo lolote na hasa Hijja.

Imepokewa kutoka kwa Imam al-Baqir (a.s.) kwamba alisema: “Hakika Ali bin Husein (a.s.) alikuwa akiifanya anaponusia kwenda Hijja au Umra, au kuuza au kununua au kumwacha huru mtumwa.” Na katika riwaya zetu nyingi kuna katazo la kutenda amali yoyote bila kufanya Istikhara.

Sura nzuri ya Istikhara ni aseme:

أَسْتَخِرُ اللَّهَ بِرَحْمَتِهِ خَيْرَةً فِي عَافِيَةٍ

“Namuomba Mwenyezi Mungu kheri kupitia rehema Zake katika lile lenye afya.”

Aseme hivyo mara tatu au saba au kumi au hamsini au sabini au mara mia moja. Mara zote hizo zimepokewa ndani ya Hadithi, kisha baada ya dua hii aendelee na amali yake au safari yake.

2. **Kuchagua wakati:** Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Anayetaka kusafiri

basi safari yake iwe ni siku ya jumamosi, kwani lau jiwe litadondoka toka mlimani siku ya Jumamosi basi Mwenyezi Mungu atalirudisha sehemu yake. Au siku ya Jumanne, kwani ndiyo siku ambayo Mwenyezi Mungu aliyayusha chuma kwa ajili ya Daud (a.s.). Au siku ya Alhamisi, kwani Mtume (s.a.w.w.) na masahaba zake walikuwa wakipigana ndani ya siku hii na wakashinda.”

Kuna riwaya zimepatikana zikikataza kusafiri siku ya Jumatatu, kwani ndio siku ambayo humo alifariki Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na Wahyi ukakoma. Na ndio siku aliyouawa Husain (a.s.). Na imekatazwa kusafiri siku ya Jumatano, kwani ndio siku ambayo humo zilumbwa nguzo za moto na kuangamizwa Ummah zilizotangulia. Na imekatazwa kusafiri siku ya Ijumaa kabla ya Sala. Na pia imekatazwa kusafiri siku ya tatu, ya nne, naya tano ya mwezi mwandamo.

3. **Kutoa sadaka:** Ni mustahabu kutoa sadaka kwa ajili ya safari. Na asome dua hii wakati wa kutoa sadaka hiyo:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَشْتَرِيتُ بِهَذَا الصَّدَقَةِ سَلَامَتِي وَسَلَامَةَ سَفَرِي وَمَا
مَعِي. اللَّهُمَّ وَاحْفَظْنِي وَاحْفَظْ مَا مَعِي وَسَلِّنِي وَسَلِّمْ مَا مَعِي
وَبَلِّغْنِي وَبَلِّغْ مَا مَعِي بِبِلَاغِ الْحَسْنَى الْجَيْلَ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi kupitia sadaka hii nimenunua usalama wangu na usalama wa safari yangu na wa vile vilivyo pamoja nami. Ewe Mwenyezi Mungu!

Nihifadhi na vihifadhi vile vilivyo pamoja nami, nisalimishe na visalimishe vile vilivyo pamoja nami, na kwa mafikio yako mema na mazuri nifikishe mimi pamoja na vifikishe vile vilivyo pamoja nami.”

4. **Wosia:** Ni Sunna kukabidhi Wosia wakati wa kutoka, na hasa unaohusu haki za wajibu na za kidini.
5. **Kuaga:** Atakaponua kutoka asali rakaa mbili au nne, kisha awaage wanafamilia yake na awaweke amana kwa Mola wake Mlezi, na amfanye Mwenyezi Mungu kuwa mrithi wake juu yao, aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْتَوْدِعُكَ نَفْسِي وَأَهْلِي وَمَالِي وَذْرِيقَتِي وَدُنْيَايِ
وَآخِرَتِي وَأَمَانَتِي وَخَاتَمَةَ عَبْلِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naiweka Kwako kama amana nafsi yangu, ndugu zangu, mali yangu, kizazi changu, dunia yangu, akhera yangu, amani yangu na hatima ya amali yangu.”

Imepokewa kutoka kwa as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Mtu hawezi kuacha usimamizi bora kwa ajili ya familia yake kushinda huo, na hakuna mtu aliyeuacha kupertia dua hiyo ila Mwenyezi Mungu alimpa alichoomba.”

6. **Awajulishe ndugu zake:** Imepokewa kutoka kwa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Ni haki juu ya mwislamu atakapo kusafiri awajulishe ndugu zake, na ni haki juu ya ndugu zake atakaporejea waende kumlaki.”

- Ni Sunna kusoma dua na Sura zilizofundishwa na Ahlul-Baiti, awekapo tu mguu katika kipando aseme:

سبحان الذي سخر لنا هذَا و ما كنَّا لَهُ مُقْرِنِينَ.

“Ametakasika Yeye aliyetutiishia haya na tusingeliweza kutenda haya wenyewe.”

Kisha aseme mara saba:

سبحان الله والحمد لله ولا إله إلا الله

“Ametakasika Mwenyezi Mungu, na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, na hapana mungu ila Mwenyezi Mungu.”

Na dua nyinginezo mionganoni mwa zile zilizofundishwa na Ahlul-Baiti.

- Kuwasakiwa wasafiri wenzake:** Awasakiwa wasafiri wenzake na awatangulie katika kutekeleza haja kwa kadiri aewazavyo, na wala asipuuze kujitolea kwa juhudhi zake katika kuwakidhia haja zao ili Mwenyezi Mungu amwondolee matatizo yake na amwepushe hapa duniani na huzuni na shida, na ili amwondolee shida adhimu siku ya Kiyama. Na imekuja katika hadithi kwamba: “Ndugu mbaya mno safarini ni yule ambaye ana uwezo wa kuwasaidia wengine lakini hawasakiii na bado anasubiri wengine wamsaidie.” Na kuna msisitizo wa kwamba awe mvumilivu kwa ndugu zake na awe na maadili mema kwao.

- 9. Atekeleze Sala ndani ya wakati wake:** Azingatie safarini kutekeleza Sala za wajibu mwanzo wa wakati, na iwapo sehemu na mazingira vitamlazimu kuwafuata Masunni katika Sala basi asipuuzie kufanya hivyo.

Inapasa kwa mwenye kwenda Hijja anapokuwa anakwenda Hijja nia yake iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, kiasi kwamba asiichanganye na malengo mengine ya kidunia, na wala sababu ya kwenda Hijja isiwe ila ni kutekeleza amri ya Mwenyezi Mungu, kupata thawabu Zake na kuijokoa na moto Wake. Ajihadhari sana kwamba asiwe na sababu nydingine ya siri moyoni mwake, kama vile kujionyesha kwa watu, kujiadhari na tuhuma za watu na kushutumiwa kwa uovu iwapo hatakwenda Hijja, au kuhofia ufakiri na mali kuharibika iwapo hatokwenda Hijja, kama ilivyo mashuhuri kwamba mwenye kuacha kwenda Hijja atapata balaa la ufakiri na kurudi nyuma kiuchumi, au awe amekusudia kufanya biashara au shughuli nydingine. Hayo yote hukitoa kitendo katika wigo wa ikhlasi na hukizua kutoa faida na kupata thawabu zilizoahidiwa kwacho.

Ni ujinga ulioje! Kuvumilia matendo mazito ambayo kwayo unaweza kupata mafanikio mema kwa ajili ya ndoto zisizo na faida ambazo hazisababishi chochote ila hasara. Hivyo ajitolee juhudhi zake zote kwa kuifanya azma yake iwe ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu tu, iliyo mbali na kila aina ya kujionyesha kwa watu na kutaka kusifiwa. Na awe na yakini kwamba kusudio lake na amali yake havitokubaliwa ila iwapo tu ni mwenye ikhlasi, na kwamba uchafu mbaya mno ni kuiende Nyumba ya Mfalme (Allah) na eneo lake tukufu ilihali anayekusudiwa ni mwingine (si Allah). Aisahihishe azma yake nafsini

mwake, na kuisahihisha ni kuwa na ikhlasi kwa kujiepusha na kila aina ya kujionyesha na kutaka kusifiwa.

Atubie kwa Mwenyezi Mungu kwa toba halisi, na aadhimishe ndani ya nafsi yake hadhi ya Nyumba na hadhi ya Mola Mlezi wa Nyumba. Aiepushe nafsi yake na kila chenye kuushughulisha moyo wake, mpaka iwe hamu yake ni Mwenyezi Mungu tu, na moyo uwe umetulia umejielekeza kwa Mwenyezi Mungu na ukiadhimisha alama zake.

Masurufu yake yawe ni ya halali na awasaide wengine masurufu hayo kwa moyo mkunjufu, asinung'unike kwa kutoa na kuwapa wengine, bali nafsi yake iwe radhi kwa hilo, kwani kutoa mali kwa ajili ya Hijja ni kutoa mali katika njia ya Mwenyezi Mungu, na dirhamu moja atoayo hapo ni sawa na kutoa dirhamu mia saba.

Awe na maadili mema na maneno mazuri, akithirishe unyenyekevu na ajiepushe na maadili mabaya na maneno machafu. Awe aliye rafurafu asiyejjipamba, na asiwe ni mwenye kuelemea kwenye mambo yanayopelekea ufahari na kujilimbikizia mali ili asije kuandikwa katika orodha ya wenyewe kiburi na kutolewa kwenye kundi la wanyonge masikini.

FASLU YA PILI

ADABU ZA ZIARA

Adabu zinazopasa kutekelezwa maeneo matakatifu na kwenye makaburi matukufu ni nyingi mno, nasi hapa tutataja baadhi tu, nazo ni:

1. Kuoga unapokusudia kwenda kumzuru Mtume (s.a.w.w.) na Maimam (a.s.).
2. Kuwa katika hali ya tohara dhidi ya najisi, hadathi ndogo na hadathi kubwa.
3. Avae nguo yenyе tohara na safi, na ni Sunna kwamba iwe mpya na nyeupe.
4. Atembee kwa hatua fupi fupi aelekeapo kwenye eneo tukufu, atembee kwa utulivu na unyenyekevu na hali ni mwenye hofu na aliyeinamisha kichwa chini na bila kugeuka huku na huku.
5. Asijinukize manukato ila tu aendapo kulizuru kaburi la Husain.
6. Aendapo kufanya Ziara aushughulishe ulimi wake kwa Takbira, Tasbihi, Tahlili, Tamjidi na kumsalia Mtume na aali zake.
7. Asimame kwenye mlango wa kuingilia eneo takatifu na aanze kuomba idhini ya kuingia kupitia mafundisho yaliyofundishwa na Ahlul-Baiti. Ajitahidi kuleta hali ya unyenyekevu na kuishiwa nguvu, ajiweke kama mtu aliye mbele ya hadhara ya mheshimiwa, na kwamba (huyo mheshimiwa)

anamuona, anasikia maneno yake na anamjibu salamu yake, kama zithibitishavyo hilo Ziyara¹ mbalimbali zilizofunzwa na Ahlul-Baiti. Atafakari huruma yao na mapenzi yao kwa wafuasi wao na kwa wale wenye kuwazuru. Atafakari kuhusu uharibifu wa nafsi yake, kuwatenga kwake, kukataa kwake mafunzo yao mengi na yale maudhi aliyowatendea wao, wafuasi wao na vipenzi vyao. Akijitazama mwenyewe mtazamo wa kutafakari na umakini basi nyayo zake zitashindwa kutembea, moyo wake utapatwa na hofu na hatimaye macho yake yatatokwa na machozi. Na huu ndio moyo hasa wa adabu zote za Ziara.

Na Ziara muhimu kushinda zote ni kumzuru Mtume (s.a.w.w.) na hasa kwa mahujaji, na kuna hadithi nyingi zikihimiza hilo, na hapa tutatosheka na hadithi moja. Imepokewa katika kitabu *al-Wasa'il* kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: "Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alisema: 'Atakayekuja Makka kwa ajili ya Hijra na akawa hakunizuru mimi huko Madina, nitamnyanyapaa Siku ya Kiyama. Na atakayekuja kunizuru basi atawajibikiwa kupata Shufaa yangu, na atakayewajibikiwa kupata Shufaa yangu atawajibikiwa kuingia peponi. Na atakayekufa na hali akiwa katika hali ya kuhamia kwa Mwenyezi Mungu atafufuliwa Siku ya

¹ Haya ni maneno anayotamka au kuyasoma yule mwenye kufanya Ziara. Ama neno Ziara lenyewe linamaanisha shughuli nzima ya kumzuru marehemu, kama inavyosema Kamusi ya Kiswahili Sanifu, toleo la pili la Oxford University: "Ziara: 1- Ni tendo la kwenda mahala patakatifu kufanya kisomo au tendo maalumu la kidini. 2- Kaburi.)" – Mtarjumu.

Kiyama pamoja na watu wa Badri.””

Mwenyezi Mungu anasema: “**Na bila shaka una tabia njema, tukufu.**” (Sura al-Qalami: 4).

Na Mwenyezi Mungu anasema: “**Bila shaka amekufikieni Mtume kutoka mionganoni mwenu, yanamhuzunisha yanayokutaabisheni, anakuhangaikieni, kwa Waumini ni Mpole, Mwenye kurehemu.**” (Sura Tawba: 128).

FASLU YA TATU

YANAYOHUSU UMRA NA HIJJA

Hapa tutataja kwa muhtasari mambo yaliyo wajibu katika Umra na Hijja, na ni juu ya mukalafu kurejea kwa Marjaa wake ili achukue matendo ya ibada hiyo.

Hijja ya Uislamu:

Inakamilika kwa ibada mbili, ya kwanza huitwa Umra na ya pili huitwa Hijja, na kuna wakati ibada ya pili huitwa Hijja ya Tamatui. Na ni lazima kutekeleza kipengele cha Umra kabla ya kile cha Hijja.

Mambo yaliyo wajibu katika Umra ya Tamatui ni matano:

Kwanza: Kuhirimia kuanzia moja ya vituo.

Pili: Kutufu.

Tatu: Rakaa mbili nyuma ya Maqam Ibrahim (a.s.) za Sala ya Tawafu.

Nne: Kutembea baina Swafa na Mar'wa.

Tano: Kupunguza nywele.

Mambo yaliyo wajibu katika Kuhirimia ni matatu:

Kwanza: Kuvalaa nguo ya Ihramu.

Pili: Niya, nayo ni kujikurubisha kwa Allah, na iambatane na uanzaji wa ibada hiyo, na suala la kuainisha baina ya

ihramu ya Umra au ya Hijja linarejea kwa mtu mwenyewe

Tatu: Tamko la kuitikia (Talbiya), nalo ni:

لَبَيِّكَ اللَّهُمَّ لَبَيِّكَ، لَبَيِّكَ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَيِّكَ، إِنَّ الْحَمْدَ

وَالنِّعْمَةُ لَكَ وَالْمُلْكُ لَا شَرِيكَ لَكَ لَبَيِّكَ

“Labeika! Ewe Mwenyezi Mungu Labeika! Labeika! hauna mshirika Labeika! hakika sifa njema na neema ni Zako na ufalme pia, hauna mshirika Labeika! ”

Mambo yaliyo wajibu katika Hijja ni kumi na tatu, nayo ni kama ifuatavyo:

1. Kuhirimia kuanzia Makka, na bora ni ahirimie kuanzia Msikiti Mtukufu, na bora ni kuanzia kwenye Jiwe la Ismail au Maqam Ibrahim (a.s.), na tayari umeshajifunza mambo yaliyo wajibu katika ihramu katika matendo ya Umra.
2. Kusimama Arafa kuanzia kukengeuka kwa jua kwa siku ya mwezi tisa mpaka kuingia kwa magharibi.
3. Kusimama Muzdalifa Siku ya Idi al-Udh'ha, kuanzia alfajri mpaka kuchomoza kwa jua.
4. Kumtupia shetani mawe huko Mina Siku ya Iddi, na wakati wake ni kuanzia mwanzo wa kuchomoza jua mpaka kuzama kwa jua.
5. Kuchinja Siku ya Idi huko Mina.

6. Kunyoa au kupunguza nywele au kucha huko Mina. Na kwa hilo huwa halali kwake yale yaliyokuwa haramu kwake kutokana na iheramu, isipokuwa mke na manukato, bali pia uwindaji kwa tahadhari kwa mujibu wa baadhi. Na hiki kitendo huitwa kihalalishi cha kwanza.
7. Tawafu ya ziara, baada ya kurejea Makka.
8. Sala ya Tawafu kama ilivyotangulia kwenye Tawafu ya Umra.
9. Kutembea baina ya Safa na Mar'wa. Na kwa kitendo hicho huwa halali kwake yale yaliyokuwa haramu kwake kutokana na iheramu, isipokuwa mke. Na kitendo hiki huitwa kihalalishi cha pili.
10. Tawafu Nisaa.
11. Sala ya Tawafu Nisaa. Na kwa kitendo hiki mke huwa halali kwake pia. Kama ambavyo lau kama mwanamke atatufu na kusali Sala ya Tawafu hiyo mumewe huwa halali kwake. Na hiki ndio kihalalishi cha tatu kwa wanasharia wa Kiislamu, na lililo mashuhuri kwao ni kwamba maeneo halalishi ni matatu. Ndio, hubakia uharamu wa kuwinda mpaka adhuhuri ya mwezi kumi na tatu kwa mujibu wa tahadhari kwa baadhi ya wanasharia wa kiislamu.
12. Kulala Mina usiku wa mwezi kumi na moja, wa kumi na mbili bali na wa mwezi kumi na tatu katika baadhi ya sura.
13. Kurusha mawe matatu siku ya mwezi kumi na moja, bali kwa tahadhari na mwezi kumi na tatu iwapo

mukalafu atalala hapo.

Mambo yaliyo haramu kwa aliyeirimia ni:

Mtu atakapohirimia ni haramu juu yake mambo ishirini na tano:

1. Kuwinda mnyama wa nchi kavu.
2. Kujamiana na mwanamke.
3. Kumbusu mwanamke.
4. Kumgusa mwanamke kwa matamanio.
5. Kumtizama mwanamke kwa matamanio na kumchezea.
6. Kujitoa manii.
7. Kufunga ndoa, pia kuwa shahidi wa ndoa na yanayohusu ndoa.
8. Kutumia manukato.
9. Kuvaal nguo iliyoshonwa, hii ni kwa wanaume.
10. Kupaka wanja.
11. Kujitizama kwenye kioo.
12. Kuvaal khofu na soksi, hii ni kwa wanaume. Inasemekana ni kwa wanawake pia.
13. Kufanya ufasiki, nao ni uongo, kutukana na kujifakharisha.

14. Kuapa, nako ni kusema: “Hapana wallahi! ” au “Ndio wallahi” au tamko lingine.
15. Kuuwa wadudu wanaoshambulia mwili kama vile chawa na mfano wake.
16. Kujipodoa.
17. Kujipaka mafuta.
18. Kung’oa unywele toka mwilini.
19. Kufunika kichwa, hii ni kwa wanaume.
20. Kufunika uso, hii ni kwa wanawake.
21. Kutembea chini ya kivuli, hii ni kwa wanaume.
22. Kujitoa damu mwilini.
23. Kukata kucha.
24. Kung’oa jino.
25. Kubeba silaha.

Kung’oa mtı̄ na mmea wa eneo takatifu (Haram):

Mpaka hapa yamekwisha mambo ambayo ni haramu kwa aliyeirimia kuyatenda, na kuna mambo mengine ambayo ni haramu kwa aliye katika ihramu na yule asiyé katika ihramu, nayo ni mambo mawili: Kwanza ni kuwinda eneo takatifu, hiyo ni haramu kwa aliye katika ihramu na yule asiyé katika ihramu. La pili ni kung’oa aina yoyote ya mmea katika eneo takatifu au kukata mtı̄ na kinginecho, ila katika maeneo yaliyotajwa sehemu yake.

Mambo yaliyo wajibu katika Umra ya Mufrada ni saba, nayo ni kama ifuatavyo:

1. Kuhirimia, na tayari umeshajua kuwa kunatimia kwa kuvaan nguo mbili za Ihram, niya na tamko la kuitikia(*Talbiya*).
2. Kuitufu Nyumba mara saba.
3. Kusali Sala ya Tawafu katika Maqam Ibrahim (a.s.).
4. Kutembea baina ya Safa na Mar'wa.
5. Kupunguza au kunyoa nywele.
6. Kutufu Tawafu Nisaa kwa kuizunguka Ka'ba mara saba.
7. Sala ya Tawafu Nisaa, kama ilivyotangulia kwenye Tawafu ya Umra.

Umra ya Mufrada inasihi katika miezi yote, na bora mno ni katika mwezi wa Rajabu na baada yake ni Ramadhani. Ama Umra ya Tamatui, yenewe haipatikani ila katika miezi ya Hijja, nayo ni Shawali, Dhul-Qa'dah na Dhul-Hijja. Na inaruhusiwa kuhirimia kwa ajili ya Umra Mufrada katika vituo vilevile ambavyo unahirimia kwa ajili ya Umra Tamatui. Mukalafu akiwa Makka na akataka kufanya Umra Mufrada inajuzu kwake kutoka nje ya mipaka ya eneo tukufu (Haram) na ahirimie akiwa nje ya eneo tukufu (Haram), wala si wajibu juu yake kurejea kwenye vituo na kuhirimia kuanzia hapo. Na bora ni kwamba kuhirimia kwake kuwe ni kuanzia Hudaybiya au al-Ja'ranatah au at-Taniimi.

Umra ya Mufrada ni wajibu kwa yule anayetaka kuingia Makka, kwani haijuzu kwake kuingia humo ila akiwa ni mwenye kuhirimia. Katika hukumu hiyo anavuliwa yule tu ambaye anaingia na kutoka mara kwa mara, kama vile mkusanya kuni na mvuna majani, na pia anavuliwa yule ambaye ametoka Makka baada ya kuwa ametimiza matendo yake ya Hijja au baada ya Umra ya Mufrada, hakika yeye anaruhusiwa kurudi Makka bila kuhirimia, ikiwa ni kabla ya kupita mwezi mzima.

FASLU YA NNE

MAMBO YALIYO SUNNAH KATIKA IHRAMU, TAWAFU NA KUTEMBEA BAINA YA SWAFA NA MAR'WA KATIKA UMRA

Nayo ni mengi, tutataja baadhi tu:

Kuoga:

Ni mustahabu kuoga kwa ajili ya Ihram na asome dua hii wakati wa kuoga:

بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ. أَللَّهُمَّ اجْعَلْنَا لِنُورٍ وَطَهُورًا وَحِرْزًا وَأَمْنًا مِنْ كُلِّ خَوْفٍ، وَشِفَاءً مِنْ كُلِّ دَاعٍ وَسُقُمٍ. أَللَّهُمَّ طَهِّرْنِي وَطَهِّرْلِي قَلْبِي، وَأَشْرَحْلِي صَدْرِي، وَأَجْرِعْلِي لِسَانِي مَحَبَّتَكَ وَمِدْحَاتَكَ وَالثَّنَاءَ عَلَيْكَ، فَإِنَّهُ لَا قُوَّةَ لِإِلَّا بِكَ، وَقَدْ عَلِمْتُ أَنَّ قِوَامَ دِينِي التَّسْلِيمُ لِأَمْرِكَ، وَالإِتِّبَاعُ لِسُنْنَةِ نَبِيِّكَ، صَلَواتُكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu na naapa kwa Mwenyezi Mungu! Ewe Mwenyezi Mungu! Lifanye nuru kwangu, tohara, kinga na amani dhidi ya kila hofu, na tiba ya kila gongwa na ugonjwa. Ewe Mwenyezi Mungu! Nitakase na utakase moyo wangu, kipanue kifua changu, na pitisha juu ya ulimi wangu mapenzi Yako, himidi Yako na sifa Zako, kwani hakika sina nguvu ila kupitia Kwako, na tayari nimeshajua kwamba hakika kunyooka kwa dini yangu ni

kujisalimisha Kwako na kufuata Sunnah za Nabii Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake.”

Wakati wa kuваяа nguo mbili za Ihram aseme:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي رَزَقَنِي مَا أُوْرِى بِهِ عَوْرَقٍ، وَأَعْدَى بِهِ فَرَّطٍ،
وَأَعْبَدُ فِيهِ رَبِّي، وَأَتُّهِي فِيهِ إِلٰى مَا أَمَرْنِي، الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي
قَصَدْتُهُ فَبَلَغْنِي، وَأَرَدْتُهُ فَأَعْانَنِي وَقَبِلْنِي، وَلَمْ يَقْطَعْ بِي
وَوْجْهُهُ، أَرَدْتُ فَسَلَّنِي، فَهُوَ حِصْنِي وَكَهْفِي وَحِرْزِي وَظَهْرِي
وَمَلَادِي وَمَلْجَئِي وَمَنْجَائِي وَذُخْرِي وَعُدَّقِي فِي شِدَّقِي وَرَحَائِي

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye ameniruzuku kile ninachotumia kuusitiri utupu wangu, kutekelezea faradhi yangu, kumwabudia Mola Wangu Mlezi na kuyafikia yale aliyoniamuru. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye nimemkusudia Naye akanifikisha, nimemtaka Naye akanisaidia na akanipokea na hajaondoa Uso Wake kwangu, na nimetaka Naye akanisalimisha, hivyo Yeye ndiye ngome yangu, tegemeo langu, kinga yangu, mgongo wangu, hifadhi yangu, kimbilio langu, uokovu wangu, akiba yangu na maandalizi yangu wakati wa shida yangu na raha yangu.”

**Kisha asali rakaa mbili au sita Sala ya Ihram, na
asome dua hii:**

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَنِي مِنْ اسْتَجَابَ لَكَ وَآمِنَ بِوَعْدِكَ
وَاتَّبِعْ أَمْرَكَ فِيْ عَبْدِكَ وَفِيْ قَبْضَتِكَ لَاْ أُوقِنُ إِلَّاْ مَا وَقَيْتَ وَلَاْ أَخْذُ
إِلَّاْ مَا أُعْطَيْتَ وَقَدْ ذَكَرْتُ الْحَجَّ فَأَسْأَلُكَ أَنْ تَعْزِمْ لِي عَلَيْهِ عَلَىْ
كِتَابِكَ وَسَنَةِ نَبِيِّكَ صَلَوَاتُكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَتَقْوِينِي عَلَىْ مَا
ضَعَفَتْ عَنْهُ وَتَسْلِمَ مَثْنَىْ مَنَاسِكِ فِيْ يَسِيرٍ مِنْكَ وَعَافِيَةَ
وَاجْعَلْنِي مِنْ وَفْدِكَ الَّذِي رَضِيَتْ وَارْتَضَيْتَ وَسَيِّئَتْ وَكَتَبْتَ
اللَّهُمَّ إِنِّي خَرَجْتُ مِنْ شَقَّةَ بَعِيدَةَ وَأَنْفَقْتَ مَالِي ابْتِغَاءَ
مَرْضَاتِكَ اللَّهُمَّ فَتَسِّمْ لِي حَجَّتِي وَعَمِيقَ اللَّهُمَّ إِنِّي أَرِيدُ التَّمَّتُّ
بِالْعِرْبَةِ إِلَى الْحَجَّ عَلَى كِتَابِكَ وَسَنَةِ نَبِيِّكَ صَلَوَاتُكَ عَلَيْهِ وَآلِهِ
فِيْ إِنْ عَرَضَ لِيْ عَارِضَ يَحْبِسَنِي فَخَلَّنِي حِيثَ حَبَسْتَنِي بِقَدْرِكَ
الَّذِي قَدِرْتَ عَلَى اللَّهُمَّ إِنْ لَمْ تَكُنْ حَجَّةَ فَعِرْبَةَ أَحْرَمَ لَكَ
شَعْرِيْ وَبَشْرِيْ وَلَحْيِيْ وَدَمِيْ وَعَظَامِيْ وَمَتْنِيْ وَعَصَبِيْ مِنَ النِّسَاءِ

والثياب والطيب أبتنى بذالك وجهك والدار الآخرة

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba unijaalie niwe mionganoni mwa waliokujibu, akaamini ahadi Yako na akafuata amri Yako, kwani hakika mimi ni mja Wako na nimo mikononi Mwako, sikingwi ila na yale uliyokinga na wala sichukui ila uliyotoa. Bila shaka umeitaja Hijja hivyo nakuomba unipe azma juu yake kwa mujibu wa Kitabu Chako na Sunnah ya Nabii Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake, na unipe nguvu juu ya yale niliyo dhaifu kwayo, na upokee toka kwangu ibada zangu za Hijja kwa wepesi toka Kwako na afya, na nijaaliye mionganoni mwa ugeni Wako ambao umeuridhia, umeuteua, umeupa jina na umeuandika.

Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimetoka ardhi ya mbali na nimetao mali kwa ajili ya kutafuta radhi Zako. Ewe Mwenyezi Mungu! Nitimizie Hijja yangu na Umra yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nataka kustarehe kwa Umra mpaka Hijja kwa mujibu wa Kitabu Chako na Sunnah ya Nabii Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake, hivyo iwapo nitatokewa na lolote litakalonizuia basi nitowe kizuizini kama ulivyoniweka kizuizini kwa makadara Yako uliyokadiria juu yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Ikiwa si Hijja basi ni Umra ndio iliyoharamisha kwa ajili Yako nywele zangu, ngozi yangu, nyama yangu, damu yangu, mifupa yangu, ubongo wangu na mishipa yangu dhidi ya wanawake, nguo na manukato. Nafanya hivyo nikitafuta ridhaa Yako na nyumba ya Akhera.”

Na ni mustahabu kwenye tamko la wajibu la kuitikia (talbiya) aongeze:

لَبَّيْكَ ذَا الْمَعَارِجِ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ دَاعِيًّا إِلَى دَارِ السَّلَامِ لَبَّيْكَ،
لَبَّيْكَ غَفَارَ الدُّنُوبِ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ أَهُلَ التَّلْبِيَةِ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ ذَا
الْجَلَالِ وَالْأَكْرَامِ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ تُبَدِّيُ وَالْمَعَادُ إِلَيْكَ لَبَّيْكَ،
لَبَّيْكَ تَسْتَغْنِي وَيُفْتَقِرُ إِلَيْكَ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ مَرْهُوبًا وَمَرْغُوبًا
إِلَيْكَ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ إِلَهُ الْحَقِّ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ ذَا التَّعْمَاءِ وَالْفَضْلِ
الْحَسَنِ الْجِيلِ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ كَشَافَ الْكُرْبَابِ الْعِظَامِ لَبَّيْكَ
لَبَّيْكَ عَبْدُكَ وَابْنُ عَبْدِكَ لَبَّيْكَ، لَبَّيْكَ يَا كَرِيمُ لَبَّيْكَ

“Labaika! Mwenye utukufu mkubwa Labaika! Labaika!
Mwenye kuitia kwenye nyumba ya amani Labaika!
Labaika! Mwenye kughufuri dhambiLabaika! Labaika!
Mwenye kustahiki kuitikiwa Labaika! Labaika! Mwenye
utukufu na ukarimu Labaika! Labaika! Unaanzisha na
marejeo ni Kwako Labaika! Labaika! Unajitosheleza na
unahitajiwa Labaika! Labaika! Ewe Ambaye chenyne
kuraghibiwa na kuogopwa kipo Kwako Labaika! Labaika!
Mungu wa haki Labaika! Labaika! Mwenye neema na
fadhila njema na nzuri Labaika! Labaika! Mwenye
kuondoa matatizo makubwa Labaika! Labaika! Mimi ni
mja Wako na mwana wa waja Wako Labaika! Labaika!
Ewe Mkarimu Labaika! ”

Adabu za kuingia eneo takatifu la Makka (Haram):

Wakati wa kuingia eneo takatifu aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي قُلْتَ فِي كِتَابِكَ الْمُنْزَلِ وَقَوْلُكَ الْحَقُّ : « وَأَذْنُ فِي النَّاسِ بِالْحِجَّةِ يَأْتُوكَ رِجَالًا وَعَلَى كُلِّ ضَامِرٍ يَأْتِينَ مِنْ كُلِّ فَجَّ عَيْقٍ » ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَرْجُو أَنْ أَكُونَ مِنَ أَجَابَ دُعَوَاتَكَ ، وَقَدْ جِئْتُ مِنْ شُقَّةَ بَعِيدَةٍ وَ مِنْ فَجَّ عَيْقٍ ، سَامِعًا لِنِدَايَكَ ، وَ مُسْتَجِيبًا لَكَ ، مُطِيعًا لِأَمْرِكَ ، وَ كُلُّ ذَلِكَ بِفَضْلِكَ عَلَيَّ وَإِحْسَانِكَ إِلَيَّ ، فَلَكَ الْحَمْدُ عَلَى مَا وَقَعْتَنِي لَهُ ، أَبْتَغَى بِنِدِيكَ الرُّلْفَةَ عِنْدَكَ ، وَ الْقُرْبَةَ إِلَيْكَ ، وَ الْمُسْنَدَةَ لَدَيْكَ ، وَ الْمُغْفِرَةَ لِذُنُوبِي ، وَ التَّوْبَةَ عَلَى مَنْهَا بِنِيكَ ، اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ ، وَ حِرْمَمْ بَدَنِي عَلَى النَّارِ ، وَ آمِنِي مِنْ عَذَابِكَ وَ عِقَابِكَ ، بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe umesema katika kitabu Chako na kauli Yako ni haki: “**Na utangaze kwa watu habari za Hijja watakujia kwa miguu na juu ya kila mnyama wakija toka kila njia ya mbali.**” Ewe

Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nataraji kuwa mionganoni mwa yule aliyejibu wito Wako na nimekuja toka ardhi ya mbali na njia ya mbali nikiwa ni mwenye kusikia wito Wako na mwenye kukujibu Wewe na mwenye kutii amri Yako, na hayo yote ni kwa fadhila Zako zilizopo juu yangu na ihsani Yako kwangu, hivyo una kila sifa njema kwa yale uliyonifakisha nikitafuta kwayo daraja Kwako, ukaribu Kwako, cheo Kwako, kughufiriwa dhambi zangu na kusamehewa kwa ukarimu Wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na uharamishie moto mwili wangu, na nisalimishe na adhabu Yako na mateso Yako, kwa rehema Zako ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Na ni mustahabu kwamba asimame mkabala na mlango wa salamu (*Babus-Salam*), na aseme:

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّهَا النِّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ
وَمِنَ اللَّهِ وَما شاءَ اللَّهُ، وَالسَّلَامُ عَلَى أَنْبِياءِ اللَّهِ وَرُسُلِهِ
السَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ وَآلِهِ، السَّلَامُ عَلَى إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ اللَّهِ،
وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ

“Amani iwe juu yako ewe Nabii na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake, kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa haki ya Mwenyezi Mungu, kutoka kwa Mwenyezi Mungu na alivyotaka Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Manabii wa Mwenyezi Mungu na Mitume Wake! Amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na aali

zake! Amani iwe juu ya Ibrahim khalili wa Mwenyezi Mungu! Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe wote.”

Na katika riwaya nyingine ni kwamba asimame kwenye mlango wa msikiti na aseme:

بِسْمِ اللَّهِ وَبِبِاللَّهِ وَمِنَ اللَّهِ وَإِلَى اللَّهِ وَمَا شَاءَ اللَّهُ وَعَلَى مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَخَيْرُ الْأَسْمَاءِ لِلَّهِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ، وَالسَّلَامُ عَلَى رَسُولِ اللَّهِ، أَلْسَلَامُ عَلَى مُحَمَّدٍ بْنِ عَبْدِ اللَّهِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ أَيُّهَا النَّبِيُّ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَّكَاتُهُ، أَلْسَلَامُ عَلَى أَنْبِياءِ اللَّهِ وَرُسُلِهِ، أَلْسَلَامُ عَلَى إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ الرَّحْمَانِ، أَلْسَلَامُ عَلَى الْمُرْسَلِينَ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، أَلْسَلَامُ عَلَيْنَا وَعَلَى عِبَادِ اللَّهِ الصَّالِحِينَ

أَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَأَرْحَمْ مُحَمَّدًا وَآلَ مُحَمَّدٍ. كَمَا صَلَّيْتَ وَبَارَكْتَ مُحَمَّدًا، وَتَرَحَّمْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ وَآلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَيْيٌ مَجِيدٌ. أَللَّهُمَّ

صَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ، وَعَلَى إِبْرَاهِيمَ
 خَلِيلِكَ وَعَلَى أَنْبِيائِكَ وَرُسُلِكَ وَسَلِّمَ عَلَيْهِمْ، وَسَلَامٌ عَلَى
 الْمُرْسَلِينَ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، أَللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ
 رَحْمَتِكَ، وَاسْتَعْبِلْنِي فِي طَاعَاتِكَ وَمَرْضَاكَ، وَاحْفَظْنِي بِحِفْظِ
 الْأَيْمَانِ أَبْدًا مَا أَبْقَيْتِنِي، جَلَّ شَنَاءً وَجُهَّاكَ، أَلْحَمْ لِلَّهِ الَّذِي
 جَعَلَنِي مِنْ وَفْدِهِ وَزُوْارِهِ، وَجَعَلَنِي مِنَّ مَنْ يَعْبُرُ مَسَاجِدَهُ،
 وَجَعَلَنِي مِنَّ مَنْ يُنَاجِيهِ

أَللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ وَزَاعِرُكَ فِي بَيْتِكَ، وَعَلَى كُلِّ مَا تَقْرَبُ
 حَقَّ لِيَنْ أَتَاهُ وَزَارَهُ، وَأَنْتَ خَيْرُ مَا مَلَأْتِ وَأَكْرَمُ مَمْزُورِ، فَأَسْأَلُكَ يَا أَللَّهُ يَا رَحْمَانُ
 بِأَنَّكَ أَنْتَ أَنْتَ اللَّهُ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، وَحْدَكَ لَا شَرِيكَ لَكَ، بِأَنَّكَ
 وَاحِدٌ أَحَدٌ صَمَدٌ، لَمْ تَلِدْ وَلَمْ تُولَدْ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ كُفُواً أَحَدٌ، وَأَنَّ
 مُحَمَّدًا عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَعَلَى أَهْلِ
 بَيْتِهِ، يَا جَوَادُ يَا مَاجِدُ يَا جَبَّارُ يَا كَرِيمُ، أَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ

تُحَفَّتَكَ إِلَيْاَيِ بِنِيَارَقِي إِلَيْاَكَ أَوَّلَ شَيْءٍ تُعْطِيَنِي فَكَاكَ رَقَبَتِي مِنَ

النَّارِ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa haki ya Mwenyezi Mungu, kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kuelekea kwa Mwenyezi Mungu, alivyotaka Mwenyezi Mungu, kwa mujibu wa mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na juu ya aali zake, jina bora kushinda yote ni la Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu.

“Na amani iwe juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu ya Muhammad bin Abdillah! Amani iwe juu yako ewe Nabii na rehema za Mwenyezi Mungu na baraka Zake! Amani iwe juu ya Manabii wa Mwenyezi Mungu na Mitume Wake! Amani iwe juu ya Ibrahim khalili wa Rahman! Amani iwe juu ya Mitume! Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe wote. Amani iwe juu yetu na juu ya waja wema wa Mwenyezi Mungu!

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na mbariki Muhammad na aali Muhammad na mrehemu Muhammad na aali Muhammad kama ulivyomsalia, ulivyombariki na kumrehemu Ibrahim na aali Ibrahim, hakika Wewe ni mhimidiwa msifika. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad mja Wako na Mtume Wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Ibrahim khalili Wako na Manabii Wako na Mitume Wako na uwasalimie! Na amani iwe juu ya Mitume! Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe wote. Ewe Mwenyezi Mungu nifungulie milango

ya rehema Zako, nishughulisse katika kukutii Wewe na katika ridhaa Yako, na nihifadhi kwa hifadhi ya imani muda wote utakaonibakisha hai, ewe Ambaye zimetukuka sifa za utukufu Wako. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amenijaalia kuwa mionganini mwa ugeni Wake na mazuwari (wenye kuzuru) Wake, na amenijaalia kuwa mwenye kuimarisha misikiti Yake na amenijaalia kuwa mwenye kusema Naye kwa siri.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako na ni mwenye kukuzuru katika nyumba Yako, na kila mwenye kuijiwa ana haki ya yule aliyemjia na kumzuru, na Wewe ni mbora kushinda wote wenye kuijiwa na ni mkarimu kushinda wote wenye kutembelewa, hivyo nakuomba ewe Allah. Ewe Rahman! Kwa kuwa hakika Wewe ni Allah hapana mungu ila Wewe Mmoja usiye na mshirika, na kwa kuwa hakika Wewe ni Mmoja wa pekee Mkusudiwa kwa haja, hujazaa wala hujazaliwa wala huna ye yeyote unayefanana naye, na kwa hakika Muhammad ni mja Wako na Mtume Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya watu wa nyumba yake, ewe Mkarimu! Ewe Mkarimu! Ewe Msifika! Ewe Jabari! Ewe Mkarimu! Nakuomba ujaalie zawadi Yako kwangu kwa kule kukuzuru Wewe na jambo la kwanzaa utakalonipa, liwe ni kunikomboa na moto.

Kisha aseme mara tatu:

أَللّٰهُمَّ فُكْ رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nikomboe na moto.”

Kisha aseme:

وَ أَوْسِعْ عَلَىٰ مِنْ رِنْقِكَ الْحَلَالِ الطَّيِّبِ، وَادْرَأْ عَنِّي شَرَّ
شَيَاطِينِ الْإِنْسَنِ وَالْجِنِّ وَشَرَّفَسَقَةِ الْعَرَبِ وَالْعَجَمِ

“Na nipanulie riziki Yako ya halali iliyio nzuri, na niondolee shari ya mashetani wa kibinadamu na kimajini, na shari ya mafasiki wa kiarabu na wasio waarabu.”

Kisha aingie msikitini na aseme:

بِسْمِ اللَّهِ وَبِاللَّهِ وَعَلَىٰ مِلَّةِ رَسُولِ اللَّهِ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ،

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa haki ya Mwenyezi Mungu, na kwa mujibu wa mila ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.).”

Kisha inua mikono yako miwili mbinguni hali ukiwa umeelekea Ka’ba, na useme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ فِي مَقَامِ هَذَا، فِي أَوَّلِ مَنَاسِكِي أَنْ تَقْبِلَ
تَوْبَتِي، وَأَنْ تَجَاوِزَ عَنِّي خَطِيئَتِي وَتَضَعَّعَ عَنِّي وِرْبَانِي، الْحَمْدُ لِلَّهِ
الَّذِي بَلَغَنِي بَيْتَهُ الْحَمَامُ. اللَّهُمَّ إِنِّي أَشْهَدُ أَنَّ هَذَا بَيْتُكَ
الْحَامُ الَّذِي جَعَلْتَهُ مَثَابَةً لِلنَّاسِ وَأَمْنًا مُبَارَكًا وَهُدًى
لِلْعَالَمِينَ. اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، وَالْبَدَدُ بَدْدُكَ، وَالْبَيْتَ بَيْتُكَ،

جِئْتُ أَطْلُبُ رَحْمَتَكَ، وَأَعْمَرُ طَاعَتَكَ، مُطِيعًا لِأَمْرِكَ، راضِيًّا
 بِقَدَرِكَ، أَسْأَلُكَ مَسْأَلَةَ الْبُضْرَى إِلَيْكَ الْخَائِفُ لِعَقْوَبَتِكَ.
 أَللَّهُمَّ افْتَحْ لِي أَبْوَابَ رَحْمَتِكَ، وَاسْتَغْبِلْنِي بِطَاعَتِكَ
 وَمَرْضَا تِكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba katika kisimamo changu hiki na mwanzo wa ibada zangu za Hijja ukubali toba yangu na ufumbie macho makosa yangu na uniondolee mzigo wangu. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amenifikasiha nyumba Yake tukufu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nashahidilia kwamba hakika hii ni Nyumba Yako ambayo umeifanya kuwa marejeo ya watu na mahala pa amani, yenyе kubarikiwa na mwongozo kwa viumbe.

Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako na mji huu ni mji Wako na Nyumba hii ni nyumba Yako, nimekuja nikitafuta rehema Zako na nikitanguliza utiifu Kwako, ni mwenye kutii amri Yako na mwenye kuridhia makadara Yako. Nakuomba maombi ya mwenye kukimbilia Kwako mwenye kuogopa adhabu Yako. Ewe Mwenyezi Mungu! Nifungulie milango ya rehema Zako na nishughulishe katika kukutii Wewe na katika radhi Zako.”

Kisha itazame Ka’ba na useme:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي عَظَمَكِ وَشَرَفَكِ وَجَعَلَكِ مَثَابَةً لِلنَّاسِ وَأَمْنًا

مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amekutukuza, amekusharifu, amekupa heshima na amekufanya marejeo ya watu na mahala pa amani, penye kubarikiwa na mwongozo kwa viumbe.”

Kisha nenda kwenye Jiwe Jeusi na liguse na kusema:

أَلْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي هَدَانَا لِهَذَا وَمَا كُنَّا لِنَهْتَدِي لَوْلَا أَنْ
هَدَانَا اللَّهُ، سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، أَكْبَرُ
مِنْ خَلْقِهِ، وَأَكْبَرُ مِنْ أَخْشَى وَأَحْذَرُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ
لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْبُدْلُكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، يُحِبِّي وَيُبَيِّنُ،
وَيُبَيِّنُ وَيُحِبِّي، وَهُوَ حِيٌّ لَا يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ عَ
قِدِيرٌ. أَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَبَارِكْ عَلَى مُحَمَّدٍ
وَآلِ مُحَمَّدٍ، كَافُضِلِ مَا صَلَّيْتَ وَبَارَكْتَ وَتَرَحَّبْتَ عَلَى إِبْرَاهِيمَ
وَآلِ إِبْرَاهِيمَ، إِنَّكَ حَيْيٌ مَحِيدٌ، وَسَلَامٌ عَلَى جَمِيعِ النَّبِيِّينَ
وَالْمُرْسَلِينَ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ. أَللَّهُمَّ إِنِّي أُوْمِنُ

بِوَعْدِكَ، وَأَصَدِّقُ رُسُلَكَ، وَأَتِّبِعُ كِتَابَكَ

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye ametuongoza kufikia haya wala hatukuwa wenyewe kuongoka kama Mwenyezi Mungu hakutuongoza. Ametakasika Mwenyezi Mungu! Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, na hakuna mungu ila Allah, na Mwenyezi Mungu ni mkubwa mno! Mkubwa mno kushinda viumbe Wake! Mwenyezi Mungu ni mkubwa mno kushinda ninachoogopa na kujihadhari nacho. Hakuna mungu ila Allah Mmoja wa pekee asiye na mshirika, ana ufalme na ana sifa njema, anahuisha na kufisha, anafisha na kuhuisha, Naye ni Mzima wa milele, heri imo mikononi Mwake na Yeye juu ya kila kitu ni muweza.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na mbariki Muhammad na aali Muhammad kama sala bora uliyomsalia na kumbariki na kumrehemu Ibrahim na aali Ibrahim, hakika Wewe ni Mhimidiwa Msifika. Na amani iwe juu ya Manabii wote na Mitume na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa viumbe wote. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi naamini ahadi Yako, nawasadikisha Mitume Wako na ninafuata Kitabu Chako.”

Na katika riwaya sahihi kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) ni kwamba: “Utakapolikaribia Jiwe Jeusi inua mikono yako na mhimidi Mwenyezi Mungu na kumtukuza, mswalie Mtume na muombe Mwenyezi Mungu akubali toka kwako. Kisha liguse kwa mkono wako Jiwe Jeusi na libusu, na kama hutawezeku kulibusu basi liguse tu kwa mkono wako, na kama hutawezeku kuligusa kwa mkono wako basi liashirie, na sema:

أَللّٰهُمَّ أَمَانَتِي أَدِيْتُهَا وَمِيشَاقِ تَعَاهَدْتُهُ لِتَشَهِّدَ لِي بِالْمُوافَاتِ،
 أَللّٰهُمَّ تَصْدِيقًا بِكِتَابِكَ وَعَلَى سُنْنَةِ نَبِيِّكَ، أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا
 اللّٰهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ، آمَنْتُ
 بِإِلَهِهِ، وَكَفَرْتُ بِالْجِبْرِ وَالْطَّاغُوتِ وَبِالْلَّاتِ وَالْعُزَّى، وَعِبَادَةِ
 الشَّيْطَانِ، وَعِبَادَةِ كُلِّ نَدِيدٍ عَنِ الْمُنْدِدِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Amana yangu nimeitekeleza na ahadi yangu nimeitimiza ili initolee ushahidi kwamba nimetekeleza. Ewe Mwenyezi Mungu! Kwa ajili ya kusadikisha Kitabu Chako na kufuata Sunnah ya Nabii Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake, nashahidilia kwamba hapana mungu ila Allah, Mmoja wa pekee hana mshirika, na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake. Nimemwamini Mwenyezi Mungu na nimelikufuru sanamu na shetani, Lata na Uzza, ibada ya mashetani na ibada ya kila mshirika ambaye anaombwa kinyume na Mwenyezi Mungu.”

Ikiwa hauwezi kusema haya, basi sema baadhi yake na useme:

أَللّٰهُمَّ إِلَيْكَ بَسَطْتُ يَدِي وَفِيهَا عِنْدَكَ عَطَيْتُ رَغْبَتِي فَاقْبِلْ
 سُبْحَاتِي، وَاغْفِنِي وَارْحَنِي، أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْكُفَّارِ

وَالْفَقْرُ وَمَوَاقِفُ الْخِزْنِي فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nimenyoosha mkono wangu Kwako na raghba yangu ya kutamani yaliyopo Kwako imekuwa kubwa, hivyo nikubalie tasbihi yangu, nighufirie na kunirehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najikinga Kwako dhidi ya ukafiri, ufakiri na visimamo vya hizaya duniani na Akhera.”

Dua Zisomwazo Katika Hali Ya Kutufu:

Na ili mwenye kutufu asipatwe na shaka juu ya idadi ya mizunguko basi katika kila mzunguko mmoja wa tawafu yake asome dua hizi zilizopokewa kutoka kwa Maimamu (a.s.) kwa nia ya kupata radhi, hata kama ni kwa kurudia:

Dua ya mzunguko wa kwanza:

أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ الَّذِي يُعْشِي بِهِ عَلٰى طَلَلِ الْبَاعِ، كَمَا
يُعْشِي بِهِ عَلٰى جَدَادِ الْأَرْضِ، وَأَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ الَّذِي يَهْتَرِئُ لَهُ
عَرْشُكَ، وَأَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ الَّذِي تَهْتَرِئُ لَهُ أَقْدَامُ مَلَائِكَتِكَ،
وَأَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ الَّذِي دَعَاكَ بِهِ مُوسَى مِنْ جَانِبِ الطُّورِ،
فَاسْتَجَبْتَ لَهُ، وَأَلْقَيْتَ عَلَيْهِ مَحَبَّةً مِنْكَ، وَأَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ
الَّذِي غَفَرْتَ بِهِ لِمُحَمَّدٍ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ مَا تَقدَّمَ مِنْ

ذَنْبِهِ وَمَا تَأْخَرَ، وَأَتَيْتَ عَلَيْهِ نِعْمَتَكَ، أَنْ تَرْزُقَنِي خَيْرَ الدُّنْيَا

وَالْآخِرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kwa jina Lako ambalo kwalo hutembeza juu ya vivuli vya maji kama ambavyo hutembeza juu ya misitari ya ardhi. Na ninakuomba kwa jina Lako ambalo Arshi Yako hutikisika kwa ajili yake. Na ninakuomba kwa jina Lako ambalo nyayo za Malaika Wako hutikisika kwa ajili yake. Na ninakuomba kwa jina Lako ambalo kwalo Musa alikuomba toka upande wa mlima Nawe ukamjibu na ukaweka mapenzi juu yake toka Kwako. Na ninakuomba kwa jina Lako ambalo kwalo ulimghufiria Muhammad (s.a.w.w.) dhambi zake zilizotangulia na zijazo, na ukamtumizia neema Yako, uniruzuku heri ya dunia na Akhera. “

Kisha omba haja yako.

Dua ya mzunguko wa pili:

اللّٰهُمَّ إِنِّي إِلَيْكَ فَقِيرٌ، وَإِنِّي خَائِفٌ مُسْتَجِيرٌ، فَلَا تُغَيِّرْ جِسْمِي
وَلَا تُبَدِّلِ اسْمِي سَاعِدْكَ فَقِيرِكَ، مِسْكِينْكَ بِبَابِكَ، فَتَصَدَّقُ
عَلَيْهِ بِالْجَنَّةِ. اللّٰهُمَّ الْبَيْتُ بَيْتُكَ، وَالْحَرَمٌ حَرَمُكَ، وَالْعَبْدُ
عَبْدُكَ، وَهَذَا مَقَامُ الْعَائِدِ الْمُسْتَجِيرِ بِكَ مِنَ النَّارِ،

فَأَعْتَقْنِي وَالِدَّى وَأَهْلِى وَوُلْدِى وَإِخْرَانِ الْبُؤْمِنِينَ مِنَ النَّارِ
يَا جَوَادُ يَا كَرِيمُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mhitaji Kwako, na hakika mimi ni mwenye hofu mwenye kuomba hifadhi, hivyo usiubadili mwili wangu wala usilibadili jina langu.Mwombaji Wako, fakiri Wako na maskini Wako yupo mlangoni Kwako, mzawadie pepo. Ewe Mwenyezi Mungu! Nyumba hii ni nyumba Yako, eneo hili tukufu ni eneo Lako na mja huyu ni mja Wako, na hiki ni kisimamo cha mwenye kujikinga Kwako na mwenye kuomba hifadhi Kwako dhidi ya moto hivyo nikomboe na moto mimi na wazazi wangu wawili, ndugu zangu, kizazi changu na ndugu zangu waumini, ewe Mkarimu ewe Mkarimu.”

Dua ya mzunguko wa tatu:

أَللّٰهُمَّ أَدْخِلْنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ، وَأَجِرْنِي بِرَحْمَتِكَ مِنَ النَّارِ
وَاعافِنِي مِنَ السُّقُمِ، وَأَوْسِعْ عَلَيَّ مِنَ الرِّزْقِ الْحَلَالِ، وَادْرِأْ
عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْأَنْسِ، وَشَرَّ فَسَقَةِ الْعَرَبِ وَالْعَجَمِ، يَا ذَا
الْبَنِ وَالْطَّوْلِ، وَالْجُودِ وَالْكَرَمِ، إِنَّ عَلَيِّ ضَعْفٌ فَضَاعِفْهُ
لِي، وَتَقَبَّلْهُ مِنِّي، إِنَّكَ أَنْتَ السَّمِيعُ الْعَلِيمُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Niingize peponi kwa rehema

Zako na niepushe na moto kwa rehema Zako, nipe afya njema dhidi ya ugonjwa na nipanulie riziki ya halali na niondolee shari za mafasiki wa kijini na kibinadamu na shari ya mafasiki wa kiarabu na wasiokuwa waarabu. Ewe Mwenye neema na uwezo, fadhila na ukarimu! Hakika amali yangu ni dhaifu hivyo iongeze kwa ajili yangu na ipokee toka kwangu, hakika Wewe ni Msikivu, Mjuzi.”

Dua ya mzunguko wa nne:

يَا اللَّهُ يَا وَلِيَ الْعَافِيَةِ، وَخَالِقَ الْعَافِيَةِ، وَرَازِقَ
الْعَافِيَةِ، وَالْمُنْعَمَ بِالْعَافِيَةِ، وَالْمَنَانَ بِالْعَافِيَةِ، وَالْمُتَفَضِّلُ
بِالْعَافِيَةِ عَلَى وَعَلَى جَيِيعِ خَلْقِكَ، يَا رَحْمَانَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ
وَرَحِيمَهُمَا، صَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَأَرْسَلَنَا الْعَافِيَةَ، وَ
دَوَامَ الْعَافِيَةَ، وَتَامَ الْعَافِيَةَ، وَشُكْرُ الْعَافِيَةِ فِي الدُّنْيَا
وَالْآخِرَةِ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mmliki wa afya, Muumba wa afya, Mwenye kuruzuku afya, Mwenye kuneemesha afya, Mpaji wa afya na Mwenye kunifadhili afya mimi na viumbe Wako wote! Ewe Mwenye sikitiko duniani na Akhera na uliyehu Rahimu humo! Msalie Muhammad na aali Muhammad, na turuzuku afya, kudumu katika afya, utimilifu wa afya na kushukuru afya duniani na Akhera, kwa rehema Zako ewe Mwenye kurehemu kushinda wote

wenye kurehemu.”

Dua ya mzunguko wa tano:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ شَفِّٰعٰكَ وَعَظِّٰمٰكَ، وَالْحَمْدُ لِلّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ بَعَثَ مُحَمَّداً نَبِيًّاً، وَجَعَلَ عَلٰيًّا إِمَاماً أَلَّهُمَّ اهْدِ لَهُ خِيَارَ خَلْقِكَ،
وَجَنِّبْهُ شَرَارَ خَلْقِكَ. رَبَّنَا آتَنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَ فِي الْآخِرَةِ
حَسَنَةً وَ قِنَاعَذَابَ النَّارِ

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amekupa heshima na amekutukuza. Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amemleta Muhammad Nabii na amemfanya Ali Imam. Ewe Mwenyezi Mungu! Waongoze kwake walio bora kati ya viumbe Wako na mwepushe na wale walio waovu mionganini mwa viumbe Wako. Mola wetu Mlezi! Utupe wema duniani na wema katika Akhera na utulinde na adhabu ya Moto.”

Dua ya mzunguko wa sita:

أَلَّهُمَّ أَبْيَثْ بَيْتَكَ، وَالْعَبْدُ عَبْدُكَ، وَهَذَا مَقَامُ الْعَائِذِ بِكَ
مِنَ النَّارِ أَلَّهُمَّ مِنْ قَبْلِكَ الرَّوْحُ وَالْفَرْجُ وَالْعَافِيَةُ. أَلَّهُمَّ إِنَّ
عَمَلِي ضَعِيفٌ فَضَاعَفْهُ لِي، وَاغْفِرْ لِي مَا أَطْلَعْتَ عَلَيْهِ مِنِّي وَخَفِي

عَلَى خَلْقِكَ، أَسْتَجِيرُ بِاللّٰهِ مِنَ النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nyumba hii ni nyumba Yako, mja huyu ni mja Wako na hiki ni kisimamo cha aliyejikinga Kwako na moto. Ewe Mwenyezi Mungu! Rehema, faraja na afya ni kutoka Kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika amali yangu ni dhaifu hivyo iongeze kwa ajili yangu na unighufirie yale uliyoyajua toka kwangu na yakafichika kwa viumbe Wako. Naomba hifadhi kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya moto.”

Dua ya mzunguko wa saba:

اللّٰهُمَّ إِنِّي عِنْدِي أَفْواجٌ مِّنْ ذُنُوبٍ، وَأَفْواجٌ مِّنْ خَطَايَا وَعِنْدَكَ
أَفْواجٌ مِّنْ رَحْمَةٍ، وَأَفْواجٌ مِّنْ مَغْفِرَةٍ، يَا مَنِ اسْتَجَابَ لِأَبْغَضِ
خَلْقِهِ إِلَيْهِ إِذْ قَالَ أَنْظِرْنِي إِلَى يَوْمِ يُعَشَّونَ، إِسْتَجِبْ لِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika kwangu kuna makundi mengi ya dhambi na makundi mengi ya makosa, na Kwako kuna makundi mengi ya rehema na makundi mengi ya maghfira. Ewe Ambaye alimjibu kiumbe amchukiaye zaidi kushinda wote pale aliposema: Nipe muda mpaka siku watakapofufuliwa! Nijibu.”

Kisha sema:

اللّٰهُمَّ قَنْعَنِي بِسَارَقَتِنِي، وَبَارِكْ لِي فِيمَا آتَيْتِنِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nikinaishe nayale uliyoniruzuku na niwekee baraka katika yale uliyonipa.”

Dua baada tu ya kusali Sala ya Tawafu:

اللّٰهُمَّ تَقْبَلُ مِنِّي، وَلَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنِّي، الْحَمْدُ لِلّٰهِ
بِسَاحِمِدِهِ كُلُّهَا عَلٰى نَعْبَائِهِ كُلُّهَا، حَتّٰى يَتَتَّهِ الْحَمْدُ إِلٰى مَا
يُحِبُّ رَبِّي وَيَرِضِي. اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ، وَتَقْبَلُ مِنِّي،
وَطَهِّرْ قِلْبِي، وَزَكِّ عَمَلِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Pokea toka kwangu na wala usifanye hii kuwa ahadi ya mwisho toka kwangu. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa himidi Zake zote juu ya neema Zake zote mpaka kila sifa njema ya Mwenyezi Mungu ikomee kwenye lile alipendalo na kuliridhia. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad na pokea toka kwangu na utakase moyo wangu na itakase amali yangu.”

Ni mustahabu kunywa maji ya Zamzam:

Ni Sunnah kunywa maji ya Zamzam na kujirushia kichwani mwake na mwilini na kusoma dua hii:

اللّٰهُمَّ اجْعَلْهُ عَلٰيْا نَافِعًا، وَرُزْقًا وَاسِعًا، وَشِفَاءً مِنْ كُلِّ دَاءٍ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Yafanye elimu yenyе manufaa,

riziki pana na tiba ya kila ugonjwa.”

Abul-Hasan (a.s.) alikuwa akisema anywapo maji ya Zamzam:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu, na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu na shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu.”

Imepokewa kutoka katika kitabu *al-Mahasin* kutoka kwa Mtume (s.a.w.w.) kwamba alisema: “Maji ya Zamzam ni dawa ya ugonjwa utakaokunywa kwa ajili yake.” Na ni mustahabu kuyanywa kwa wingi na kuyajaza kwa wingi. Na Mtume alikuwa akituma aletewe zawadi ya maji ya Zamzam naye akiwa Madina.

Na amepokea Hammad kwamba jamaa miongoni mwa ulamaa walikuwa wakiyanywa kwa ajili ya mambo muhimu ikiwemo kupata elimu, kukidhiwa haja, kuponywa na maradhi, na mengineyo. Na muhimu zaidi ni kuomba maghfira toka kwa Mwenyezi Mungu, hivyo asome Bismillahi na anuwiye kuyanywa kwa kuomba maghfira na kufuzu kupata Pepo na uokovu dhidi ya moto na mengineyo. Na ni mustahabu kuyabeba na kuyatoa zawadi.

Adabu za kutembea baina ya Swafa na Mar’wa:

Ni mustahabu kwenda Swafa kwa kutokea mlanga ambao alitokea Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) nao ni ule mlanga ambao upo mkabala na Jiwe Jeusi, kwa sasa unaitwa Mlango wa Swafa. Aende kwa utulivu na unyenyekevu, apande juu ya Mlima Swafa mpaka awe

anaiona Nyumba, na aeletee kwenye nguzo ambayo lipo Jiwe Jeusi. Na ni mustahabu kwamba arefushe kisimamo juu ya Mlima Swafa. Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: “Ambaye anataka mali yake iongezeke basi arefushe kusimama juu ya Mlima Swafa na Mlima Mar’wa, na akumbuke neema za Mwenyezi Mungu zilizopo juu yake, na ataje neema zake na mitihani yake na wema Wake kwake kwa kadiri awezavyo.”

Aseme mara saba akiwa ameelekea Ka’aba:

اللَّهُ أَكْبَرُ

Mwenyezi Mungu mkubwa!

Mara saba:

الْحَمْدُ لِلَّهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu.

Mara saba:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ

Hapana mungu ila Allah.

Na asome dua hii mara tatu:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْبُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، يُحْبِي

وَبِيْتُ، وَهُوَ حَمّْ لَا يَبُوتُ، بِيْدِهِ الْخَيْرُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ
 أَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ،

“Hakuna mungu ila Allah mmoja wa pekee asiyé na mshirika, ana ufalme na ana sifa njema, anahuisha na kufisha, Naye ni mzima wa milele hafi, na Yeye ni Muweza juu ya kila kitu. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad.”

Na asome dua hii mara tatu:

أَللَّهُ أَكْبَرُ عَلَى مَا هَدَانَا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى مَا أَبْلَانَا، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ
 الْحَمْدُ لِلَّهِ الْقَيُّومِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ الْحَمْدُ الدَّائِمِ

“Mungu mkubwa kwa yale aliyo tuongoza. Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa yale aliyo tuneemesha. Na kila sifa njema ni Mwenyezi Mungu aliye Mzima Mwenye kusimamia mambo. Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Mzima wa milele.”

Na asome dua hii mara tatu:

أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَشْهُدُ أَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ
 لَا نَعْبُدُ إِلَّا إِيَّاهُ، مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ، وَلَوْ كَرِهَ الْمُشْرِكُونَ

“Nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah, na

nashahidilia kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake, hatumwabudu ila Yeye kwa kumtakasia Yeye dini hata kama washirikina watachukia.”

Na asome dua hii mara tatu:

اللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ الْعَفْوَ وَالْعَافِيَةَ وَالْيَقِينَ فِي الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba msamaha, afya na yakini duniani na Akhera.”

Na mara tatu:

اللّٰهُمَّ آتِنَا فِي الدُّنْيَا حَسَنَةً وَ فِي الْآخِرَةِ حَسَنَةً وَ قِنَا عَذَابَ

النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Utupe wema duniani na wema katika Akhera na utulinde na adhabu ya Moto.”

Na mara mia moja:

اللّٰهُ أَكْبَرُ

Mwenyezi Mungu mkubwa.

Na mara mia moja:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللّٰهُ

Hakuna mungu ila Allah.

Na mara mia moja:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ

Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu.

Na mara mia moja:

سُبْحَانَ اللّٰهِ

Ametakasika Mwenyezi Mungu!

Kisha asome:

لَا إِلٰهَ إِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهُ، أَنْجَزَ وَعْدَهُ، وَنَصَرَ عَبْدَهُ، وَغَلَبَ الْأَخْرَابَ
وَحْدَهُ، فَلَهُ الْبُدْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ وَحْدَهُ . أَللّٰهُمَّ بارِكْ لِي فِي الْمَوْتِ
وَفِيهَا بَعْدَ الْمَوْتِ . أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ ظُلْمَةِ الْقَبْرِ وَ حُشْتِهِ .
أَللّٰهُمَّ أَظِلْنِي فِي ظِلِّ عَرْشِكَ يَوْمًا لَا ظِلَّ إِلَّا ظِلُّكَ

“Hakuna mungu ila Allah Mmoja wa pekee, ametekeleza ahadi yake, amemnusuru mja wake na ameyashinda makundi peke yake. Ana ufalme na ana kila sifa njema peke Yake. Ewe Mwenyezi Mungu! Nibariki mimi katika mauti na baada ya mauti. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika

mimi najilinda Kwako na giza la kaburi na upweke wake. Ewe Mwenyezi Mungu! Niweke kwenye kivuli cha Arshi Yako siku ambayo hakutakuwa na kivuli ila kivuli Chako.”

Kariri dua hii kwani ni ya kuiweka amana dini yako na nafsi yako Kwake:

أَسْتَوْدِعُ اللَّهَ الرَّحْمَنَ الرَّحِيمَ الَّذِي لَا تَضِيَعُ وَدَائِعُهُ دِينِي
وَنَفْسِي وَأَهْلِي. أَللَّهُمَّ اسْتَغْفِلْنِي عَلَى كِتَابِكَ وَسُنْنَةِ نَبِيِّكَ،
وَتَوَفَّنِي عَلَى مِلَّتِهِ، وَأَعِذْنِي مِنَ الْفِتْنَةِ

“Naiweka dini yangu, nafsi yangu na ndugu zangu amana kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu ambaye amana zake hazipotei. Ewe Mwenyezi Mungu! Nishughulishe kwa kufuata Kitabu Chako na Sunnah ya Nabii Wako na unifishe juu ya mila yake na unilinde na fitina.”

Kisha sema mara tatu:

اللهُ أَكْبَر

Mwenyezi Mungu mkubwa.

Kisha arudie mara mbili dua ya kujiweka amana, kisha aseme:

اللهُ أَكْبَر

Mwenyezi Mungu mkubwa.

Kisha aombe tena mara moja ile dua ya kujiweka amana. Na kama hawezi utaratibu huu basi atosheke na kidogo.

Na ni mustahabu kwamba aielekee Ka’ba, anyanyuwe mikono yake na aseme:

اللَّهُمَّ اغْفِرْ لِي كُلَّ ذَنْبٍ أَذْتُ بِنَتْهُ قَطْ، فَإِنْ عُدْتُ فَعُدْ عَلَىَّ
بِالْمَغْفِرَةِ، فَإِنَّكَ أَنْتَ الْغَفُورُ الرَّحِيمُ. اللَّهُمَّ افْعُلْ بِي مَا أَنْتَ
أَهْلُهُ، فَإِنَّكَ إِنْ تَفْعَلْ بِي مَا أَنْتَ أَهْلُهُ تَرْحَمِنِي، وَإِنْ تُعَذِّبِنِي
فَأَنْتَ غَنِّيٌّ عَنْ عَذَابِي، وَأَنَا مُحْتَاجٌ إِلَى رَحْمَتِكَ، فَيَا مَنْ أَنَا
مُحْتَاجٌ إِلَى رَحْمَتِهِ إِرْحَمِنِي. اللَّهُمَّ لَا تَفْعَلْ بِي مَا أَنَا أَهْلُهُ، فَإِنَّكَ
إِنْ تَفْعَلْ بِي مَا أَنَا أَهْلُهُ تُعَذِّبِنِي، وَلَمْ تَظْلِمْنِي، أَصْبَحْتُ أَتَقِيَّ
عَذَالَكَ، وَلَا أَخَافُ جَوَارَكَ، فَيَا مَنْ هُوَ عَدْلٌ لَا يَجُورُ إِرْحَمِنِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nighufirie kila dhambi niliyoitenda, na kama nitarudia basi Nawe nirudie kwa maghfira, kwani hakika Wewe ni Msamehevu, Mwenye sikitiko. Ewe Mwenyezi Mungu! Nitendee yale unayostahiki Wewe kwani hakika ikiwa utanitendea yale unayostahiki Wewe utanirehemu, na Wewe huna haja na adhabu yangu hata kama utaniadhibu, lakini mimi ni mwenye kuhitaji rehema Zako, hivyo ewe Ambaye mimi

nahitaji rehema Zake nirehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Usinitendee yale ninayostahili mimi kwani hakika ukinitendea yale ninayostahili mimi utaniadhibu na hutakuwa umenidhulumu. Nimepambazukiwa na hali ninajikinga na uadilifu Wako na wala siogopi uonevu Wako, hivyo ewe Ambaye ni Uadilifu usiyeonea nirehemu.”

Kisha aseme:

يَا مَنْ لَا يَخِبُّ سَائِلُهُ، وَلَا يَنْفَدُ نَائِلُهُ، صَلَّى اللَّهُ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ
مُحَمَّدٍ، وَأَعُذُّنِي مِنَ النَّارِ بِرَحْمَتِكَ

“Ewe Ambaye hamrudishi mikono mitupu muombaji Wake na wala haliishi gawo Lake! Msalie Muhammad na aali Muhammad na nilinde na moto kwa rehema Zako.”

Jiombee utakalo, na urefushe kusimama kwako juu ya Mlima wa Swafa kwa mara ya kwanza kuliko mara nyingine. Kisha teremka kidogo na simama, na soma dua hii hali umeelekea Ka’ba:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ وَفِتْنَتِهِ وَغُرْبَتِهِ وَوَحْشَتِهِ
وَظُلْمَتِهِ وَضِيقَهِ وَضَنْكِهِ。اللَّهُمَّ أَظِلِّنِي فِي ظَلَّلٍ عَنْ شَكَّ يَوْمٍ لَا
ظِلَّ لِإِلَّا ظِلَّكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najilinda Kwako na

adhabu ya kaburi, mitihani yake, ugeni wake, upweke wake, giza lake, mbinyo wake na shida zake. Ewe Mwenyezi Mungu! Niweke kwenye kivuli cha Arshi Yako siku ambayo hakutakuwa na kivuli ila kivuli Chako.”

Kisha teremka na hali umefunua mgongo wako na soma dua hii wakati wa kuteremka toka Mlima Swafa:

يَا رَبَّ الْعَفْوِ، يَا مَنْ أَمَرَ بِالْعَفْوِ، يَا مَنْ هُوَ أَوْلَى بِالْعَفْوِ، يَا مَنْ
يُشَيِّبُ عَلَى الْعَفْوِ، الْعَفْوَ الْعَفْوَ الْعَفْوَ، يَا جَوَادُ يَا كَرِيمُ يَا قَرِيبُ، يَا
بَعِيدُ، أُرْدُدْ عَلَى نِعْتَكَ، وَاسْتَغْمِلْنِي بِطَاعَتِكَ وَمَرْضَاتِكَ

“Ewe Mola Mlezi wa msamaha! Ewe Ambaye aliamuru msamaha! Ewe Ambaye anafaa zaidi kusamehe! Ewe Ambaye hulipa thawabu za msamaha, naomba msamaha, naomba msamaha, naomba msamaha, ewe Mkarimu! Ewe Mkarimu! Ewe Uliye karibu! Ewe Uliye mbali! Nirudishie neema Zako na unishughulishe katika kukutii Wewe na katika maridhawa Yako.”

Kisha utatembea kwa utulivu na unyenyekevu mpaka ufile eneo la mwendo wa kasi, na haifai kwa wanawake kutembea mwendo wa kasi. Na ni mustahabu kusoma dua hii eneo la mwendo wa kasi:

بِسْمِ اللَّهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ. أَللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، أَللَّهُمَّ
أَغْفِرْ وَارْحَمْ وَتَجَاوِزْ عَنَّا تَعْلَمُ، إِنَّكَ أَنْتَ الْأَعَزُّ الْأَكْرَمُ، وَاهْدِنِي

لِلَّهِيْ تِيْ هِيْ أَقْوَمُ. أَلَّهُمَّ إِنَّ عَمَلِي ضَعِيفٌ فَضَاعِفْهُ لِي، وَتَقْبَلْ
 مِنِّي. أَلَّهُمَّ لَكَ سَعْيِي، وَبِكَ حَوْلِي وَقُوَّتِي، تَقْبَلْ عَمَلِي، يَا مَنْ
 يَقْبَلُ عَمَلَ الْمُتَّقِينَ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni Mkubwa. Ewe Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad na aali Muhammad. Ewe Mwenyezi Mungu! Samehe, rehemu na fumbia macho yale unayoyajua, kwani hakika Wewe ni Mtukufu mno Mkarimu zaidi, na niongoze kwenye lile lililo la sawa. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika amali yangu ni dhaifu hivyo iongeze kwa ajili yangu na ipokee toka kwangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Matembezi yangu ni kwa ajili Yako, ujanja wangu na nguvu zangu ni Kwako, ipokee amali yangu ewe Ambaye anapokea amali za wachamungu.”

Ukivuka eneo la mwendo wa kasi, kata mwendo wa kasi na tembea kwa utulivu na unyenyekevu, na soma dua hii:

يَا ذَا الْبَنِ وَالْفَضْلِ وَالْكَرِمِ وَالثَّغْبَاءِ وَالْجُودِ، اغْفِرْ لِي ذُنُوبِي، إِنَّهُ
 لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبُ إِلَّا أَنْتَ

“Ewe Mwenye upaji, fadhila, ihsani, neema na ukarimu! Nighufirie madhambi yangu kwani hakika haghufirii dhambi ila Wewe.”

Mpaka utakapofika Mlima wa Mar'wa, upande na tenda kama ulivyotenda juu ya Mlima wa Swafa, muombe Mwenyezi Mungu haja zako na sema katika dua yako:

يَا مَنْ أَمْرَبِ الْعَفْوِ، يَا مَنْ يَجْزِي عَلَى الْعَفْوِ، يَا مَنْ دَلَّ عَلَى
الْعَفْوِ، يَا مَنْ زَيَّنَ الْعَفْوَ يَا مَنْ يُثِيبُ عَلَى الْعَفْوِ، يَا مَنْ يُحِبُّ
الْعَفْوَ، يَا مَنْ يُعْطِي عَلَى الْعَفْوِ، يَا مَنْ يَغْفُو عَلَى الْعَفْوِ، يَا رَبَّ
الْعَفْوِ، الْعَفْوَ الْعَفْوَ الْعَفْوَ،

“Ewe Ambaye aliamuru msamaha! Ewe Ambaye hulipa kutohana na msamaha! Ewe Ambaye alijulisha msamaha! Ewe Ambaye aliupamba msamaha! Ewe Ambaye hulipa thawabu za msamaha! Ewe anayependa msamaha! Ewe Ambaye hutoa kwa ajili ya msamaha! Ewe Ambaye hutoa msamaha juu ya msamaha! Ewe Mola Mlezi wa msamaha! naomba msamaha, naomba msamaha, naomba msamaha.”

Jinyenyekeze kwa Mwenyezi Mungu na lia, na kama huwezi kulia basi jilize, na jitahidi utokwe na machozi, na jitahidi kuomba dua. Na rejea Swafa toka Mar'wa kwa utaratibu huu. Na soma dua hii katika hali ya matembezi kwani ni dua bora mno:

أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ حُسْنَ الظِّنِّ بِكَ عَلَى كُلِّ حَالٍ، وَصِدْقَ النِّيَّةِ
فِي التَّوْكِلِ عَلَيْكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba hali ya kuwa na dhana nzuri Nawe katika kila hali, na nia njema katika kukutawakali Wewe.

Adabu za kupunguza nywele:

Ni Sunnah kufanya haya kwa pamoja: Kupunguza nywele za kichwani, ndevu, masharubu na kukata kucha, na kutopindukia ili kibakie kiwango fulani kwa ajili ya Hijja. Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: “Ukimaliza matembezi yako (baina ya Swafa na Mar’wa) na hali ukiwa katika Hijja*Tamatui* basi punguza nywele zako tokea pande zake, ndevu zako na masharubu yako, na kata kucha zako na acha kidogo kwa ajili ya Hijja yako. Ukifanya hivyo utakuwa umehalalisha kila kitu ambacho ni halali kwa aliye katika ihramu ambacho ulikuwa umeharamisha...”

FASLU YA TANO

ADABU ZA IHRAMU YA HIJA, KUSIMAMA ARAFA, MASH'ARUL-HARAM, NA AMALI ZA MINA

Adabu zilizotangulia zinazohusu Ihramu ya Umra zinaingia pia katika Ihramu ya Hijja. Na ni bora Ihramu iwe baada ya Sala ya Adhuhuri au Alasiri au faradhi iliyosaliwa kadha au Sala ya Sunnah, na uchache wake ni rakaa mbili. Na bora isaliwe ndani ya Msikiti Mtukufu, na bora iwe katika Jiwe la Ismail au Maqam Ibrahim. Na ni mustahabu kuitamka nia na ulete tamko la kuitikia (Talbiya) ambalo tumetangulia kulitaja katika Umra ila ni kwamba badala ya kauli yako:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَرِيدُ التَّمَتعَ بِالْعُمْرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nataka kufanya Umra Tamattui”

sema:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَرِيدُ الْحَجَّ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nataka kuhiji.

Utakapohirimia kwa ajili ya Hijja na ukawa unatoka Makka basi njiani utakuwa unasoma tamko la kuitikia (Talbiya) kwa sauti ya chini mpaka utakapofika Abtahi, ndipo utanyanya sauti yako. Na utakapoelekea Mina utasema:

اللَّهُمَّ إِيَّاكَ أَرْجُو وَإِيَّاكَ أَدْعُو، فَبَلَّغْنِي أَمْلِي، وَأَصْلِحْنِي عَمَلِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ni Wewe tu nakutaraji na ni Wewe tu nakuomba, basi nitimizie matarajio yangu na nitengenezee amali yangu.

Kisha utakwenda Mina kwa utulivu na unyenyekevu huku ukijishughulisha na kumtaja Mwenyezi Mungu, utakapofika hapo utasema:

**الْحَمْدُ لِلَّهِ الَّذِي أَقْدَمَنِيهَا صَالِحًا فِي عَافِيَةٍ وَبَلَّغَنِي هَذَا
الْكَانَ الْلَّهُمَّ هَذِهِ مِنِّي وَهِيَ مِنَّا مَنَّتَ بِهِ مِنَ الْبَنَاسِكِ،
فَأَسْأَلُكَ أَنْ تَعْلَمَ فِيهَا بِمَا مَنَّتَ بِهِ عَلَى أَوْلِيَائِكَ، فَإِنَّا
أَنَا عَبْدُكَ وَفِي قَبْضَتِكِ**

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Ambaye amenileta nikiwa katika afya njema na ameniflikisha sehemu hii. Ewe Mwenyezi Mungu! Hii ni Mina, nayo ni miongoni mwa ibada za Hijja ulizonineemesha, hivyo nakuomba unineemeshe yale uliyowaneemesha Manabii Wako, kwani hakika mimi ni mja Wako na nimo mikononi Mwako.”

Ni mustahabu kwako kulala Mina usiku wa Arafa ukiutimiza katika kumtii Mwenyezi Mungu, na lililo bora ni iwe ibada yako na hususan Sala zako katika Msikiti wa Khayfu, na Sala yako humo uisalie kwenye mnara uliyopo

katikati ya msikiti. Na eneo lililopo baada ya dhiraat thelathini toka pembe zake zote (Msikiti wa Khayfu) huo ni msikiti wa Mtume (s.a.w.w.) na sehemu ya kusalia Manabii ambao walisali hapo kabla yake (a.s.). Ukishasali Sala ya Alfajri fuatiliza dua za baada ya Sala mpaka kuchomoza kwa juu, kisha nenda Arafa.

Adabu za kusimama Arafa:

Dua zilizopokewa toka kwa Ahlul-Baiti (a.s.) unapokuwa umesimama Arafa ni nyingi, nasi hapa tutataja baadhi ya dua hizi, hivyo utasema:

اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، فَلَا تَجْعَلْنِي مِنْ أَخْيَابِ وَفْدِكَ، وَارْحَمْ
مَسِيرِي إِلَيْكَ مِنَ الْفَجْرِ الْعَيْقِ. اللَّهُمَّ رَبَّ الْمَشَايِرِ كُلُّهَا،
فُكْ رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ، وَأُوسِعْ عَلَيَّ مِنْ رِزْقِكَ الْحَلَالِ، وَادْرُأْ
عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ. اللَّهُمَّ لَا تَنْكِبْ بِي، وَلَا تَخْدُعْنِي،
وَلَا تَسْتَدِرْ جِنِّي. اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِحَوْلِكَ وَجُودِكَ وَكَرَمِكَ
وَمَثِيلَكَ وَفَضْلِكَ، يَا أَسْمَاعَ السَّامِعِينَ، وَيَا أَبْصَرَ النَّاظِرِينَ، وَيَا
أَسْمَاعَ الْحَاسِبِينَ، وَيَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ، أَنْ تُصَلِّيَ عَلَى مُحَمَّدٍ
وَآلِ مُحَمَّدٍ وَأَنْ تَرْزُقَنِي خَيْرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako hivyo usinifanye mgeni niliyeshindwa kushinda wageni Wako wote, na urehemu mwendo wangu kuja Kwako toka njia ya mbali. Ewe Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa maeneo yote ya Hijja nikomboe na moto, nipanulie riziki yako ya halali na niondolee shari ya mafasiki wa kijini na kibinadamu. Ewe Mwenyezi Mungu! Usinifanyie hila na wala usinidanganye na wala usinivute polepole. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kwa uwezo Wako, ukarimu Wako, ihsani Yako, upaji Wako na fadhila Zako. Ewe Msikivu kushinda wasikivu wote! Ewe Mwenye kuona kushinda waonaji wote! Ewe Mwepesi wa kuhesabu kushinda wahasibu wote! Ewe Mwenye kurehemu kushinda marahimu wote, umswalie Muhammad na aali Muhammad na uniruzuku heri ya dunia na Akhera.”

Inua mikono yako mbinguni na omba haja yako toka kwa Mwenyezi Mungu, sema:

اللَّهُمَّ حاجِقِي إِلَيْكَ الَّتِي إِنْ أَعْطَيْتَنِي لَمْ يَضْرُّنِي مَا
مَنْعَتِنِي، وَالَّتِي إِنْ مَنْعَتِنِي لَمْ يَنْفَعْنِي مَا أَعْطَيْتِنِي، أَسْأَلُكَ
خَلَاصَ رَقَبَتِي مِنَ النَّارِ، اللَّهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، وَمِلْكُ يَدِكَ،
نَاصِيَتِي بِيَدِكَ، وَأَجْلِي بِعِلْمِكَ، أَسْأَلُكَ أَنْ تُوَقْقِنِي لِمَا يُرضِيكَ
عَنِّي، وَأَنْ تُسَلِّمَ مِنِّي مَنَاسِكِي الَّتِي أَرَيْتَهَا خَلِيلَكَ إِبْرَاهِيمَ
عَلَيْهِ السَّلَامُ، وَدَلَّتَ عَلَيْهَا نَبِيَّكَ مُحَمَّداً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ

وَآلِهِ. اللّٰهُمَّ اجْعَلْنِي مِنْ رَّضِيَتْ عَبْلَهُ، وَأَطْلُتْ عُبْرَةً
وَأَحْيِيْتَهُ بَعْدَ الْبَوْتِ حَيَاةً طَيِّبَةً

“Ewe Mwenyezi Mungu! Haja yangu Kwako ambayo lau utanipa hayatanidhuru yale uliyozuia na lau utaninyima hayataninufaisha yale uliyotoa, nakuomba uokovu wa shingo yangu dhidi ya moto. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako na miliki ya mikono Yako, nywele zangu za utosi zimo mikononi Mwako na kifo changu ni kwa elimu Yako, nakuomba uniwfikishie yale yatakayokufanya uwe radhi nami, na upokee toka kwangu ibada za Hijja ambazo ulimwonyesha khalili Wako Ibrahim sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, na ukamjulisha Nabii Wako Muhammad (s.a.w.w.). Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie mionganini mwa uliyeridhia amali zake, ukarefusha Umra yake na ukampa maisha mazuri baada ya kifo.”

Kisha sema:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللّٰهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْبُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ، يُحْبِي
وَيُبَيِّنُ وَيُبَيِّنُ وَيُحْبِي، وَهُوَ حَقٌّ لَا يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ، اللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ كَالَّذِي تَقُولُ وَخِيرًا مِّمَّا يَقُولُونَ
الْقَائِلُونَ، اللّٰهُمَّ لَكَ صَلَاتٍ وَنُسُكٍ وَمَحْيَايَ وَمَمَاتٍ وَلَكَ

تُراثي، وبِكَ حَوْلٍ وَمِنْكَ قُوتٌ، اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْفَقْرِ وَمِنَ
 وَسُوَاسِ الصَّدُورِ وَمِنْ شَتَاتِ الْأَمْرِ وَمِنْ عَذَابِ الْقَبْرِ، اللَّهُمَّ
 إِنِّي أَسْأَلُكَ خَيْرَ الرِّيَاحِ، وَأَعُوذُ بِكَ مِنْ شَرِّ مَا تَأْتِيَ بِهِ الرِّيَاحُ،
 فَأَسْأَلُكَ خَيْرَ اللَّيلِ وَخَيْرَ النَّهَارِ اللَّهُمَّ اجْعَلْ فِي قَلْبِي نُورًا وَفِي
 سَعْيِ نُورًا وَفِي بَصَرِي نُورًا وَفِي لَحْيِي وَدَمِي وَعَظَامِي وَعَرْدَقِي
 وَمَقْعَدِي وَمَقَامِي وَمَدْخَلِي وَمَخْرَجِي نُورًا وَأَعْظَمْ لِي نُورًا يَا رَبَّ
 يَوْمِ الْقِيَامَةِ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

‘Hakuna mungu ila Allah Mmoja wa pekee asiyé na mshirika, ana ufalme na ana sifa njema, anahuisha na kufisha, na anafisha na kuhuisha, Naye ni Mzima wa milele, heri zimo mikononi Mwake na Yeye juu ya kila kitu ni Muweza. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema kama unayoisema na ni bora kushinda tunayoisema na ni ya juu kupita wanayoisema wenyé kusema. Ewe Mwenyezi Mungu! Ni kwa ajili Yako Sala yangu, ibada zangu, uzima wangu na kufa kwangu. Na ni kwa ajili Yako urithi wangu, ni kupitia Kwako ujanja wangu na ni kutoka Kwako nguvu zangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najilinda Kwako na ufakiri, wasiwasi wa vifua, mtawanyiko wa jambo na adhabu ya kaburi. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba heri ya pepo na ninajilinda Kwako na shari inayoletwa na pepo, hivyo nakuomba heri ya usiku na heri ya mchana. Ewe Mwenyezi Mungu! Weka nuru

moyoni mwangu, nuru masikioni mwangu, nuru machoni mwangu, na nuru ndani ya nyama yangu, damu yangu, mifupa yangu, mishipa yangu, makalio yangu, masimamio yangu, maingilio yangu na matokeo yangu. Na niongezee nuru ewe Mola Mlezi siku ambayo nitakutana Nawe hakika Wewe juu ya kila kitu ni Muweza.”

Kithirisha kutoa sadaka katika siku hii, na elekea Kibla na useme mara mia moja:

سُبْحَانَ اللَّهِ أَكْبَرُ مَا شَاءَ اللَّهُ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْحُكْمُ وَلَهُ الْحَمْدُ، يُحِبِّي وَيُبَيِّنُ، وَيُبَيِّنُ وَيُحِبِّي، وَهُوَ حَقٌّ لَا يُؤْتُ، بِيَدِهِ الْخَيْرُ، وَهُوَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Ametakasika Mwenyezi Mungu! Mwenyezi Mungu Mkubwa mno! Aliyoyataka Mwenyezi Mungu! Na hakuna nguvu ila kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu! Nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah Mmoja wa pekee hana mshirika, ana ufalme na ana sifa njema, anahuisha na kufisha, Naye ni Mzima wa milele, heri imo mikononi Mwake na Yeye ni Muweza wa kila kitu. “

Kisha soma Aya kumi za mwanzo wa Sura al-Baqara, kisha soma Sura Ikhlasi mara tatu, soma Aya Kursiyu, kisha soma Aya ya utiishaji, nayo ni:

إِنَّ رَبَّكُمُ اللَّهُ الَّذِي خَلَقَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ فِي سِتَّةٍ أَيَّامٍ ثُمَّ
 اسْتَوَى عَلَى الْعَرْشِ يُغْشِي اللَّيْلَ النَّهَارَ يُطْلِبُهُ حَشِيشًا
 وَالشَّمْسَ وَالقَمَرَ وَالنُّجُومَ مُسَخَّرًا بِأَمْرِهِ أَلَا لَهُ الْخَلْقُ
 وَالْأَمْرُ تَبَارَكَ اللَّهُ رَبُّ الْعَالَمِينَ

“Hakika Mola wenu Mlezi ni Mwenyezi Mungu aliyeziumba mbingu na ardi katika hatua sita, kisha ukakamilika katika Arshi. Huufunika usiku kwa mchana uufluatiao upesi, na jua na mwezi na nyota vimetiishwa kwa amri Yake. Fahamuni kuumba na amri zote ni Zake. Ametukuka Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu wote.” (Sura A’raf: 54).

Kisha soma Sura al-Falaqi na Sura an-Nasi, kisha mhimidi Mwenyezi Mungu kwa kila neema aliyokuneemesha na taja neema Zake moja baada ya nyingine kadiri uwezavyo. Na mhimidi kwa zile neema alizokuneemesha mionganoni mwa familia au mali, na mhimidi kwa majaribu aliyokupa na sema:

أَللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ عَلَى نَعْمَائِكَ الَّتِي لَا تُحْصِي بِعَدَدٍ، وَلَا
 تُكَافِئُ بِعَبْلٍ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kila sifa njema ni Yako kwa neema Zako ambazo hazihesabiki kwa idadi wala hazilipwi kwa matendo.”

Na mhimidi kwa kila Aya ambayo humo amejihimidi Mwenyewe ndani ya Qur'ani, na msabihi kwa kila tasbihi aliyojisabihi Mwenyewe katika Qur'ani, na mtukuze kwa kila utukuzo ambao amejitukuza Mwenyewe katika Qur'ani, na mhalilie kwa kila tahalili ambayo kajihalilia Mwenyewe katika Qur'ani, na mswalie Muhammad na aali Muhammad na kithirisha kufanya hivyo na jitahidi kufanya hayo. Na muombe Mwenyezi Mungu kwa kila jina alilojiita Mwenyewe ndani ya Qur'ani na kwa kila jina unaloona zuri, na muombe kwa majina Yake yaliyopo mwishoni mwa Sura al-Hashri.

Na soma dua hii:

أَسْأَلُكَ يَا أَللَّهُ يَا رَحْمَانُ بِكُلِّ اسْمٍ هُوَ لَكَ، وَأَسْأَلُكَ بِقُوَّتِكَ
 وَقُدْرَتِكَ وَعِزْتِكَ وَبِجِيْعِ مَا أَحَاطَ بِهِ عَلِيْكَ وَبِأَرْكَانِكَ كُلِّهَا،
 وَبِحَقِّ رَسُولِكَ صَلَواتُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَبِإِسْمِكَ الْأَكْبَرِ الْأَكْبَرِ،
 وَبِإِسْمِكَ الْعَظِيمِ الَّذِي مَنْ دَعَاكَ بِهِ كَانَ حَقًّا عَلَيْكَ أَنْ لَا
 تُخَيِّبَهُ، وَبِإِسْمِكَ الْأَعْظَمِ الْأَعْظَمِ الْأَعْظَمِ الَّذِي مَنْ دَعَاكَ بِهِ
 كَانَ حَقًّا عَلَيْكَ أَنْ لَا تَرْدَدْهُ، وَأَنْ تُعْطِيهِ مَا سَأَلَ، أَنْ تَغْفِرَ لِ
 ذُنُوبِ فِي جَيْعِ عَلِيْكَ فِي

“Nakuomba ewe Mwenyezi Mungu ewe Mwingi wa rehema kwa kila jina ambalo ni Lako. Na ninakuomba kwa

nguvu Zako, uwezo Wako, utukufu Wako na kwa yote yaliyodhibitiwa na elimu Yako, na mkusanyo Wako na nguzo Zako zote, na kwa haki ya Mtume Wako sala Zako ziwe juu yake na juu ya aali zake, na kwa jina Lako kubwa lililo tukufu mno, na kwa jina Lako adhimu ambalo atakayekuomba kwalo huwa ni haki juu Yako kumjibu, na kwa jina Lako adhimu mno, adhimu kushinda kila lililo adhimu, ambalo atakayekuomba kwalo huwa ni haki juu Yako kutokumnyima na kumpa yale aliyokuomba, unighufirie dhambi zangu zote katika yote unayoyajua kwangu.”

Muombe Mwenyezi Mungu haja Zako zote na omba akuafikishe kuhiji mwaka ujao, na jiombee lile upendalo, na jitahidi sana kwani hii ni siku ya dua na maombi, na jilinde kwa Mwenyezi Mungu na shetani kwani shetani hatokusahau katika sehemu aipendayo sana Mwenyezi Mungu kukusahaulisha katika sehemu hiyo, na jiepushe kuwatizama watu.

Sema mara sabini:

أسألكَ الْجَنَّةَ

“Nakuomba Pepo.”

Na mara sabini:

أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ رَبِّيْ وَأَتُوْبُ إِلَيْهِ

“Namuomba maghfira Mwenyezi Mungu na ninatubu Kwake.”

Na soma dua ambayo Jibril (a.s.) alimfunza Adam (a.s.) ili akubaliwe toba yake:

سَبَّحَنْكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ عَبْلَتْ سُوءًا وَظَلَمْتَ

نَفْسِي وَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِي فَاغْفِرْ لِي إِنَّكَ أَنْتَ خَيْرُ الْغَافِرِينَ.

سَبَّحَنْكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ عَبْلَتْ سُوءًا وَظَلَمْتَ

نَفْسِي فَاعْتَرَفْتُ بِذَنْبِي فَاغْفِرْ لِي إِنَّكَ أَنْتَ التَّوَابُ الرَّحِيمُ.

“Umetakasika Ewe Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni Yako, hakuna mungu ila Wewe. Nimetenda mabaya, nimeidhulumu nafsi yangu na nimekiri dhambi zangu hivyo nighufirie hakika Wewe ni Mwenye kughufuri kushinda wote wenyе kughufuri.Umetakasika Ewe Mwenyezi Mungu na kila sifa njema ni Yako, hakuna mungu ila Wewe. Nimetenda mabaya, nimeidhulumu nafsi yangu na nimekiri dhambi zangu hivyo nighufirie hakika Wewe ni Mwenye kupokea toba Mwenye kurehemu.”

Na wakati wa kuzama juu soma dua hii:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَعُوذُ بِكَ مِنَ الْفَقْرِ، وَمِنْ تَشْتِتِ الْأُمُرِ، وَمِنْ شَرِّ ما
يَحْدُثُ بِاللَّيْلِ وَالنَّهَارِ، أَمْسَى ظُلْمِي مُسْتَجِيرًا بِعَفْوِكَ،
وَأَمْسَى خَوْفِي مُسْتَجِيرًا بِأَمَانِكَ، وَأَمْسَى ذُلْمِي مُسْتَجِيرًا

بِعِزَّكَ، وَأَمْسِي وَجْهِي الْفَانِي مُسْتَجِيرًا بِوَجْهِكَ الْبَاقِي، يَا خَيْرَ
 مَنْ سُيِّلَ، وَيَا أَجْوَدَ مَنْ أَعْطَى، يَا أَرْحَمَ مَنِ اسْتَرْحَمَ، جَلَّ
 بِرَحْمَتِكَ، وَأَلْبِسْنِي عَافِيَّتَكَ، وَاصْرِفْ عَنِّي شَرَّ جَيِيعِ خَلْقِكَ
 وَارْزُقْنِي خَيْرَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi najilinda Kwako na ufakiri, mtawanyiko wa mambo na shari ya yale yatokeayo usiku na mchana. Dhulma yangu imeshinda na hali ni yenye kuomba hifadhi kwenye msamaha Wako, hofu yangu imeshinda na hali ni yenye kuomba hifadhi kwenye amani Yako, udhalili wangu umeshinda na hali ni wenye kuomba hifadhi kwenye utukufu Wako, uso wangu wenye kutoweka umeshinda na hali ni wenye kuomba hifadhi kwenye utukufu Wako. Ewe mbora aliyeombwa! Ewe mkarimu aliyetao! Na ewe Mwenye kurehemu aliyeombwa rehema! Nifunike kwa rehema Zako, nivishe afya Yako na niondolee shari ya viumbe Wako wote. Na niruzuku heri ya dunia na Akhera.”

Jiombee mwenyewe, wazazi wako na ndugu zako waumini, na kwa uchache wawe waumini arubaini. Imepokewa kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: Jua likizama Siku ya Arafa sema:

اللّٰهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ هَذَا الْبَوْقِفِ، وَارْزُقْنِيهِ أَبْدًا

مَا أَبْقَيْتَنِي، وَاقْلِبْنِي الْيَوْمَ مُفْلِحًا مُسْتَجَابًا
 لِي، مَرْحُومًا مَغْفُورًا لِي، بِأَفْضَلِ مَا يَنْقِلِبُ بِهِ الْيَوْمَ أَحَدُ مِنْ
 وَفْدِكَ، وَحُجَّاجٍ بَيْتِكَ الْحَرَامِ، وَاجْعَلْنِي الْيَوْمَ مِنْ أَكْرَمِ
 وَفْدِكَ عَلَيْكَ، وَأَعْطِنِي أَفْضَلَ مَا أَعْطَيْتَ أَحَدًا مِنْهُمْ مِنَ الْخَيْرِ
 وَالْبَرَكَةِ وَالْعَافِيَةِ وَالرَّحْمَةِ وَالرِّضوانِ وَالْغُفْرَةِ، وَبَارِكْ لِي فِيهَا
 أَرْجِعُ إِلَيْهِ مِنْ أَهْلِ أَوْ مَالِ أَوْ قَلِيلِ أَوْ كَثِيرٍ، وَبَارِكْ لَهُمْ فِي

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usifanye kisimamo changu hiki kuwa ahadi yangu ya mwisho na niruzuku (Hijja) zizazo muda wote utakaoniacha hai, na nirudishe leo na hali nikiwa ni mwenye kufaulu, kufanikiwa, mwenye kujibiwa, mwenye kurehemewa na mwenye kughufuriwa, katika hali bora kushinda ile atakayorudi nayo ye yote toka katika ugeni Wako na mahujaji wa Nyumba Yako tukufu, na nijaalie leo kuwa mkirimiwa kushinda wageni Wako wote waliofika Kwako, na nipe kilicho bora kushinda ulichompa ye yote kati yao mionganini mwa heri, baraka, rehema, radhi na maghfira. Na niwekee baraka katika yale nitakayoyarejelea mionganini mwa familia au mali, au kichache au kingi, na wawekee baraka kwangu.”

Kariri kauli yako:

اللَّهُمَّ فُكْ رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nikomboe na moto.”

Adabu za kusimama al-Mash’ari:

Atoke Arafa kwa utulivu na unyenyekevu baada ya kuzama kwa jua huku akiwa ni mwenye kujishughulisha na dua na kuomba maghfira. Akifika al-Kathibul-Ahmar kuliani mwa njia ni mustahabu kusoma dua hii:

اللّٰهُمَّ ارْحَمْ مَوْقِنِي، وَزِدْ عَمَلِي، وَسَلِّمْ لِي دِينِي وَتَقْبِيلْ مَنَا سِكِّي
اللّٰهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ هَذَا الْمَوْقِفِ، وَأُرْثُرْ قُنْيِهِ مِنْ
قَابِلِ أَبَدًا مَا أُبَقَّيْتُنِي،

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kirehemu kisimamo changu, nizidishie katika amali yangu, nisalimishie dini yangu na zipokee ibada zangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Usifanye kisimamo changu hiki kuwa ahadi yangu ya mwisho na niruzuku tena muda wote utakaoniacha hai.”

Wakati wa kutembea kithirisha kusema:

اللّٰهُمَّ فُلِّ رَبْقَتِي مِنَ النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! ikomboe shingo yangu na moto.”

Kisha soma dua hii:

اللّٰهُمَّ هِنْدِهِ جَمِيعٌ. اللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ أَنْ تَجْعَلَ لِي فِيهَا جَوَامِعَ

الْخَيْرُ. اللَّهُمَّ لَا تُؤْسِنِنِي مِنَ الْخَيْرِ الَّذِي سَأَلْتُكَ أَنْ تَجْعَهُ لِ
 فِي قَلْبِي، وَأَطْلُبُ إِلَيْكَ أَنْ تُعْرِفَنِي مَا عَرَفْتَ أُولِيَاءَكَ فِي مَنْزِلِ
 هَذَا، وَأَنْ تَقِينِي جَوَامِعَ الشَّرِّ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Huu ni mkusanyiko ewe Mwenyezi Mungu nakuomba unikusanyie humu ya kusanyayo heri. Ewe Mwenyezi Mungu! Usinikatishe tamaa na heri ambayo nimkuomba unikusanyie moyoni. Kisha naomba toka Kwako unijulishe katika mafikio yangu haya yale uliyowajulisha mawalii Wako, na unikinge na yakusanyayo shari.”

Ni mustahabu kuchelewesha Salaya Maghrib na Isha mpaka atakapofika Muzdalifa na azisali hapo kwa adhana moja na iqama mbili. Na aokote mawe ya kupigia shetani toka hapo Muzdalifa na idadi yake ni sabini, ukiweza basi ni bora uhuishe usiku wako kwa ibada, dua zilizopokewa toka kwa Ahlul-Baiti (a.s.) na nyinginezo, na mionganii mwa yaliyopokewa toka kwa Ahlul-Baiti (a.s.) ni kusoma dua hii:

آللَّهُمَّ رَبَّ الْشَّعْرَالْحَرَامِ، فُكْ رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ، وَأَوْسِعْ عَلَيَّ
 مِنْ رُنْقَكَ الْحَلَالِ، وَادْرَأْ عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ،
 آللَّهُمَّ أَنْتَ خَيْرُ مَطْلوبِ إِلَيْهِ، وَخَيْرُ مَدْعُوٍّ وَخَيْرُ مَسْؤُولٍ، وَلِكُلِّ

وَافِدٌ جَائِزٌ، فَاجْعَلُ جَائِزٍ فِي مَوْطِنِي هَذَا أَنْ تُقِيلَنِي عَثْرَتِي،
 وَتَقْبَلَ مَعْذِرَتِي، وَأَنْ تَجَاوِزَ عَنْ خَطِيئَتِي، ثُمَّ اجْعَلِ التَّقْوَى
 مِنَ الدُّنْيَا زَادِي وَتَقْلِبِنِي مُفْلِحًا مُنْجِحًا مُسْتَجَابًا بِأَفْضَلِ
 مَا يَرِجُعُ بِهِ أَحَدٌ مِنْ وَفْدِكَ وَزُوْرِ بَيْتِكَ الْحَرام

“Ewe Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa Mash’ari tukufu! Ikomboe shingo yangu na moto, nipanulie riziki Yako ya halali iliyo nzuri na niondolee shari za mafasiki wa kijini na kibinadamu. Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe ni mbora kushinda kila ambaye hutafutwa (mahitaji) Kwake, ni mbora kushinda kila mwenye kuitwa na ni mbora kushinda kila mwenye kuombwa, na kila mgeni ana zawadi hivyo jaalia zawadi yangu sehemu yangu hii kwa kufumbia macho kujikwaa kwangu, kukubali udhuru wangu na kusamehe makosa yangu. Kisha jaalia kujeipusha na dunia kuwa masurufu yangu, na nirudishe na hali ni mwenye kufaulu, mwenye kufanikiwa na mwenye kujibiwa, katika hali bora kushinda ile atakayorejea nayo yejote toka katika ugeni Wako na mahujaji wa Nyumba Yako tukufu.”

Jua likichomoza ungama dhambi zako kwa Mwenyezi Mungu mara saba, omba toba mara saba na mtaje Mwenyezi Mungu wakati wa kutoka, yaani wakati unapotoka al-Mash’ar kuelekea Mina, na kutembea kwa kasi katika bonde, na kiwango cha kutembea ni hatua mia moja, na soma dua hii:

أَللّٰهُمَّ سَلِّمْ لِي عَهْدِي، وَاقْبِلْ تَوْتِي، وَأَجِبْ دَعْوَتِي، وَاحْلُفْنِي
 فِيمَنْ تَرَكْتُ بَعْدِي رَبٌّ اغْفِرْ وَارْحَمْ وَتَجَاوِزْ عَنِّيَا تَعْلَمْ إِنَّكَ أَنْتَ
 الْأَعْزَلُ الْأَكْرَمُ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Pokea ahadi yangu, kubali toba yangu, nijibu dua yangu na kuwa mrithi wangu kwa wale niliowaacha baada yangu.Mola Mlezi! Ghufuria, rehemu na samehe unayoyajua, hakika Wewe ni Mtukufu sana Mkarimu mno.”

Faida:

Mina, Arafa na al-Mash’arul-Haram ndio maeneo matakatifu kushinda maeneo mengine matakatifu. Kuhusu ubora wake zimepokewa hadithi nyingi, katika hadithi moja imesemwa: “Atakayesimama sehemu hizi mbili (Arafa na Muzdalifa) na akatembea baina ya milima hii miwili (Swafa na Mar’wa), kisha akatufu Nyumba hii na akasali nyuma ya Maqamu Ibrahim (a.s.) na akadhani kwamba Mwenyezi Mungu hajamghufiria basi ye ye ni miongoni mwa watu wenye mzigo mkubwa.”

Na katika Hadithi nyingine: “Watu watakapochukua mafikio yao huko Mina mnadi hunadi toka upande wa Mwenyezi Mungu: Ikiwa mnataka niridhie basi nimesharidhia.”

Na katika Hadithi nyingine: “Watu watakapochukua mafikio yao huko Mina mnadi hunadi: Lau mngekuwa mnaujua ni uwanja wa nani mliyofikia mngekuwa na

yakini na maghfira.”

Kutokana na Hadithi inadhihiri kwamba maeneo haya yaliyobarikiwa ni kati ya maeneo makubwa mno ya kudhihirikia rehema za Mola Mlezi, hivyo inapasa kwa wale wenye kupata heshima ya kufika maeneo hayo matukufu kutumia fursa hiyo ipasavyo, kwani hakika muda, sehemu na hali ni mionganoni mwa nyenzo za karibu za kujikurubisha na kujibiwa. Ni wazi kwamba Mina na Mash’arul-Haram zimo katika wigo wa eneo takatifu (Haram), na Arafa ipo nje ya wigo wa eneo takatifu (Haram), na mpaka wa Arafa ni mashuhuri huko.

Adabu za kutupa mawe:

Nazo ni mambo yafuatayo:

1. Mtupaji mawe atembee kwa miguu asiwe juu ya kipando.
2. Atembee kwa utulivu na unyenyekevu aendapo kutupa.
3. Mtupaji awe katika tohara wakati wa kutupa.
4. Akipe mgongo Kibla na aelekee upande wa nguzo ya kwanza, hiyo ni kinyume na nguzo mbili zilizobaki zenyewe atazipiga mawe hali ameelekea Kibla tukufu.
5. Kati yake na nguzo kuwe na hatua kumi au kumi na tano.
6. Mawe yawe mkono wake wa kushoto na atupe kutumia mkono wa kulia.

7. Wakati wa kutupa aseme:

اَللّٰهُمَّ هذِهِ حَصِيلَاتٍ، فَاحْصِهِنَّ لِي، وَارْفَعْهُنَّ فِي عَمَلِي

Ewe Mwenyezi Mungu hakika haya ni mawe yangu yahesabu kwa ajili yangu na yaongeze katika amali yangu.”

8. Kama akiweza basi ayatupe kwa mtindo wa kutumia kidole gumba.

9. Wakati wa kutupa kila jiwe aseme:

اَللّٰهُ اَكْبَرُ۔ اَللّٰهُمَّ ادْحُرْ عَنِّي الشَّيْطَانَ۔ اَللّٰهُمَّ تَسْدِيقًا بِكِتَابِكَ
وَعَلَى سُنْنَةِ نَبِيِّكَ۔ اَللّٰهُمَّ اجْعَلْهُ لِي حَجًّا مَبُورًا، وَعَمَلًا مَقْبُولًا،
وَسَعْيًا مَشْكُورًا، وَذَنْبًا مَغْفُورًا

“Mwenyezi Mungu mkubwa! Ewe Mwenyezi Mungu! Niepushie shetani na askari wake. Ewe Mwenyezi Mungu ni kwa ajili ya kusadikisha Kitabu Chako na kwa kufuata Sunnah ya Nabii Wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Ijaalie iwe Hijja njema kwangu, amali yenye kupokewa, mwendo wenyenye kuthaminiwa na dhambi yenye kughufiriwa.”

Na inajuzu mtupaji kutosheka na takbira tu.

10. Mtupaji akikamilisha na akarudi kwenye mafikio yake huko Mina aseme:

اَللّٰهُمَّ بِكَ وَثَقْتُ، وَعَلَيْكَ تَوَكَّلْتُ، فَنِعْمَ الرَّبُّ، وَنِعْمَ الْمُؤْمِنُ

وَنِعْمَ النَّصِيرُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nimekuamini na nimekutawakali, ni Mola Mlezi mzuri ulioje! Ni kiongozi mzuri ulioje! Na ni Msaidizi mzuri ulioje! ”

Adabu za sadaka ya kuchinja:

Nazo ni mambo yafuatayo:

1. Awe ana ngamia na akishindwa basi ng'ombe, na akishindwa awe kondoo mweusi kisha mwenye mapembe mwenye haiba kubwa.
2. Amhudhurishe Mina siku ya Arafa, kwa maana ya kwamba amnunue siku ya Arafa kisha aje naye Mina kwa ajili ya kumchinja.
3. Amchinje ngamia na hali ngamia huyo akiwa amesimama huku kafungwa mikono yake baina ya kwato na magoti. Na amchinjie tokea upande wa kulia na hali yeye mwenyewe akiwa wima.
4. Sadaka iwe nono.
5. Uchinjaji ufanywe na alhaji mwenyewe, na kama hawezi kuchinja basi yeye ashike kisu na mchinjaji aushike mkono wake. Na si vibaya alhaji kuweka mkono wake juu ya mkono wa mchinjaji wakati wa kuchinja.

6. Wakati wa kuchinja aseme:

وَجَهْتُ وَجْهِي لِلَّذِي فَطَرَ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضَ حَنِيفًا مُسْلِمًا
وَمَا أَنَا مِنَ الْمُشْرِكِينَ، إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحْيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ
رَبِّ الْعَالَمِينَ، لَا شَرِيكَ لَهُ، وَبِذِلِّكَ أُمِرْتُ وَأَنَا مِنَ
الْمُسْلِمِينَ، أَللَّهُمَّ مِنْكَ وَلَكَ بِسْمِ اللَّهِ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، أَللَّهُمَّ تَقْبِلْ
مِنِّي كَمَا تَقْبِلَتْ مِنْ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِكَ وَمُوسَى كَلِيلِكَ وَمُحَمَّدٌ
حَبِيبِكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ وَعَلِيهِمْ.

“Mimi nimeuelekeza uso wangu kwa yule aliyeziumba mbingu na ardhi, hali yakuwa nimeacha dini za upotovu niliye mwislamu, na mimi si mionganii mwa mushrikina. Hakika Sala yangu, ibada zangu, uzima wangu na kufa kwangu ni kwa ajili ya Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa ulimwengu wote, hana mshirika, na hayo ndiyo niliyoamrishwa, na mimi ni wa kwanza wa waliojisalimisha. Ewe Mwenyezi Mungu! Ni kutoka Kwako na ni kwa ajili Yako: kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa haki ya Mwenyezi Mungu na Mwenyezi Mungu ni mkubwa. Ewe Mwenyezi Mungu! Pokea toka kwangu kama ulivyopokea toka kwa Ibrahim khalili Wako, Musa msemeza Wako na Muhammad hababi Wako sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na juu ya aali zake na juu yao.”

Adabu za kunyoa na kupunguza:

Nazo ni mambo yafuatayo:

1. Kuelekea Kibla.
2. Kusoma Bismillahi.
3. Wakati wa kunyoa asome:

اللّٰهُمَّ أَعْطِنِي بِكُلِّ شَعْرَةٍ نُورًا يَوْمَ الْقِيَامَةِ، وَحَسَنَاتِ
مُضاعَفَاتٍ، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ

مُحَمَّدٍ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nipe kwa kila unywele nuru siku ya Kiyama na mema maradufu, hakika Wewe juu ya kila kitu ni Muweza. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad.”

4. Azizike nywele zake huko Mina.
5. Baada ya kunyoa akate ndevu zake na masharubu yake na akate kucha zake.

Adabu za kurudi Makka kwenda kutekeleza matendo matano:

Nayo ni Kutufu tawafu ya Hijja, Sala yake, kutembea baina ya Swafa na Mar’wa, kutufu tawafu Nisaa na kusali rakaan zake mbili. Adabu hizo ni mambo yafuatayo:

1. Kuoga huko Mina kwa ajili ya kuingia Makka.
2. Kukata kucha na masharubu.
3. Kumtaja Mwenyezi Mungu na kumsalia Mtume wakati wa kuelekea Msikiti Mtukufu.
4. Kusimama kwenye mlango wa Msikiti Mtukufu na kusoma dua hii:

أَللّٰهُمَّ أَعُنِّي عَلٰى نُسُكِكَ، وَسَلِّنِي لَهُ وَسَلِّنِيهِ لِي، أَسْأَلُكَ مَسْأَلَةً
 الْعَلِيلِ الْذَّلِيلِ الْمُعْتَرِفُ بِذَنْبِهِ، أَنْ تَغْفِرَ لِي ذُنُوبِي، وَأَنْ
 تَرْجِعِنِي بِحاجَتِي. أَللّٰهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ، وَالْبَلْدُ بَلْدُكَ، وَالْبَيْتُ
 بَيْتُكَ، جِئْتُ أَطْلُبُ رَحْمَتَكَ، وَأَعُمْ طَاعَتَكَ، مُتَّبِعاً لِأَمْرِكَ،
 راضِياً بِقَدَرِكَ، أَسْأَلُكَ مَسْأَلَةَ الْمُضْطَرِّ إِلَيْكَ، الْمُطِيعُ
 لِأَمْرِكَ، الْمُشْفِقُ مِنْ عَذَابِكَ، الْخَائِفُ لِعَقُوبَتِكَ، أَنْ تُبَلِّغَنِي
 عَفْوَكَ، وَتُجِيرَنِي مِنَ النَّارِ بِرَحْمَتِكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nisaidie katika ibada zangu, nisalimishe kwazo na zisalimishe kwa ajili yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba maombi ya mgonjwa aliye dhalili mwenye kukiri dhambi zake unighufirie dhambi zangu na unirejeshe nikiwa na haja yangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako

na mji huu ni mji Wako, na Nyumba hii ni nyumba Yako nimekuja na hali natafuta rehema Zako, natanguliza utiifu Kwako, ni mwenye kufuata amri Yako na ni mwenye kuridhia makadara Yako. Nakuomba maombi ya fakiri aliyekimbilia Kwako, mwenye kukutii amri Yako na mwenye kuogopa adhabu Yako na mwenye hofu na adhabu Yako, unifikishie msamaha Wako na uniepusha na moto kwa rehema Zako.”

5. Adabu zote tulizozitaja katika tawafu ya Umrah, sala yake na matembezi yake zote zinaingia pia katika tawafu ya ziara, katika matembezi baina ya Safwa na Mar’wa na katika Tawafu Nisaa.
6. Ni mustahabu baada ya kumaliza matendo ya Mina kurejea Makka Siku ya Idi kwa ajili ya matendo yaliyotajwa.

Adabu za mawe matatu baada ya kurejea Mina:

Nazo ni mambo yafuatayo:

1. Kusimama kwenye kila nguzo hali ukiomba dua zilizopokewa toka kwa Ahlul-Baiti (a.s.), atasema yale aliyosema siku ya kutupa mawe.
2. Atupe kwa mkono wa kushoto hali ameelekea Kibla ila jiwe la kwanza lenyewe atalitupa hali kaipa mgongo Kibla kama ulivyokwishajua, na atalitupa kwa mkono wake wa kulia na wala asisimame hapo.
3. Adabu zote zinazozingatiwa katika kutupa mawe siku ya kutupa mawe zinazingatiwa hapa kama ilivyotangulia.

Mambo yaliyo mustahabu huko Mina na Msikiti wa Khayfa:

Nayo ni yafuatayo:

1. Kubakia Mina siku za Tashriq, yaani siku tatu za baada ya Siku ya Idi, baada ya kuisha muda wa kutupa mawe. Kitendo hicho (cha kubaki Mina) ni bora kuliko kwenda Makka kutufu tawafu ya Sunnah na mfano wake.
2. Kutoa takbira huko Mina baada ya Sala kumi na tano, ya kwanza ni Sala ya Adhuhuri ya siku ya kuchinja mpaka Sala ya Asubuhi ya siku ya nne, bali ni hata baada ya Sala za Sunnah pia. Na katika miji isiyokuwa Mina ni baada ya Sala kumi, kuanzia Sala ya Adhuhuri ya siku ya kuchinja mpaka Sala ya Asubuhi ya siku ya tatu. Na sura ya takbira hiyo ni aseme:

أَلْهُمْ أَكْبِرُ أَلْهُمْ أَكْبِرُ، لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ، أَلْهُمْ أَكْبِرُ وَلِلَّهِ الْحَمْدُ،
أَلْهُمْ أَكْبِرُ عَلَى مَا هَدَانَا، أَلْهُمْ أَكْبِرُ عَلَى مَا رَزَقَنَا مِنْ بَهِيمَةِ
الْأَنْعَامِ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ عَلَى مَا أَبْلَانَا

“Mwenyezi Mungu mkubwa! Mwenyezi Mungu mkubwa! Hakuna mungu ila Allah na Mwenyezi Mungu mkubwa! Mwenyezi Mungu mkubwa! Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu. Mwenyezi Mungu mkubwa! Kwa aliyoutuongoza. Mwenyezi Mungu mkubwa! Kwa aliyoturuzuku mionganoni mwa wanyama howa. Na kila sifa

njema ni ya Mwenyezi Mungu kwa yale aliyotujaribu.”

3. Asali Sala zake zote (faradhi na Sunnah) katika Msikiti wa Khayfa, na sehemu bora humo ni alipokuwa akisalia Mtume wa Mwenyezi Mungu, napo ni kuanzia kwenye mnara mpaka kiasi cha takribaa dhiraal thelathini tokea upande wa Kibla, kuliani mwa Kibla, kushotonii mwake na nyuma yake. Imepokewa katika Hadithi tukufu kwamba kusali rakaa mia katika Msikiti wa Khayfa kabla ya kutoka Mina kunalingana na ibada ya miaka sabini.
4. Kufanya tasbihi mara mia moja. Imepokewa kwamba atakayesema humo: “Ametakasika Mwenyezi Mungu” ataandikiwa thawabu za mtu aliyemwacha huru mtumwa.
5. Kuhalili mara mia moja. Imepokewa kwamba atakayesema humo mara mia moja: “Hakuna mungu ila Allah.” Ataandikiwa thawabu za mtu aliyeihuisha nafsi.
6. Kumhimidi Mwenyezi Mungu mara mia moja. Imepokewa kwamba atakayesema humo mara mia moja: “Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu.” Ni sawa na aliyetoa mapato ya Kufa na Basra katika njia ya Mwenyezi Mungu.
7. Kusali rakaa sita katika asili ya kilele cha mlima, na bora ni asali Sala hii wakati anapotaka kurejea Makka hali ni mwenye kuiaga Mina. Na hiyo ni wakati jua litakapofifia (yaani mwishoni mwa mchana) katika siku ya mwezi kumi na tatu.

Mambo yaliyo mustahabu wakati wa kurudi

Makka:

Nayo ni yafuatayo:

1. Kusali rakaa sita katika Msikiti wa Khayfa kama ilivyotangulia.
2. Kuoga kwa ajili ya kuingia Makka na kwa ajili ya kuingia Msikiti mtukufu.
3. Kuingilia mlango wa Bani Shayba kama alivyotaja Ash-Shahid.

Amali na mambo yaliyo mustahabu kufanywa huko Makka:

Nayo ni yafuatayo:

1. Asalie Sala zake ndani ya Msikiti Mtukufu kwani katika ulimwengu hakuna eneo tukufu kushinda hilo, na kusali sala moja humo ni sawa na maelfu ya sala. Yatosha katika fadhila zake kwamba Mwenyezi Mungu hakumleta Nabii yejote wala Wasii yejote ila alipata heshima ya kusalia humo na kuizunguka Nyumba ambayo imo ndani ya msikiti huu.
2. Asome Qur'ani nzima huko Makka. Imepokewa kwamba atakayesoma Qur'ani yote huko Makka hatakuwa mpaka awe amemwona Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na sehemu yake Peponi.
3. Akithirishe kumtaja Mwenyezi Mungu.
4. Akithirishe kuitazama Ka'ba. Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Kuitizama Ka'ba kwa kuipenda

kunasambaratisha kabisa makosa.” Na imepokewa toka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba alisema: “Mahujaji mtakapotoka kwenda kwenye Nyumba ya Mwenyezi Mungu basi kithirisheni kuitazama Nyumba ya Mwenyezi Mungu, kwani hakika Mwenyezi Mungu ana rehema mia moja na ishirini katika Nyumba Yake Tukufu, sitini ni kwa ajili ya wenyе kuitufu, arubaini kwa ajili ya wenyе kusali humo, na ishirini kwa ajili ya wenyе kuitazama.”

5. Baada ya kumaliza Tawafu ya Hijja ni mustahabu kufanya Tawafu ya Wiki (yaani mizunguko saba) na kusali rakaa mbili kwa niaba ya baba, mama, mke au mme, watoto, mndani, na watu wote wa mji wake, kila mmoja Tawafu yenyе mizunguko saba pamoja na rakaa zake mbili, na inatosha pia kwa ajili ya wote Tawafu moja na rakaa zake mbili, lakini akimtengеa kila mmoja Tawafu yake na Sala yenyе kujitegemea ni bora zaidi.
6. Ni mustahabu kwa alhaji muda atakaobakia Makka kutufu Tawafu mia tatu na sitini sawa na idadi ya siku za mwaka, kila Tawafu moja ni mizunguko saba, la sivyo azunguke mizunguko mia tatu na sitini na nne, ambapo itakuwa ni sawa na Tawafu hamsini na mbili kila Tawafu ikiwa na mizunguko saba, hiyo ni iwapo anaweza hilo. Kama hawezи basi atatufu kadiri awezavyo, kwani Tawafu ni sawa na Sala akitaka afanye kwa uchache na akipenda afanye kwa wingi. Tawafu ni bora kuliko Sala kwa mtu aliye jirani na Msikiti Mtukufu na mkazi wa Makka.
7. Kunywa maji ya Zamzam. Imam as-Sadiq (a.s.) amesema: “Maji bora katika sura ya ardhi ni maji ya Zamzam.” Ni lazima hiyo iwe ni kwa sababu yapo

ndani ya Msikiti Mtukufu, au jirani na Ka'ba tukufu, na jirani na wenyе kukunuti, kurukuu, kusujudu na kutufu usiku na mchana, mionganі mwa watu wema, wabora na malaika watakatifu. Mtume (s.a.w.w.) alikuwa akiomba aletewe zawadi ya maji hayo hali akiwa Madina. Na Imam as-Sadiq (a.s.) anasema: "Maji ya Zamzam ni tiba ya nia yatakayonyewa."

Ubora wa maeneo matakatifu ndani ya Msikiti Mtukufu:

1. **Ka'ba:** Yenyewe ndio kilele cha matumaini ya muumini mwenye kuielekea, mwenye kutambua na mwenye kumkusudia Mungu. Wana shauku nayo bila kuijua na wanaielekea wakiwa nchi kavu, angani na baharini. Ukiitizama sema:

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الَّذِي عَظَّمَكَ وَشَرَّفَكَ وَجَعَلَكَ مَثَابَةً لِلنَّاسِ وَأَمْنًا
مُبَارَكًا وَهُدًى لِّلْعَالَمِينَ

"Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye amekutukuza, amekusharifu, amekupa heshima na amekufanya marejeo ya watu na mahala pa amani, penye kubarikiwa na mwongozo kwa viumbе. "

Ni mustahabu kukithirisha kuitazama Ka'ba. Mtume (s.a.w.w.) amesema: "Kuitizama Ka'ba kwa kuipenda kunasambaratisha kabisa makosa." Na imepokewa toka kwa Imam Ali (a.s.) kwamba alisema: "Mahujaji mtakapotoka kwenda kwenye Nyumba ya Mwenyezi Mungu basi kithirisheni kuitazama Nyumba ya Mwenyezi Mungu, kwani hakika Mwenyezi Mungu ana rehema mia

moja na ishirini katika Nyumba Yake Tukufu, sitini ni kwa ajili ya wenyewe kuitufu, arubaini kwa ajili ya wenyewe kusali humo, na ishirini kwa ajili ya wenyewe kuitazama.”

2. **Zamzam:** Tayari umeshajua ubora wa maji yake na kwamba ni mustahabu kuyanywa, bali ni mustahabu kuyanywa mpaka utosheke. Na katika baadhi ya hadithi ni kwamba: “Atakayekunywa maji ya Zamzam atakuwa amejipa dawa na amejiondolea ugonjwa.” Na ni mustahabu kuyabeba, kuyatoa zawadi na kuomba uletewe kama zawadi, utakapokunywa maji hayo sema:

أَللّٰهُمَّ اجْعِلْنِي عَلٰيْا نَافِعًا وَرِزْقًا وَسِعًًا وَشِفَاءً مِنْ كُلِّ دَاعٍ
وَسُقْمٌ بِسْمِ اللّٰهِ وَبِاللّٰهِ وَالشَّكْرِ اللّٰهِ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Yafanye elimu yenyewe manufaa, riziki pana na dawa ya kila gonjwa na ugonjwa.Kwa jina la Mwenyezi Mungu, kwa haki ya Mwenyezi Mungu na shukrani ni kwa Mwenyezi Mungu.”

3. **Jiwe Jeusi:** Hapo ndipo inapoanzia na kuishia Tawafu yako. Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Hakuna yeyote mwenye kuitufu Nyumba hii wakati wa kukengeuka jua hali ameacha wazi kichwa chake, yuko peku, anatembea kwa hatua fupifupi, ameangusha macho yake na akaligusa Jiwe katika kila Tawafu bila ya kumuudhi yeyote na akawa hakati utajo wa Mwenyezi Mungu ulimini kwake, ila ni lazima Mwenyezi Mungu atamwandikia kwa kila hatua moja mema elfu sabini, atamfutia makosa elfu sabini, atampandisha daraja

elfu sabini, na atampa thawabu za aliywapa uhuru watumwa elfu sabini kila mtumwa akiwa na thamani ya dirhamu elfu kumi, atampa nafasi ya kuwaombea watu sabini wa nyumba yake na atakidhiwa haja elfu sabini, ima duniani akitaka na ima Akhera akitaka.” Zimepokewa habari nyingi kwa fadhila zake na kuanza kuumbwa kwake.

Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) amesema: “Iguseni nguzo (yaani nguzo ambayo lipo jiwe hilo) kwani hakika yenyewe ni yamini ya Mwenyezi Mungu kwa viumbe wake, kwayo huwapa mkono viumbe wake upajji apewao mtumwa....” Ni mustahabu kulibusu, usipoweza basi liguse na kama huwezi bali liashirie, na sema:

أَمَانَتِي أَدِّيْتُهَا وَمِيثَاقَ تَعَاهُدِتِهِ لَتَشَهَّدَ لِي بِالْبَوَافَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Amana yangu nimeitekeleza na ahadi yangu nimeitimiza ili initolee ushahidi kwamba nimetekeleza.”

Kama ilivyotangulia.

4. **al-Hatim (kisambaratishi):** Nalo ni eneo lililopo kati ya Ka’ba Tukufu na Jiwe Jeusi, nalo ni mionganoni mwa maeneo matukufu na ni lazima kuomba toba na maghufira hapo, kusali hapo, kuomba dua na kushikilia kitambaa cha Ka’ba, kitendo hicho husambaratisha madhambi makubwa, na ndio maana likaitwa al-Hatim (kisambaratishi). Na katika baadhi ya habari ni kwamba ni eneo ambalo Mwenyezi Mungu alimkubalia hapo Adam (a.s.) toba yake.

5. **Maqam Ibrahim (a.s.):** Mwenyezi Mungu amesema: “Na mpafanye mahala aliposimama Ibrahim pawe pa kusali”, jina lake linatoshwa kubainisha fadhila zake, kwani ni cheo kipi unachofikiria kipo juu kushinda cheo cha halili kwa Mola Wake Jalili, ambaye aliitoa nafsi yake, ahli zake na mali yake katika njia ya Tauhid, katika kuweka alama tukufu na katika kujenga Ka’ba ndani ya Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu akashukuru baadhi ya tabu zake kwa kuuweka unabii katika kizazi chake na dini nyooofu ya milele katika njia yake na mila yake.
6. **Shadharuwani:** Nalo ni sehemu iliyobaki toka kwenye msingi wa ukuta wa Nyumba na ambayo hairuhusiwi kuivuka wakati wa kutufu.
7. **Nguzo ya Iraki:**
8. **Uzio wa Ismail:** Uzio ni nyumba ya Ismail (a.s.) na humo ndimo lilimo kaburi la Hajar na kaburi la Ismail. Na katika riwaya ya al-Halbiy kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) ni kwamba alisema: Nilimuuliza kuhusu Uzio akasema: “Ninyi mnauita al-Hatim (kisambaratishi) na lilikuwa (eneo) la kondoo wa Ismail, alizikwa humo mama yake na hakupenda kaburi lake likanyagwe hivyo akaliwekea uzio, na humo mna makaburi ya Manabii (a.s.).” Na Baqir (a.s.) amesema: “Hakika eneo lililopo kati ya nguzo na Maqam limesheheni makaburi ya Manabii (a.s.).”

Na as-Sadiq (a.s.) amesema: “Eneo lililopo kati ya nguzo ya Yemen na Jiwe Jeusi lina Manabii sabini, katika sehemu hii tukufu utamzuru Ismail, mama yake na Manabii wengine (a.s.).” Itafuata Ziyara katika faslu ya nne, na ni

mustahabu kuhirimia Hijja ya Tamatui katika Uzio huku ukiwa mkabala na Bomba (*al-Mizabu*) la rehema, nalo ni eneo la dua na kuomba rehema toka Kwake kama ilivyotangulia.

9. **Bomba la rehema (*al-Mizabu*):** Ni mustahabu kulielekea Bomba (*al-Mizabu*) na kuomba dua zilizopokewa toka kwa Ahlul-Baiti (a.s.), hiyo ni kutokana na hadithi ya Ayyub kutoka kwa Sheikh yaani Musa bin Ja'far (a.s.) kwamba aliniambia: “Baba yangu alikuwa aelekeapo Bomba (*al-Mizabu*) husema:

اللَّهُمَّ فُكِنِي مِنَ النَّارِ، وَأَوْسِعْ عَلَيَّ مِنْ رِزْقَكَ الْخَلَالِ الطَّيِّبِ،
وَادْرُأْ عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ، وَشَرَّ فَسَقَةِ الْعَرَبِ
وَالْعَجمِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nikomboe na moto, nipanulie riziki Yako ya halali na niondolee shari ya mafasiki wa kijini na wa kibinadamu.”

Na katika habari nyingine kutoka kwa Abu Abdillah (a.s.) kwamba alisema: “Ali bin Husain (a.s.) alikuwa afikapo kwenye Uzio kabla hajafika kwenye Bomba (*al-Mizabu*) huinua kichwa chake na husema hali akilitizama Bomba (*al-Mizabu*):

اللَّهُمَّ أَدْخِنِي الْجَنَّةَ بِرَحْمَتِكَ وَأَجْنِي بِرَحْمَتِكَ مِنَ النَّارِ وَ

عافني من السقم وأوسع علىَ مِنْ رُنِيقَ الْحَلَالِ الطَّيِّبِ،
 وَادْرُأْ عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْإِنْسِ، وَشَرَّ فَسَقَةِ الْعَرَبِ
 وَالْعَجمِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Niingize Peponi kwa rehema Zako. Na kwa rehema Zako niepushe na moto, niponye na magonjwa, nipanulie riziki ya halali iliyo nzuri, na niondolee shari ya mafasiki wa kijini na wa kibinadamu, na shari ya mafasiki wa kiarabu na wasiokuwa waarabu.”

10. **Nguzo ya Sham:** Ni mustahabu kuzigusa nguzo zote kutokana na hadithi iliyopokewa kutoka kwa Jamili bin Salih kwamba alimuona Abu Abdillah (a.s.) akizigusa nguzo zote. Ndio, msisitizo zaidi ni kwenye nguzo ya Yemeni na nguzo ambayo lipo Jiwe Jeusi. Na kutokana na habari zilizopokewa tunastafidi kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) alikuwa anazigusa mara kwa mara.

Hii yote ni iwapo tu hakuna hali ya kuwabughudhi watu, la sivyo itakuwa si mustahabu bali ni haramu. Kisha hakika Nguzo ya Mashariki ndio nguzo ya Jiwe Jeusi, na Nguzo ya Kaskazini ndio ile ya baada ya mlango wa Ka’ba Tukufu kabla hujafika kwenye Uzio wa Ismail, na inajulikana kwa jina la Nguzo ya Iraki, na pia huitwa Nguzo ya Shamu. Na Nguzo ya Magharibi ni ile iliyopo baada ya Uzio wa Ismail na inaitwa Nguzo ya Shamu. Na Nguzo ya Kusini ni ile iliyopo kabla ya Nguzo ya Jiwe Jeusi, nayo huitwa Nguzo ya Yemeni. Na linalopatika katika kitabu *al-Jawahiru* Juz. 19, Uk. 415 ni kwamba

Nguzo ya Iraki ndio Nguzo ya Jiwe Jeusi. Katika hadithi kutoka kwa Ibnu Mahmud amesema: Nilimwambia Ridha (a.s.): Je napaswa kugusa Nguzo ya Yemen, Sham, Irak na Magharibi? Akasema ndio.

11. ***al-Mustajaru (Lililohifadhiwa)***: Eneo ambalo lipo usawa wa mlango wa Ka'ba kwa nyuma ya Nyumba linaitwa *al-Mustajaru*(Lililohifadhiwa), *al-Mutaawadhu* (Lililolindwa) na *al-Multazamu* (Lililofuatiliwa), kuhusu ubora wake zimepokewa habari nyingi, Ali (a.s.) amesema: “Ungameni kwenye *al-Multazamu* (Lililofatiliwa) dhambi zenu mlizozihifadhi, na zile ambazo hamjazihifadhi semenii: Na zile walizozihifadhi juu yetu watunza kumbukumbu Wako nasi tumezisahau nazo tughufirie.” Kwa hakika atakayeungama dhambi zake eneo hilo, akaziorodhesha, akazitaja na akaomba maghfira ni haki juu ya Mwenyezi Mungu kumghufiria. Na katika sahihi ya Ibnu Ammara ni kwamba Abu Abdillah (a.s.) alikuwa afikapo *al-Multazamu* (Lililofatiliwa) huwaambia watumwa wake: ‘Nipisheni ili niungame dhambi zangu kwa Mola Wangu Mlezi katika eneo hili, kwani katika eneo hili mja hataungama dhambi zake kwa Mola wake Mlezi kisha akaomba maghfira ila ni lazima Mwenyezi Mungu atamghufiria.’”

Na katika hadithi nyingine ni kwamba Adam alipoitufu Nyumba na kufika *al-Multazamu*, Jibril (a.s.) alimwambia: “Ewe Adam! Ungama dhambi zako kwa Mola Wako Mlezi katika sehemu hii.” Baada ya kufanya hivyo ndipo Mwenyezi Mungu akampelekea wahyi: Ewe Adam! Nimeshakusamehe dhambi yako. Adam akasema: “Ewe Mola Wangu Mlezi! Je na kizazi changu?” Mwenyezi

Mungu akampelekea wahyi: Ewe Adam! yeote katika kizazi chako atakayekuja sehemu hii na akaungama dhambi zake na kutubu kama ulivyotubu kisha akaomba kughufiriwa basi nitamghufiria.” Na ni mustahabu mwenye kutufu katika mzunguko wa saba au baada ya kumaliza kutufu aweke mikono yake juu ya Nyumba kwa kuikunjua, na aambatanishe mwili wake na shavu lake na Nyumba hiyo, na aombe dua aliyoomba Abu Abdilla as-Sadiq (a.s.) sehemu hii, nayo ni:

أَللّٰهُمَّ الْبَيْتُ بَيْتُكَ، وَالْعَبْدُ عَبْدُكَ، وَهَذَا مَقَامُ الْعَائِدِ بِكَ
 مِنَ النَّارِ أَللّٰهُمَّ مِنْ قَبْلِكَ الرَّوْحُ وَالْفَرْجُ وَالْعَافِيَةُ. أَللّٰهُمَّ إِنَّ
 عَمَلِي ضَعِيفٌ فَضَاعِفْهُ لِي، وَاغْفِرْ لِي مَا اطْلَعْتَ عَلَيْهِ مِثْنَى وَخَفْنَى
 عَلَى خَلْقِكَ، أَسْتَجِيرُ بِاللّٰهِ مِنَ النَّارِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nyumba hii ni nyumba Yako, mja huyu nimja Wako na hikini kisimamo cha aliyejikinga Kwako na moto. Ewe Mwenyezi Mungu! Rehema, faraja na afya ni kutoka Kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika amali yangu ni dhaifu hivyo iongeze kwa ajili yangu na unighufirie yale uliyoyajua toka kwangu na yakafichika kwa viumbi Wako. Naomba hifadhi kwa Mwenyezi Mungu dhidi ya moto.”

Nguzo ya Yemeni: Kona iliyo usawa wa Jiwe Jeusi kwa nyuma ya Nyumba huitwa Nguzo ya Yemeni. Kuhusu fadhila zake zimepokewaa habari nyingi zinazostaajabisha akili. Mtume (s.a.w.w.) amesema: “Sikuja kwenye Nguzo

ya Yemen ila nilimkuta Jibril akiwa ameshanitangulia bila kuiacha.” Abu Abdillah (a.s.) amesema: “Nguzo ya Yemen ni mlango wetu ambao tunaingilia peponi.” Na akasema tena: “Na hapo kuna mlango mionganoni mwa milango ya pepo, haujafungwa tangu ulipofunguliwa, na hapo pana mto mionganoni mwa mito ya peponi ambao ndani yake hutupiwa matendo ya waja.” Akasema tena (a.s.): “Malaika aliyekabidhiwa Nguzo ya Yeme ni tangu Mwenyezi Mungu alipoumba mbingu na ardhi hana kazi ila kuitikia dua zenu, hivyo achunguze mja ni kipi anachoomba.” Ni lazima mtu atumie ipasavyo fursa ya wakati na hali katika eneo hili tukufu, na ni mustahabu kwamba aombe katika eneo hili tukufu ile dua aliyoomba Abu Hasan Ridha (a.s.) alipokuwa usawa wake baada ya kuwa ameinua mikono yake, nayo ni:

يَا أَللَّهُ يَا وَلِيَ الْعَافِيَةِ، وَخَالِقَ الْعَافِيَةِ، وَرَازِقَ
 الْعَافِيَةِ، وَالْبَنِينَعَمْ بِالْعَافِيَةِ، وَالْبَشَّانَ بِالْعَافِيَةِ، وَالْمُتَفَضِّلُ
 بِالْعَافِيَةِ عَلَى وَعَلَى جَيْبِع خَلْقِكَ، يَا رَحْمَانَ الدُّنْيَا وَالْآخِرَةِ وَ
 رَحِيمَهُمَا، صَلَّى عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ، وَارْزُقْنَا الْعَافِيَةَ، وَ
 دَوَامَ الْعَافِيَةِ، وَتَامَ الْعَافِيَةِ، وَشُكْرَ الْعَافِيَةِ فِي الدُّنْيَا
 وَالْآخِرَةِ، يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mmiliki wa afya, Muumba wa afya, Mwenye kuruzuku afya, Mwenye kuneemeshaa

afya, Mpaji wa afya na Mwenye kunifadhili afya mimi na viumbe Wako wote! Ewe Rahman duniani na Akhera na uliye Rahimu humo! Msalie Muhammad na aali Muhammad, na turuzuku afya, kudumu katika afya, utimilifu wa afya na kushukuru afya duniani na Akhera, kwa rehema Zako ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Mambo yaliyo mustahabu wakati wa kuingia Ka’ba Tukufu:

Ni mustahabu kuingia ndani ya Ka’ba Tukufu, katika Hadithi imepokewa kwamba: Kuingia humo ni kuingia katika rehema za Mwenyezi Mungu, na kutoka humo ni kujivua toka kwenye dhambi. Na Sunnah hii ni ya mkazo kwa yule anayehiji kwa mara ya kwanza, ndio si Sunnah ya mkazo kwa wanawake. Mambo yaliyo mustahabu katika kuingia humo ni haya yafuatayo:

1. Kuoga kabla ya kuingia Ka’ba Tukufu.
2. Kuingia ndani ya Ka’ba Tukufu bila viatu.
3. Wakati wa kuingia aseme:

اللَّهُمَّ أَنْتَ قَلْتَ فِي كِتَابِكَ وَمَنْ دَخَلَهُ كَانَ آمِنًا فَأَمِنْتُ مِنْ
عِذَابِكَ عِذَابَ النَّارِ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Wewe umesema ndani ya Kitabu Chako: ‘Atakayeetingia atakuwa katika amani.’ Basi nisalimishe na adhabu Yako, adhabu ya moto.”

Bali kwa yule anayehiji kwa mara ya kwanza inampasa aseme maneno hayo katika pembe zote.

1. Atende amali aliyopokea Muawiya bin Ammar kutoka kwa as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: “Ukitaka mtoto jiwagie ndoo ya maji ya Zamzam kisha iingie Nyumba, ukisimama mlangoni shika upande mmoja wa mlangano na useme:

اللَّهُمَّ إِنَّ الْبَيْتَ يَبْتَكُ وَالْعَبْدُ عَبْدُكَ وَقَدْ قَلْتَ مِنْ دُخْلِهِ كَانَ

آمَنَّا فَآمَنَّا مِنْ عَذَابِكَ وَأَجْرَنَا مِنْ سُخطِكَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Nyumba hii ni nyumba Yako na mja huyu ni mja Wako na umeshasema atakayejiingia atakuwa katika amani, basi nisalimishe na adhabu Yako na niepushe na ghadhabu Yako.”

2. Kusali rakaa mbili juu ya marumaru nyekundu, kisha unakwenda kwenye nguzo iliyo mkabala na Jiwe na kuiambatanisha na kifua chako, kisha sema:

يَا وَاحِدٌ يَا مَاجِدٌ يَا قَرِيبٌ يَا بَعِيدٌ يَا عَزِيزٌ يَا حَكِيمٌ لَا

تَذَرْنِي فَرَدًا وَأَنْتَ خَيْرُ الْوَارثَيْنَ وَهُبْ لِي ذَرْرَيْةً إِنَّكَ سَيِّعٌ

.الدُّعَاءُ.

“Ewe Mmoja! Ewe wa Pekee! Ewe Mtukuka! Ewe Uliye karibu! Ewe Uliye mbali! Ewe Mwenye nguvu! Ewe

Mwenye hekima! Usiniache peke yangu na Wewe ndio mrithi bora kushinda wote wanaorithi, na nipe kizazi hakika Wewe ni Msikivu wa dua.”

Kisha izunguke nguzo na uiambatanishe na mgongo Wako na tumbo lako, na uombe dua iliyotangulia.

3. Kusali rakaa mbili baina ya nguzo mbili juu ya marumaru nyekundu, katika rakaa ya kwanza soma Alhamdu na Sura Haa Miim Sajda, katika rakaa ya pili soma Alhamdu na Aya hamsini na tano ambazo ni sawa na idadi ya Sura Haa Miim Sajda.
4. Kusali kwenye pembe za Nyumba, katika kila pembe rakaa mbili.
5. Useme:

يَا إِلَهِ وَسَيِّدِي مَنْ تَهَيَّأَ أَوْ تَعَبَّأَ أَوْ أَعَدَّ أَوْ اسْتَعَدَ لِوِفَادَةِ
مَخْلُوقٍ رَجَاءً رِفْدٍ وَفَوَائِدٍ وَنَائِلِهِ وَفَوَاضِلِهِ وَجَوَائِزِهِ فَالْيُكَّ
يَا إِلَهِ كَانَتْ تَهِيَّتِي وَتَعَبَّتِي وَإِعْدَادِي وَاسْتِعْدَادِي رَجَاءً
فَوَائِدِكَ وَمَعْرُوفِكَ وَنَائِلِكَ وَجَوَائِزِكَ فَلَا تُخَيِّبُنِي مِنْ ذَلِكَ يَا
مَنْ لَا تَخِيبُ عَلَيْهِ مَسْأَلَةُ السَّائِلِ وَلَا تَنْقُصُهُ عَطِيَّةُ نَائِلٍ، فَانِّي
لَمْ آتِكَ بَعَيْلَ صَالِحٍ قَدَّمْتُهُ وَلَا شَفَاعَةٌ مَخْلُوقٍ رَجَوْتُهُ أَتَيْتُكَ

مُقِرّاً عَلَى نَفْسِي بِالْأُسْعَةِ وَالْعُلُمِ مُعْتَرِفًا بِأَنْ لَا حُجَّةَ لِي وَلَا
 عُذْرَ فَأَسْأَلُكَ يَا مَنْ هُوَ كَذِيلَكَ أَنْ تُصْلِيَ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ
 وَتُعْطِينِي مَسْأَلَتِي وَتُقِيلَنِي عَثْقَ وَتَقْلِيَنِي بِرَغْبَتِي، وَلَا تَرْدَنِي
 مَجْبُوهًا مَمْنُوعًا وَلَا خَائِبًا، يَا عَظِيمُ يَا عَظِيمُ يَا عَظِيمُ أَرْجُوكَ
 لِلْعَظِيمِ، أَسْأَلُكَ يَا عَظِيمُ أَنْ تَغْفِرِي الذَّنْبَ الْعَظِيمَ لِإِلَهِ إِلَّا أَنْتَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Atakaye jitayarisha na akajiandaa, akafanya maandalizi na akajiandaa kuwa mgeni wa kiumbe hutaraji msaada wake, zawadi yake, hiba zake na fadhila zake, basi utayarifu wangu, maandalizi yangu na kujianaa kwangu ni kwa ajili ya kuja Kwako Ewe Bwana Wangu huku nikitaraji msaada Wako, hiba Zako na zawadi Yako, basi usiyarudishe tupu matarajio yangu ewe Ambaye muombaji hakatishwi tamaa Naye na wala mchukua ji hampunguzii chochote. Kwani hakika mimi sijakujia leo na hali ni mwenye amali njema niliyoitanguliza wala na uombezi wa kiumbe nilioutaraji, lakini nimekujia na hali ni mwenye kuungama dhulma na ubaya nilioitendea nafsi yangu, kwa kweli sina hoja wala udhuru, hivyo nakuomba ewe Ambaye ndivyo ulivyo umswalie Muhammad na aali Muhammad, na unipe ombi langu, ufumbie macho kuteleza kwangu, unirudishe na raghba yangu, na wala usinirudishe na hali ni mwenye kunyimwa, kukataliwa wala kutofanikiwa. Ewe Adhimu! Ewe Adhimu! Ewe Adhimu! Nakutaraji kwa jambo adhimu. Nakuomba Ewe Adhimu unighufirie dhambi adhimu, hakuna mungu ila Wewe.”

6. Kuielekea kila pembe kati ya pembe za Nyumba Tukufu hapo ulipo ikiwa msongamano utakuzuia kuzifikia.
7. Kuomba dua na kujinyenyekesha kwa Mwenyezi Mungu, kumtukuza na kumuomba hali ukiwa sehemu uliyosalia.
8. Kusujudu ndani ya Ka'ba huku katika sijda yako ukisema yale aliyoyasema Imam Abu Abdillah as-Sadiq (a.s.):

لَا يَرِدُ غَضِيبَكَ إِلَّا حِلْمُكَ وَلَا يُنْجِي مِنْ سَخِطِكَ إِلَّا التَّضَرُّعُ إِلَيْكَ
 فَهَبْ لِي يَا إِلَهِي فَرَجًا بِالْقُدْرَةِ الَّتِي تُحْيِي بِهَا مَيْتَ الْبِلَادِ وَلَا
 تُهْلِكْنِي غَيْرًا حَتَّى تَسْتَجِيبَ لِي وَتُعَرِّفَنِي الْإِجَابَةَ فِي دُعَائِي
 وَأَذْقِنِي طَعْمَ الْعَافِيَةِ إِلَى مُنْتَهِي أَجَلِي وَلَا تُشْتِتِ بِي عَدُوّي وَلَا
 تُسْلِطْهُ عَلَيَّ وَلَا تُمْكِنْهُ مِنْ عَنْقِي اللَّهُمَّ (إِلَهِي) إِنْ وَضَعْتَنِي
 فَبَنْ ذَا الَّذِي يَرْفَعُنِي وَإِنْ رَفَعْتَنِي فَبَنْ ذَا الَّذِي يَضْعُنِي وَإِنْ
 آهُلَكْتَنِي فَبَنْ ذَا الَّذِي يَعْرِضُ لَكَ فِي عَبْدِكَ أَوْ يَسْأَلُكَ عَنْ
 أَمْرِهِ

وَقُدْ عَلِيْتُ أَنَّهُ لَيْسَ فِي حُكْمِكَ ظُلْمٌ وَلَا فِي نَقْبَتِكَ عَجَلَةً وَإِنَّا
 يَعْجَلُ مَنْ يَخَافُ الْفَوْتَ وَإِنَّهَا يَحْتَاجُ إِلَى الظُّلْمِ الْضَّعِيفِ وَقُدْ
 تَعَالَيْتَ يَا إِلَهِ عَنْ ذَلِكَ عُلُوًّا كَبِيرًا إِلَهِ فَلَا تَجْعَلْنِي لِلْبَلَاءِ
 عَرَضًا وَلَا لِنَقْبَتِكَ نَصْبًا وَمَهْلِكَةً وَنَفْسِي وَأَقْلَنِي عَثْنَقَ وَلَا تَرَدَّ
 يَدِي فِي نَحْرِي وَلَا تَتَبَعْنِي بَلَاءً عَلَى إِثْرِ بَلَاءِ قَدْ تَرَى ضَعْفِي
 وَتَضَرِّعِي إِلَيْكَ وَوَحْشَتِي مِنَ النَّاسِ وَأَنْسِي بِكَ

 وَأَعُوذُ بِكَ الْيَوْمَ فَأَعْذُنِي وَأَسْتَجِيرُ بِكَ فَأَجْرِنِي وَأَسْتَعِينُ بِكَ
 عَلَى الظَّرَاءِ فَأَعْنَى وَأَسْتَنْصِرُكَ فَانْصَرْنِي وَأَتَوَكَّلُ عَلَيْكَ فَاكْفُنِي
 وَأَوْمَنُ بِكَ فَآمِنُّى وَأَسْتَهْدِيكَ فَاهْدِنِي. وَاسْتَرْحِكَ فَارْحَنِي
 وَاسْتَغْفِرِكَ مَمَّا تَعْلَمَ فَاغْفِرْلِي وَأَسْتَرْزِقِكَ مِنْ فَضْلِكَ الْوَاسِعِ
 فَارْنَقْنِي وَلَا حُولَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ

“Haizuii ghadhabu Yako ila upole Wako, haiepushi adhababu Yako ila rehema Zako, haokoi dhidi Yako ila kujinyenyekesha Kwako, hivyo nipe Ilahi! furaha kwa uwemo Wako ambaao kwao unahuisha wafu mionganii mwa waja, na kwao unawafufua maiti wa nchi. Wala

usiniangamize Ilahi! Mpaka uwe umejibu dua yangu na kunijulisha majibu. Niruzuku utamu wa afya njema mpaka mwisho wa muda wangu, wala usimfurahishe adui yangu kupitia kwangu na wala usimpe nguvu juu yangu wala usimmakinishe shingo yangu. Ni nani atakayeninyanya ikiwa utanibwaga, na ni nani atakayenibwaga ikiwa utaninyanya, na ikiwa utaniangamiza ni nani atakayekushtaki kuhusu mja Wako na kukuuliza kuhusu jambo lake!

“Nimeshajua Ilahi! Kwamba katika hukumu Yako hakuna dhulma, wala katika adhabu Yako hakuna haraka, kwani bila shaka hufanya haraka yule anayehofia kuitwa, na huhitaji dhulma yule aliye dhaifu, Nawe Ewe Mungu Wangu umetukuka na yote hayo! Ilahi! usinifanye madhihirikio ya balaa wala fungu la ghadhabu Yako, nipe muda mimi na nafsi yangu, fumbia macho kujikwaa kwangu na wala usiirudishe mikono yangu shingoni mwangu, na wala usinifululizie balaa baada ya balaa, kwani bila shaka umeshauona udhaifu wangu, unyenyekevu wangu Kwako, kutengwa kwangu na watu na jinsi ninavyojiliwaza Nawe.

“Najilinda Kwako leo hivyo nilinde, naomba hifadhi Kwako hivyo nipe hifadhi, naomba msaada Kwako juu ya dhara hivyo nisaidie, naomba nusra Kwako hivyo ninusuru, natawakali Kwako hivyo nitoshe, ninakuamini Wewe hivyo nisalimishe, nakuomba uongofu hivyo niongoe, nakuomba rehema hivyo nirehemu, nakuomba maghufira kutokana na yale unayoyajua hivyo nighufirie, na ninakuomba riziki toka kwenye fadhila Zako pana hivyo niruzuku, na hakuna uwezo wala nguvu ila toka kwa Mwenyezi Mungu Aliye juu aliye Adhimu.”

9. Ni mustahabu kuangua kilio humo na nyuma yake

kwa kumhofu Mwenyezi Mungu, kwani as-Sadiq (a.s.) amesema: “Hakika Ka’ba alipewa jina la *Bakati* kwa sababu ya watu kuangua kilio humo na nyuma yake.

10. Ni mustahabu wakati wa kutoka Ka’ba Tukufu kutoa takbira mara tatu.
11. Aseme yale aliyopokea Imam Abu Abdillah (a.s.), nayo ni:

اللّٰهُمَّ لَا تَجْهِدْ بَلَائِنَا، رَبَّنَا وَلَا تُشْبِثْ بِنَا أَعْدَاءَنَا، فِإِنَّكَ أَنْتَ
الضَّارُّ الشَّافِعُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usiongeze balaa letu ewe Mola wetu Mlezi na wala usiwafurahishe maadui zetu kupitia kwetu, kwani hakika Wewe ni Mwenye kudhuru Mwenye kunufaisha.”

12. Wakati wa kutoka atasali rakaa mbili, na ni karaha kutema mate na kikohozi ndani ya Nyumba na ndani ya Ka’ba Tukufu.
13. Utasoma dua hii eneo alilozaliwa Amirul-Muuminina (a.s.):

اللّٰهُمَّ نُورْ بِالْعِلْمِ قَلْبِي وَاسْتَعِيلْ بِطَاعَتِكَ بَدْنِي وَخَلْصِنِي مِنْ
الْفَتْنَ وَأَشْغِلْ بِالْإِعْتِبَارِ فَكْرِي وَقُنْيَ شَرِّ وَسَاوِسِ الشَّيْطَانَ

وأجرب منه يا رحمن بالصالحات أعيالنا اللهم إِنّي أودعك
نفسى في هذا المحلول الشهيف إلى يوم القيمة خالصاً مخلصاً
أشهد أن لا إله إلا الله وأنّ محمداً عبده ورسوله.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ng’arisha moyo wangu kwa elimu, ushughulishe mwili wangu katika kukutii Wewe, niokoe na fitina, ishughulishe fikra yangu na mazingatio, nikinge na shari ya vishawishi vyta shetani na niepushe naye ewe Mwingi wa rehema kuitia vyenye kutengeneza matendo yetu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeiweka amana nafsi yangu mahali hapa patukufu mpaka Siku ya Kiyama na hali ni mwenye ikhlasi nisiye na shaka. Nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah, na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

FASLU YA SITA

KUYAZURU MAKABURI HUKO MAKKA

Alhajuni ndio eneo la makaburi lililo tukufu baada ya Baqii, nalo ndio eneo ambalo alikuwa akilizuru Mtume (s.a.w.w.) mara kwa mara, na hapo ndipo alipozikwa Abdul-Mutalib na Abdul-Manafi mababu wa Mtume (s.a.w.w.), na pia ndipo lilipo kaburi la Abu Talib ami yake Mtume (s.a.w.w.) na baba mzazi wa Amirul-Muuminina (a.s.), na ndipo lilipo kaburi la mke wa Mtume (s.a.w.w.) Khadija mama wa waumini. Mionganii mwa wema wa watoto kwa mama yao ni kulizuru kaburi lake baada ya kufariki kwake, zaidi ya hapo ni zile juhudzi zake alizotoa katika kumtumikia bwana wa Mitume (s.a.w.w.), kujitolea kwake katika kusambaza ujumbe wa Mwisho wa Mitume (s.a.w.w.) na mengineyo mwa fakhari zake ambazo zimejaa vitabu vya madhehebu zote. Hivyo baada ya hayo atakayetilia shaka uzito wa kumzuru basi atakuwa hakumtendea mama yake wema. Na pia hapo pana kaburi la mama wa Mtume (s.a.w.w.) Amina na mwanawee Qasim kwa yule anayeona kuwa kaburi lake lipo hapo.

Mwandishi wa kitabu *Wafaul-Wafai* amesema kwamba kaburi la Amina binti Wahbi lipo Abwau baina ya Makka na Madina. Na mwandishi wa kitabu *Jamiul-Latif* amesema kwamba kaburi la Maymuna mke wa Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) lipo Saraf umbali wa farsakhu mbili tokea Makka. Na kutoka katika kitabu *Muntakhabut-Tawarikh* ni kwamba kaburi la Abdullah bin Ismail bin Badhii lipo Filu karibu na Makka, na babu yake alikuwa mionganii mwa masahaba wa Imam al-Baqir, Imam as-Sadiq, Imam Musa bin Ja'far na Imam Ali bin Musa ar-Ridha (a.s.).

Na miongoni mwa maeneo ya kufanyiwa ziara ni Fukh, nalo ni eneo ambalo yalitokea mapambano na hapo wakauwawa watu mia moja toka kizazi cha Fatima (a.s.) mikononi mwa kibaraka Musa al-Hadi al-Abbasiy, hao utawazuru kupitia ziyara ya Ismail bin as-Sadiq (a.s.) iliyo tangulia. Al-Muhaddith al-Qummiy amesema ndani ya kitabu chake *al-Kunniy Wal-Alqab* akinukuu toka kwa Imam al-Jawad (a.s.) kwamba: Baada ya Tuf (Karbala) hatuna eneo la mauwaji makubwa kushinda Fukh. Na Da'bal akaashiria hilo katika beti za mashairi yake:

*Makaburi yako Kufani (Karbala)na mengine Twiba,
na mengine Fukh, sala zangu ziyafikiye.*

Mwandishi wa kitabu *Muntakhabut-Tawarikh* amesema kwamba katika makaburi ya al-Juhuni kuna makaburi ya baadhi ya ulamaa.

**Ziyara ya Abdu Manafi, babu yake Mtume
(s.a.w.w.):**

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّهَا السَّيِّدُ التَّبِيلُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّهَا الْغُصْنُ
الْمُشْرِّمُ مِنْ شَجَرَةِ إِبْرَاهِيمَ الْخَلِيلِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا جَدَّ خَيْرِ
الْوَرَى، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الْأَنْبِياءِ الْأَصْفِيَاءِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ
يَا ابْنَ الْأُوْلِيَاءِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَ الْحَرَمِ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ مَقَامِ إِبْرَاهِيمَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَاحِبَ

بَيِّنَتِ اللَّهُ الْعَظِيمُ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى آبَائِكَ الطَّاهِرِينَ وَرَحْمَةً

الله وبركاته

“Amani iwe juu yako ewe bwana mwema! Amani iwe juu yako ewe tawi litoalo matunda toka katika mti wa Ibrahim khalili! Amani iwe juu yako ewe babu wa mbora wa viumbe! Amani iwe juu yako ewe mwana wa Manabii wateule! Amani iwe juu yako ewe mwana wa Mawasii wema! Amani iwe juu yako ewe bwana wa Eneo Takatifu (*al-Haram*)! Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Maqam Ibrahim! Amani iwe juu yako ewe mhusika wa Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako na juu ya baba zako na wanao watakasifu, pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! ”

Ziyara ya Abdul-Mutalib babu wa Mtukufu Mtume (s.a.w.w.):

أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَ الْبَطْحَاءِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ نَادَاهُ
هَاتِفُ الْغَيْبِ بِأَكْرَمِ نِدَاءِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ إِبْرَاهِيمَ
الْخَلِيلِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا وَارِثَ الذَّبِيجِ إِسْمَاعِيلَ، أَلْسَلَامُ
عَلَيْكَ يَا مَنْ أَهْلَكَ اللَّهُ بِدُعَائِهِ أَصْحَابَ الْفِيلِ، وَجَعَلَ كَيْدَهُمْ
فِي تَضْلِيلٍ، وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَايِيلَ، تَرْمِيهِمْ بِحِجَارَةٍ مِنْ

سِجْيل، فَجَعَلَهُمْ كَعْصُفَ مَا كُولُ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ تَضَرَّعَ
فِي حَاجَاتِهِ إِلَى اللَّهِ، وَتَوَسَّلَ فِي دُعَائِهِ بِنُورِ رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنِ اسْتَجَابَ اللَّهُ دُعَاءً، وَنُودَى
فِي الْكَعْبَةِ، وَبُشِّرَ بِالْأُجَابَةِ فِي دُعَائِهِ، وَأَسْجَدَ اللَّهُ الْفِيلَ إِكْرَاماً
وَإِعْظَاماً لَهُ،

أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ أَنْبَعَ اللَّهُ لَهُ الْبَاءَ حَتَّى شَرَبَ وَارْتَوَى فِي
الْأَرْضِ الْقَفْرِاءِ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا ابْنَ الذَّبِيحِ وَأَبَا الذَّبِيحِ،
أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا سَاقِ الْحَبِيجِ وَحَافِرِ زَمْزَمِ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا
مَنْ جَعَلَ اللَّهُ مِنْ نَسْلِهِ سَيِّدَ الْمُرْسَلِينَ وَخَيْرَ أَهْلِ السَّمَاوَاتِ
وَالْأَرْضِينَ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ طَافَ حَوْلَ الْكَعْبَةِ وَجَعَلَهُ
سَبْعَةَ أَشْوَاطٍ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ رَأَى فِي الْبَنَامِ سِلْسِلَةَ
النُّورِ وَعَلِمَ أَنَّهُ مِنْ أَهْلِ الْجَنَّةِ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا شَيْبَةَ الْحَمْدِ،
أَللَّامُ عَلَيْكَ وَعَلَى آبَائِكَ وَأَجْدَادِكَ وَأَبْنَائِكَ جَيِيعًا وَرَحْمَةً

“Amani iwe juu yako ewe bwana wa vibonde (*Bat'hau*)! Amani iwe juu yako ewe ambaye sauti ya ghaibu ilimwita kwa wito mtukufu mno! Amani iwe juu yako ewe mwana wa Ibrahim khalili! Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Ismail Dhabihu! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu aliwaangamiza Watu wa Tembo (ndovu) kwa dua yake, akaharibu hila yao na akawapelekea juu yao ndege makundi makundi, wakawatupia mawe ya udongo mkavu na akawafanya kama majani yaliyoliwa! Amani iwe juu yako ewe ambaye alijinyenyekesha kwa Mwenyezi Mungu wakati wa haja yake na akatawassali katika dua yake kupitia nuru ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.)! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu alijibu dua yake, akaitwa katika Ka’ba, akabashiriwa jibu katika dua yake, na Mwenyezi Mungu akawasujudisha tembo kwa kumuenzi yeze na kumtukuzza yeze!

“Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu alimtolea chemchem ya maji akanywa na akatosheka katika ardhi kame! Amani iwe juu yako ewe mwana wa Dhabihu na baba wa Dhabihii! Amani iwe juu yako ewe mwenye kutoa huduma ya maji kwa mahujaji na mchimbaji wa Zamzam! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu amefanya bwana wa Mitume na mbora kushinda watu wote wa mbinguni na ardhini atoke katika kizazi chake! Amani iwe juu yako ewe ambaye aliiitufu Ka’ba na akafanya mizunguko saba! Amani iwe juu yako ewe ambaye aliona usingizini mlolongo wa nuru, na akajua kuwa ni mionganoni mwa watu wa peponi! Amani iwe juu yako ewe Shaybatul-Hamdi! Amani iwe juu yako, juu ya

baba zako, babu zako na wanao wote, na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! ”

Ziyara ya Abu Talib ami yake Mtume (s.a.w.w.):

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا سَيِّدَ الْبَطْحَاءِ وَابْنَ رَئِيسِهَا، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا
وَارِثَ الْكَعْبَةِ بَعْدَ تَأْسِيسِهَا، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا كَافِلَ الرَّسُولِ
وَنَاصِرَهُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا عَمَ الْمُصَفَّى وَأَبَا الْمُرْتَضَى، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا بَيْضَةَ الْبَلَدِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ أَلَّهَا الظَّابِ عَنِ الدِّينِ،
وَالْبَادِلُ نَفْسَهُ فِي نُصْرَةِ سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى
وَلَدِكَ أَمِيرِ الْبَوْمَنِينَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَّ كَاتِهِ

“Amani iwe juu yako ewe bwana wa al-Bat’hau na mwana wa Rais wake! Amani iwe juu yako ewe mrithi wa Ka’ba baada ya kuasiwiwa kwake! Amani iwe juu yako ewe mlezi wa Mtukufu Mtume na mnusuru wake! Amani iwe juu yako ewe ami wa al-Mustafa na baba wa al-Murtadha! Amani iwe juu yako ewe mzee wa mji! Amani iwe juu yako ewe aliyejitolea kwa ajili ya dini na kuitoa muhangaa nafsi yake katika kumtetea bwana wa Mitume! Amani iwe juu yako wewe na juu ya mtoto wako Amirul-Muuminina, na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! ”

Ziyara ya mama wa Mtume, Amina binti Wahb:

السَّلَامُ عَلَيْكَ أَيَّتُهَا الظَّاهِرَةُ الْبَطَّهَرَةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ
خَصَّهَا اللَّهُ بِأَعْلَى الشَّرَفِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ سَطَعَ مِنْ
جِبِينِهَا نُورٌ سَيِّدُ الْأَنْبِيَاءِ، فَأَضَاعَتْ بِهِ الْأَرْضُ وَالسَّمَاءُ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ نَزَّلْتُ لِأَجْلِهَا الْبَلَائِكَةُ، وَضَرَبْتُ لَهَا حِجْبَ
الْجَنَّةِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ نَزَّلْتُ لِخِدْمَتِهَا الْحُورُ الْعِينُ،
وَسَقَيْنَاهَا مِنْ شَرَابِ الْجَنَّةِ، وَبَشَّرْنَاهَا بِوِلَادَةِ خَيْرِ الْأَنْبِيَاءِ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ رَسُولِ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا أُمَّ حَبِيبِ اللَّهِ،
فَهَنِئْنَا لَكِ بِمَا آتَاكِ اللَّهُ مِنْ فَضْلٍ، وَالسَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى
رَسُولِ اللَّهِ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe mtakasifu uliyetakaswa! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu alimteua kwa sharafu ya juu makhsusi! Amani iwe juu yako ewe ambaye toka katika paji lake ilichomoza nuru ya bwana wa Mitume akaangaza kwayo ardhi na mbingu! Amani iwe juu yako ewe ambaye kwa ajili yake walishuka malaika na akawekewa sitara za peponi! Amani iwe juu yako ewe ambaye Hurulaini walishuka kuja kumhudumia, wakamnywesha kinywaji cha Peponi na wakambashiria

mazazi ya mbora wa Manabii! Amani iwe juu yako ewe mama mzazi wa Mtume wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako ewe mama mzazi wa kipenzi wa Mwenyezi Mungu, hongera ziwe juu yako kwa fadhila aliyokupa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako na juu ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake! ”

Ziyara ya Bibi Khadija Mama wa waumini:

السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا أُمَّ الْبُوُّمِنِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا رُوْجَةَ سَيِّدِ
 الْبُرُّسِلِينِ، السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا أُمَّ فَاطِيَّةَ الرَّزَّهَرَاءِ سَيِّدَةَ نِسَاءِ
 الْعَالَمِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا أَوَّلَ الْبُوُّمِنَاتِ، السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا
 مَنْ أَنْفَقْتُ مَا لَهَا فِي نُصْرَةِ سَيِّدِ الْأَنْبِيَاءِ، وَنَصَرَتُهُ
 مَا اسْتَطَاعَتْ وَدَافَعَتْ عَنْهُ الْأَعْدَاءِ، السَّلَامُ عَلَيْكِ يَا مَنْ سَلَّمَ
 عَلَيْهَا جَبْرِيلُ، وَبَلَّغَهَا السَّلَامَ مِنَ اللَّهِ الْجَلِيلِ، فَهَنِئَا لَكِ
 بِأَوْلَاكِ اللَّهُ مِنْ فَضْلِهِ، وَالسَّلَامُ عَلَيْكِ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu yako ewe mama wa waumini! Amani iwe juu yako ewe mke wa bwana wa Mitume! Amani iwe juu yako ewe mama wa Fatima Zahra mbora wa wanawake wote wa ulimwengu! Amani iwe juu yako ewe muumini wa kwanza wa kike! Amani iwe juu yako ambaye alitoa mali yake katika kumsaidia bwana wa Mitume, akamsaidia

kadiri alivyoweza na akamwondolea maadui! Amani iwe juu yako ewe ambaye alisalimiwa na Jibril na akamfikishia salamu kutoka kwa Mwenyezi Mungu Jalili, hongera kwa fadhila alizokuneemesha Mwenyezi Mungu! Na amani iwe juu yako na rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.”

Ziyara ya Ismail na Manabii wengine katika Uzio wa Ismail:

السَّلَامُ عَلَى سَيِّدِنَا إِسْمَاعِيلَ ذَبِيْحَ اللَّهِ ابْنِ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ اللَّهِ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نَبِيَّ اللَّهِ وَابْنَ نَبِيِّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا صَفِيَّ اللَّهِ
وَابْنَ صَفِيِّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ أَنْبَعَ اللَّهُ لَهُ بِئْرَ زَمْرَدِ حِينَ
أَسْكَنَهُ أَبُوهُ بِوادِ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِ اللَّهِ الْبَحْرَمِ، وَاسْتَجَابَ
اللَّهُ فِيهِ دَعْوَةَ أَبِيهِ إِبْرَاهِيمَ حِينَ قَالَ: ”رَبَّنَا إِنِّي أَسْكَنْتُ مِنْ
ذُرِّيَّتِي بِوادِ غَيْرِ ذِي زَرْعٍ عِنْدَ بَيْتِكَ الْبَحْرَمِ رَبَّنَا لِيُقِيمُوا
الصَّلَاةَ فَاجْعَلْ أَفْيَدَةً مِنَ النَّاسِ تَهُوِي إِلَيْهِمْ وَارْتَاقُهُمْ مِنْ
الثَّرَاثِ لَعَلَّهُمْ يَشْكُرُونَ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ سَلَّمَ نَفْسَهُ لِلَّذِبْحِ طَاعَةً لِأَمْرِ اللَّهِ تَعَالَى إِذْ

قالَ لَهُ أَبُوهُ: ”إِنِّي أَرَى فِي الْهَنَامِ أَنِّي أَذْبَحُكَ فَانْظُرْ مَا ذَاتِي
 قالَ يَا أَبَتِ افْعَلْ مَا تُؤْمِنُ رَسَّتْ جَدْنِي إِنْ شَاءَ اللَّهُ مِنَ الصَّابِرِينَ
 ”، فَدَفَعَ اللَّهُ عَنْهُ الرِّبَاحَ وَفَدَاهُ بِذِبْحٍ عَظِيمٍ، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا
 مَنْ أَعَانَ أَبَاكَ عَلَى بِنَاءِ الْكَعْبَةِ كَمَا قَالَ اللَّهُ تَعَالَى: ”وَإِذْ يَرْفَعُ
 إِبْرَاهِيمَ الْقَوَاعِدَ مِنَ الْبَيْتِ فَإِسْعِيلُ رَبَّنَا تَقْبَلْ مِنْ إِنَّكَ أَثْتَ
 السَّبِيعُ الْعَلِيمُ“، أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ مَدَحَهُ اللَّهُ تَعَالَى فِي
 كِتَابِهِ بِقَوْلِهِ: ”وَادْكُرْ فِي الْكِتَابِ إِسْمَاعِيلَ إِنَّهُ كَانَ صَادِقَ
 الْوَعْدِ وَكَانَ رَسُولًا نَّبِيًّا وَكَانَ يَأْمُرُ أَهْلَهُ بِالصَّلَاةِ وَالزَّكَاةِ وَكَانَ
 عِنْدَ رَبِّهِ مَرْضِيًّا

أَللَّامُ عَلَيْكَ يَا مَنْ جَعَلَ اللَّهُ مِنْ ذُرَيْتِهِ مُحَمَّدًا سَيِّدَ
 الْمُرْسَلِينَ وَخَاتَمَ النَّبِيِّينَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، أَللَّامُ عَلَيْكَ
 وَعَلَى أَبِيكَ إِبْرَاهِيمَ خَلِيلِ اللَّهِ، وَعَلَى أَخِيكَ إِسْحَاقَ نَبِيِّ اللَّهِ،
 أَللَّامُ عَلَيْكَ وَعَلَى جَيْبِكِ أَنْبِياءَ اللَّهِ الْمَدْفُونِينَ بِهِذِهِ الْبُنْقَعَةِ

الْبَارَكَةُ الْمُعَظَّمَةُ، السَّلَامُ عَلَيْكَ وَعَلَى أَمْكَانِ الظَّاهِرَةِ الصَّابِرَةِ
 هاجَرَ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، حَشَرَنَا اللَّهُ فِي زُمْرَتِكُمْ تَحْتَ لِوَاعِ
 مُحَمَّدٌ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ، وَلَا جَعَلَهُ اللَّهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ
 زِيَارَتِكُمْ، وَالسَّلَامُ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ

“Amani iwe juu ya Bwana wetu Ismail Dhabihu wa Mwenyezi Mungu mwana wa Ibrahim Khalili! Amani iwe juu yako ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu na mwana wa Nabii Wake! Amani iwe juu yako ewe mteule wa Mwenyezi Mungu na mwana wa mteule Wake! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu alimtolea kisima cha Zamzam pindi baba yake alipomuweka kwenye bonde lisilokuwa na mimea kwenye Nyumba Takatifu ya Mwenyezi Mungu, na hapo Mwenyezi Mungu akajibu dua ya baba yake Ibrahim aliposema: Mimi nimewaweka baadhi ya kizazi changu katika bonde lisilokuwa na mimea, katika Nyumba Yako Takatifu. Mola Wetu Mlezi! Ili wasimamishe Sala, basi ujaalie nyoyo za watu zielekee kwoo na uwaruzuku matunda ili wapate kushukuru!

“Amani iwe juu yako ewe ambaye alisalimisha nafsi yake kwa ajili ya kuchinjwa kwa ajili ya kutii amri ya Mwenyezi Mungu pale baba yake aliposema: “Hakika nimeona katika ndoto kuwa nakuchinja, basi fikiri unaonaje?” Akasema: “Ewe Baba yangu fanya unayoamrishwa, utanikuta inshaallah mionganini mwa wanaosubiri.” Ndipo Mwenyezi Mungu akamwondolea uchinchwaji na akamkomboea kwa dhabihu adhimu! Amani iwe juu yako ewe ambaye

alimsaidia baba yake kujenga Ka'ba kama Mwenyezi Mungu alivyosema: "**Na Ibrahim na Ismail walipoiinua misingi ya Nyumba**, "Ewe Mola Wetu Mlezi! Utukubalie hakika Wewe ndiye Msikivu Mjuzi! Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu amemsifu katika Kitabu Chake kwa kauli Yake: "**Na mtaje katika Kitabu Ismail kwani yeye alikuwa mkweli wa ahadi, na alikuwa Mtume Nabii. Na alikuwa akiwaamrisha watu wake Sala na Zaka na alikuwa maridhawa mbele ya Mola wake Mlezi!**"

"Amani iwe juu yako ewe ambaye Mwenyezi Mungu amefanya Muhammad Bwana wa Mitume na Mwisho wa Manabii (s.a.w.w.) atoke katika kizazi chake! Amani iwe juu yako na juu ya baba yako Ibrahim Khalili wa Mwenyezi Mungu na juu ya kaka yako Is'haqa Nabii wa Mwenyezi Mungu! Amani iwe juu yako na juu ya Manabii wote wa Mwenyezi Mungu waliozikwa katika ardhi hii iliyobarikiwa takatifu! Amani iwe juu yako na juu ya mama yako mtakatifu mwenye subira Hajara, pia rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake ziwe juu yake. Mwenyezi Mungu atukusanye kwenye kundi lenu chini ya bendera ya Muhammad (s.a.w.w.) na wala Mwenyezi Mungu asiifanye kuwa ndio ahadi yetu ya mwisho ya kuwazuru nyinyi. Amani, rehema za Mwenyezi Mungu na Baraka Zake viwe juu yenu."

Kisha Sali hapo rakaa mbili za ziyara na zitowe thawabu zake zawadi kwake, na baada ya rakaa hizo omba dua iliyotangulia kwa ajili ya kila kaburi mionganoni mwa makaburi, kisha omba utakalo.

FASLU YA SABA

MAENEKO MATAKATIFU HUKO MAKKA TUKUFU

Kati ya maeneo hayo ni yale maeneo ambayo yalipata heshima ya kufikiwa na Mtume wetu Mtukufu (s.a.w.w.), kama vile mahali alipozaliwa (s.a.w.w.), makazi yake na katika pango alilokuwa akiishi huko katika Mlima Hiraa, nayo ni sehemu ambayo alikuwa akiitumia kumwabudia Mwenyezi Mungu kabla ya kukabidhiwa unabii, na ndipo ulipoteremkia Wahyi. Pia pango ambalo alijihfadhi (s.a.w.w.) huko katika Mlima wa Thawru, ambalo alitumia kujificha dhidi ya mushrikina pindi alipotoka kuhamia Madina, na maeneo mengine yaliyopata heshima ya kufikiwa naye (s.a.w.w.). utakuja katika maeneo haya na uombe dua, na Sheikh al-Ansariy katika kitabu chake *al-Manasik* ametaja kwamba dua hii isomwe katika Mlima wa Thawru:

Dua isomwayo katika Mlima Thawru:

اللَّهُمَّ بِجَاهِ مُحَمَّدٍ وَأَمِينِهِ وَصِدِّيقِهِ يَسِيرْ أُمُورَنَا، وَاشْرُحْ
صُدُورَنَا، وَنَوِّرْ قُلُوبَنَا، وَاخْتِنْ بِالْخَيْرِ أُمُورَنَا، اللَّهُمَّ إِنَّكَ تَعْلَمُ
سِرَّنَا وَعَلَانِيَتِنَا فَاقْبِلْ مَعْذِرَتِنَا، وَتَعْلَمُ حاجَتِنَا وَتَعْلَمُ مَا فِي
نَفْسِنَا فَاغْفِرْ لِنَا ذُنُوبِنَا، فَإِنَّهُ لَا يَغْفِرُ الذُّنُوبَ إِلَّا أَنْتَ. اللَّهُمَّ إِنِّي
أَوَدَعْتُ فِي هَذَا الْمَحَلِ الشَّيْفِ مِنْ يَوْمِنَا هَذَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ

خالِصاً مُخْلِصاً، أَنِّي أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ، وَأَنَّ مُحَمَّداً عَبْدُهُ

وَرَسُولُهُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kwa heshima ya Muhammad, mndani wake na rafiki yake turahisishie mambo yetu, tukunjulie vifua vyetu, zing’arishe nyoyo zetu na yahitimishe mambo yetu kwa heri. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe waijua siri yangu na dhahiri yangu basi ukubali udhuru wangu, na waijua haja yangu na wayajua yaliyomo ndani ya nafsi yangu basi nighufirie dhambi zangu, kwani hakika haghufirii dhambi ila Wewe. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeliweka amana mahali hapa patukufu kuanzia siku yetu hii mpaka Siku ya Kiyama na hali ni mwenye ikhlasi nisiye na shaka tamko: hakika mimi nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

Dua ya mahali alipozaliwa Mtukufu Mtume:

Napo ni katika uwanja uliyopo karibu na soko la usiku, na kwa hivi sasa pamejengwa maktaba maarufu kwa jina la Maktaba ya Makka Tukufu. Katika ardhi hii iliyobarikiwa iliangaza nuru ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) hivyo kuzaliwa kwake kukawa idhini ya kuzaliwa hatua tukufu ya kuwatoa watu katika giza kwenda kwenye nuru. Na katika nyumba hii nyenyekevu aliishi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) pamoja na mama yake Amina na akawa ndio matumaini yake na mfariji wake. Dua ya mahali hapa ni:

أَللّٰهُمَّ بِجَاهِ نَبِيِّكَ الْمُصَطَّفِي، وَرَسُولِكَ الْبُرْتَضِي، وَأَمِينِكَ عَلَى
 وَحْيِ السَّمَاءِ، طَهَّرْ قُلُوبَنَا مِنْ كُلِّ وَصْفٍ يُبَاعِدُنَا عَنْ
 مُشَاهَدَتِكَ وَمَحَبَّتِكَ، وَأَمْتَنَّا عَلَى مُوَالَةِ أُولِيَّائِكَ، وَمُعَاوَادَةِ
 أَعْدَائِكَ، وَالشَّوْقِ إِلَى لِقَائِكَ، يَا ذَا الْجَلَلِ وَالْأُكْرَامِ。أَللّٰهُمَّ إِنِّي
 أَوْدَعْتُ فِي هَذَا الْمَحَلِ الشَّرِيفِ مِنْ يَوْمِنَا هَذَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ
 خالِصًاً مُخْلِصًاً، أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللّٰهُ، وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ
 وَرَسُولُهُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Kwa heshima ya Nabii Wako mteule na Mtume Wako mridhiwa na mwaminifu juu ya wahyi wa mbinguni, zitakase nyoyo zetu na kila aina ya sifa itakayotutenga mbali na kukushuhudia Wewe na mapenzi Yako. Na tufishe Ewe Mwenyezi Mungu juu ya Sunnah na jamaa kwa kuapenda vipenzi Vyako na kuwa na uadui na maadui Wako na kuwa na shauku ya kukutana Nawe, Ewe Mwenye utukufu na ukarimu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeliweka amana mahali hapa patukufu kuanzia siku yetu hii mpaka Siku ya Kiyama na hali ni mwenye ikhlasi nisiye na shaka na tamko: nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

Na miongoni mwa maeneo hayo matukufu ni mahali ambapo mwezi ulipasuka karibu na mlima wa Abu

Qubaysi. Njoo sehemu hii na usome dua hii:

Dua ya mahali ambapo mwezi ulipasuka:

اللَّهُمَّ صَلِّ عَلَى نَبِيِّ هَذِهِ وَكَبِّرْ وَحْجَ وَاعْتَمِرْ وَانْشِقْ لَهُ الْقَمِرُ وَ
بِدِينِ اللَّهِ أَمْرَبِ الْمَعْرُوفِ وَنَهِيِّ عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ، اللَّهُمَّ إِنِّي
أَوَدَعْتُ فِي هَذَا الْمَحْلِ الشَّيْفِ مِنْ يَوْمِنَا هَذَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ
خَالِصًا مُخْلِصًا أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ مُحَمَّدًا عَبْدُهُ
وَرَسُولُهُ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Nabii aliyetao tahalili, akatoa takbiri, akahiji akafanya Umra na mwezi ukapasuka kwa ajili yake, na kwa dini ya Mwenyezi Mungu akaamrisha mema na akakataza machafu na maovu. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeliweka amana mahali hapa patukufu kuanzia siku yetu hii mpaka Siku ya Kiyama na hali ni mwenye ikhlasi nisiye na shaka tamko: nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

Na mionganini mwa maeneo hayo matukufu ni mlima wa Abu Qubaysi ndani ya Makka, utakuja sehemu hii na usome dua hii:

Dua ya kwenye mlima wa Abu Qubaysi:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ إِيمَانًا كَامِلًا تُبَاشِرُ بِهِ قَلْبُي، وَيَقِينًا صَادِقًا
حَتَّىٰ أَعْلَمَ أَنَّهُ لَنْ يُصِيبَنِي إِلَّا مَا كَتَبَتْ لِي، إِنَّ وَلِيَّ اللَّهُ فِي الدُّنْيَا
وَالآخِرَةِ، اللَّهُمَّ أَوْدَعْتُ فِي هَذَا الْمَحَلِ الشَّافِفِ مِنْ يَوْمِنَا
هَذَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ خَالِصًا مُخْلِصًا أَشْهَدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ
مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba imani kamili ambayo kwayo utaugusa moyo wangu, na yakini ya kweli mpaka njue kwamba hayatonisibu ila uliyoniandikia, hakika mtawala wangu ni Mwenyezi Mungu duniani na Akhera. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeliweka amana mahali hapa patukufu kuanzia siku yetu hii mpaka Siku ya Kiyama na hali ni mwenye ikhlasi nisiye na shaka tamko: nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

Na mionganini mwa maeneo hayo matukufu ni nyumba ya Khadija ambayo alikuwa akiishi Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.), na humo ndimo Khadija alimomzalia Fatima Zahra (a.s.), na ndimo alimofia Khadija (a.s.). Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.) aliendelea kuishi humo mpaka alipohama, na ni mara nyingi Jibril alishukia humo, na eneo hilo lilishuhudia sala, dua na minong’ono ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (s.a.w.w.). Na ni katika

nyumba hii makuraishi walikula njama ya kutaka kumuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu, ndipo Imam Ali (a.s.) akalala kitandani kwake ili kuitoa damu yake katika njia ya Mwenyezi Mungu. Utaomba dua hii katika nyumba hii:

Dua ya nyumbani kwa Bibi Khadija (a.s.):

اللَّهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِالْبَصْرَةِ الرَّهْرَاءِ وَأَوْلَادِهَا الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ
عَلَيْهِمَا السَّلَامُ يَسِّرْ أَمْرَنَا وَأَشْرِحْ صَدُورَنَا وَاخْتِمْ
بِالصَّالِحَاتِ أَعْمَانَا أَوْ دَعْتُ فِي هَذَا الْمَحَلِ الشَّرِيفِ مِنْ يَوْمِنَا
هَذَا إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ خَالِصًا مُخْلِصًا أَشْهُدُ أَنْ لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَأَنَّ
مُحَمَّدًا عَبْدُهُ وَرَسُولُهُ.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nakuomba kupitia kipande cha nyama ya Mtume Zahrau na kupitia watoto wake Hasan na Husain (a.s.) urahisishe mambo yetu, ukunjue vifua vyetu na uhitimishe amali zetu kwa matendo mema. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeliweka amana mahali hapa patukufu kuanzia siku yetu hii mpaka Siku ya Kiyama tamko nashahidilia kwamba hakuna mungu ila Allah na kwamba hakika Muhammad ni mja Wake na Mtume Wake.”

Kuiaga Ka’ba Tukufu:

Mambo yaliyo mustahabu katika kuiaga Makka Tukufu na Ka’ba Tukufu ni mengi, nasi hapa tutataja baadhi tu, nayo

ni:

1. Alhaji atakapotaka kutoka kwenda kwa watu wake asitoke mpaka awe amenunua tende kwa dirhamu na kuzitoa sadaka kwa mafukara, hiyo inakuwa ni kafara ya zile dosari ndogondogo zilizopatikana katika Hijja yake.
2. Ni mustahabu kuazimia kurudi tena na kumuomba Mwenyezi Mungu amrudishe tena Makka, hiyo ni kutokana na riwaya iliyopokewa kwamba kitendo hicho humuongeza umri inshaallah. Bali ni makuruhu kuacha kufanya hivyo kwa mujibu wa kauli ya Abu Abdillah (a.s.) aliyosema: “Atakayetoka Makka na hali hataki kurudi tena basi muda wa kifo chake umekaribia na adhabu yake imesogea.” Na katika Hadithi nyingine: Hakika Yazid bin Muawiya alihiji na alipotoka Makka alisema: “Tukiweka Thafila kulia hatutarudi tena miaka ijayo kwa ajili ya Hijja na Umra muda wote tutakaobakia hai.” Ndipo Mwenyezi Mungu akapunguza umri wake na kumfisha kabla ya muda wake wa mwanzo.
3. Kuitufu Ka’ba mzunguko saba.
4. Kuligusa Jiwe Jeusi na Nguzo ya Yemen katika kila mzunguko kama ataweba, la sivyo ataanzia mzunguko wake hapo na atamalizia hapo kama ataweba.
5. Ataleta Sunnah zilizotangulia katika hali ya kutufu na zile za eneo la al-Mustajaru kama ataweba.
6. Amuhimidi na kumtukuza Mwenyezi Mungu na kumsalia Mtume Muhammad (s.a.w.w.) na kuomba

ayatakayo. Kisha aseme:

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ عَبْدِكَ وَرَسُولِكَ، وَنَبِيِّكَ وَأَمِينِكَ،
وَحَبِيبِكَ وَنَجِيِّكَ، وَخَيْرِتِكَ مِنْ خَلْقِكَ. اللّٰهُمَّ كَمَا بَلَغَ
رِسَالَتِكَ، وَجَاهَدَ فِي سَبِيلِكَ، وَصَدَعَ بِأَمْرِكَ، وَأَوْذِيَ فِي
جَنِيِّكَ حَتّٰى أَتَاهُ الْيَقِينُ. اللّٰهُمَّ اقْلِبْنِي مُفْلِحًا مُنْجِحًا
مُسْتَجَابًا لِي، بِأَفْضَلِ مَا يُرِجِّعُهُ أَحَدٌ مِنْ وَفْدِكَ مِنَ الْمُغْفَرَةِ
وَالْبَرَكَةِ وَالرِّضْوَانِ وَالْعَافِيَةِ، مِمَّا يَسْعُنِي أَنْ أَطْلُبَ أَنْ
تُعْطِيَنِي مِثْلَ الَّذِي أَعْطَيْتَهُ أَفْضَلَ مَنْ عَبَدَكَ، وَتَزِيدْنِي عَلَيْهِ
اللّٰهُمَّ إِنْ أَمْتَنِي فَاغْفِرْ لِي وَإِنْ أُحِيَّتِنِي فَارْزُقْنِي مِنْ قَابِلٍ.
اللّٰهُمَّ لَا تَجْعَلْهُ آخِرَ الْعَهْدِ مِنْ بَيْتِكَ.

اللّٰهُمَّ إِنِّي عَبْدُكَ وَابْنُ عَبْدِكَ وَابْنُ أَمَّتِكَ، حَلْتُنِي عَلَى
دَابِّتِكَ، وَسَيَرَتْنِي فِي بِلَادِكَ، حَتّٰى أَدْخُلَنِي حَرَمَكَ وَأَمْنَكَ،
وَقُدْ كَانَ فِي حُسْنِ ظَنِّي بِكَ أَنْ تَغْفِرِ لِي ذُنُوبِي، فَإِنْ كُنْتَ قَدْ

غَفَرَتِ لِي ذُنُوبِي فَأَزْدَدُ عَنِّي رِضَى، وَقَرِبَنِي إِلَيْكَ زُلْفَى، وَلَا
 تُبَاعِدُنِي، وَإِنْ كُنْتَ لَمْ تَغْفِرْ لِي فَهِنَ الْآنَ فَاغْفِرْ لِي قَبْلَ أَنْ تَنْأِى
 عَنْ بَيْتِكَ دَارِى، وَهَذَا أَوَانُ انْصِرافِى، إِنْ كُنْتَ أَذِنْتَ لِي غَيْرَ
 رَاغِبٍ عَنْكَ وَلَا عَنْ بَيْتِكَ، وَلَا مُسْتَبْدِلٌ بِكَ وَلَا بِهِ. أَللَّهُمَّ
 اخْفَظْنِي مِنْ بَيْنِ يَدَيْكَ وَمِنْ خَلْفِي وَعَنْ يَمِينِي وَعَنْ شِمَائِى، حَتَّى
 تُبَلِّغَنِي أَهْلِى، وَأُكِفِنِي مَؤْوِنَةً عِبَادِكَ وَعِيالِى، فَإِنَّكَ وَلِي ذِلِّكَ
 مِنْ خَلْقِكَ وَمِنْ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad mja Wako, Mtume Wako, Nabii Wako, Mwaminifu Wako, Hababi Wako, Mwokozi Wako na aliye mbora kati ya viumbe Wako. Ewe Mwenyezi Mungu! Kama alivyofikisha ujumbe Wako, akapigana jihadi katika njia Yako, akatangaza amri Yako na akaudhiwa katika jambo Lako na pembezoni Mwako mpaka yakini (kifo) ilipomfika, ewe Mwenyezi Mungu nirudishe hali ni mwenye kufaulu mwenye kufanikiwa na mwenye kujibiwa kwa kupewa lile lililo bora kushinda atakalorudi nalo yejote toka katika ugeni Wako mionganoni mwa maghfira, Baraka, ridhaa na afya. Katika yale ambayo naweza kuomba ni unipe mfano wa lile ulilompa mbora kushinda wote waliokuabudu na unizidishie kuliko yeye. Ewe Mwenyezi Mungu! Nighufirie na kama utaendelea kuniacha hai niruzuku (Hijja) tena mwaka ujao. Ewe Mwenyezi Mungu!

Usiifanye kuwa ahadi ya mwisho ya kufika katika Nyumba Yako.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi ni mja Wako, mwana wa mja Wako wa kiume na mwana wa mja Wako wa kike, ulinibeba juu ya mnyama Wako na ukanipitisha katika mji Wako mpaka ukaniingiza Eneo Lako Takatifu (Haram) na amani Yako, na ilikuwa katika dhana yangu nzuri Kwako ni unighufirie dhambi zangu, basi ikiwa umeshanighufiria nizidishie ridhaa na nisogeze karibu mno Nawe na wala usinitenge mbali. Na ukiwa hujanighufiria basi tokea sasa nighufirie kabla nyumba yangu haijawa mbali na Nyumba Yako, huu ndio wakati wa kuondoka kwangu ikiwa umeshanipa idhini, na hali si mwenye kujitenga Nawe wala na Nyumba Yako, na wala si mwenye kukufanya mbadala Wewe wala yenye. Ewe Mwenyezi Mungu! Nihifadhi mbele, nyuma, kuliani na kushotoni mpaka unifikishe kwenye familia yangu, na ukinifikisha kwenye familia yangu nitosheleze matumizi ya waja Wako na familia yangu, kwani hakika Wewe ni msimamizi wa hayo kushinda viumbe Wako na kuliko mimi.”

7. Kisha aje kwenye Zamzam anywe na wala asimwagie kichwani, na aseme:

أَعْبُونَ تَاعِبُونَ عَابِدُونَ لِرَبِّنَا حَامِدُونَ، إِلَى رَبِّنَا رَاغِبُونَ، إِلَى اللَّهِ

رَاجِعُونَ إِنْ شَاءَ اللَّهُ

“Wenyekurejea, wenyekutubu na wenyekuabudu, wenyekumhimidi Mola Wetu Mlezi, wenyekugeuka kwa Mola wetu Mlezi, wenyekurejea kwa Mola wetu Mlezi inshaallah.”

8. Kisha aje Maqam Ibrahim na asali rakaa mbili nyuma yake.
9. Kisha aje kwenye mlango wa Nyumba na aweke mkono juu yake na aseme:

المسكين على بابك فتصدق عليه بالجنة

“Maskini yupo mlangoni Kwako basi mpe sadaka ya Pepo.”

10. Kisha asujudu sijda ndefu kwenye mlango wa Msikiti, kisha asimame kwa nyayo zake hali kaelekea Kibla Tukufu na aseme:

اللَّهُمَّ إِنِّي أَنْقَلَبُ عَلَى لِإِلَهٍ إِلَّا اللَّهُ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi narudi kwa mujibu wa hapana mungu ila Allah.”

11. Kisha atokee mlango wa al-Hanatiin.

Ni mustahabu kuhitimishia ziara huko Madina:

Ni mustahabu kwa alhaji kumzuru Nabii (s.a.w.w.) na ni Sunnah iliyotiliwa mkazo kutokana na kauli ya Mtume (s.a.w.w.) kwa Ali: “Ewe Ali! Atakayenizuru wakati wa uhai wangu au baada ya kufa kwangu au akakuzuru wewe wakati wa uhai wako au baada ya kifo chako, au akawazuru wanao wakati wa uhai wao au baada ya kifo chao, nimechukua dhamana ya kumuokoa Siku ya Kiyama dhidi ya misukosuko yake na shida zake mpaka nimfanye

awe pamoa nami katika daraja langu.” Na akasema tena: “Atakayenizuru au kumzuru mmoja kati ya kizazi changu nitamzuru Siku ya Kiyama na kumuokoa na misukosuko yake.” Na kwa mujibu wa hadithi hii ni mustahabu pia kuwazuru wasiokuwa maasumu toka katika kizazi chake (s.a.w.w.). Na kutokana na baadhi ya habari tunapata kwamba ni mustahabu kumalizia ziara huko Madina kama ilivyo katika riwaya ya Ghiyabu kutoka kwa Abu Ja’far (a.s.): Nianzie Madina au Makka? Akasema: Naanzia Makka na ninamalizia Madina, na ndio bora. Kama ambavyo kutokana na baadhi ya riwaya tunapata kwamba ni mustahabu kuanza kumzuru (s.a.w.w.) na kuitanguliza ziara yake kabla ya kuja Makka Tukufu. Ndio, lau ikiwa ni kati ya kuja Makka kwa ajili ya Hijra ya Sunnah bila ya kuja Madina au kinyume, basi kinyume ni bora kutokana na maandiko yaliyopokewa katika mlango huu.

Fadhila za kuzikwa katika moja ya Maeneo mawili Matakatifu (Haramaini):

Atakayefia katika moja ya Maeneo mawili Matakatifu (Haramaini), Eneo Takatifu la Makka au Eneo Takatifu la Madina, atakuwa mionganini mwa wenyewe amali Siku ya Kiyama, hiyo ni kutokana na kauli ya Mwenyezi Mungu: “Atakayeingia atakuwa amesalimika,” na kauli ya (s.a.w.w.); “Atakayefia katika moja ya Maeneo mawili Matakatifu (Haramaini), Eneo Takatifu la Mwenyezi Mungu na Eneo Takatifu la Mtume Wake (s.a.w.w.), Mwenyezi Mungu atamfufua mionganini mwa waliosalimika. Na katika baadhi ya riwaya: Hatohisabiwa Siku ya Kiyama. Na atakayefia katika Eneo Takatifu la Makka atasalimika na mshindo mkubwa, kuanzia aliye mwema hadi yule aliyemuovu wao, kama ilivyo katika riwaya ya Harun, alisema: “Nilimsikia Abu Abdillah (a.s.)

مِنْ ذُنُوبِهِ كُلِّهَا فَغَفِرْتَهَا لَهُ يَا ذَالْجَلَلِ وَالْأَكْرَامِ، أَللَّهُمَّ وَنَقِنَا
وَسَدِّدْنَا وَاقْبِلْ تَضَّعْ عَنَا، يَا خَيْرَ مَنْ سُيِّلَ، وَيَا أَرْحَمَ مَنِ
اسْتَرْحَمَ، يَا مَنْ لَا يَخْفِي عَلَيْهِ إِغْبَاضُ الْجُفُونِ، وَلَا لَحْظَ
الْعَيْوَنِ، وَلَا مَا اسْتَقَرَّ فِي الْبَكْنُونِ، وَلَا مَا انْطَوَتْ عَلَيْهِ مُضَرَّاتُ
الْقُلُوبِ، أَلَا كُلُّ ذِلِّكَ قَدْ أَحْصَاهُ عِلْمُكَ، وَأَوْسَعُهُ حِلْمُكَ،

سُبْحَانَكَ وَتَعَالَى إِيَّاكَ يَقُولُ الظَّالِمُونَ عُلُوًّا كَبِيرًا، تُسَبِّحُ لَكَ
السَّيَّاَوَاتُ السَّبْعُ، وَالْأَرْضُونَ وَمَنْ فِيهِنَّ، وَإِنْ مَنْ شَئْ عِلَّا
يُسَبِّحُ بِحَمْدِكَ، فَلَكَ الْحَمْدُ وَالْمَجْدُ، وَعُلُوُّ الْجِدْدِ، يَا
ذَالْجَلَلِ وَالْأَكْرَامِ، وَالْفَضْلِ وَالْأَنْعَامِ، وَالْأَيْادِي الْجِسَامِ،
وَأَنْتَ الْجَوَادُ الْكَرِيمُ، الرَّءُوفُ الرَّحِيمُ، أَللَّهُمَّ أَوْسِعْ عَلَيَّ مِنْ
رُّحْرِيقَ الْحَلَالِ، وَعَافِنِي فِي بَدَنِ وَدِينِي، وَآمِنْ خَوْفَ، وَاعْتِقُ
رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ، أَللَّهُمَّ لَا تَشْكُرْ بِي، وَلَا تَسْتَدْرِجْنِي، وَلَا
تَخْدَعْنِي، وَادْرِأْ عَنِّي شَرَّ فَسَقَةِ الْجِنِّ وَالْأَنْسِ يَا أَمْسِعْ

السّامِعِينَ، يَا أَبْصَرَ النَّاظِرِينَ، وَيَا أَسْرَعَ الْحَاسِبِينَ، وَيَا أَرْحَمَ
 الرَّاحِمِينَ، صَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ السَّادَةِ الْمُيَامِينَ،
 وَأَسْأَلُكَ اللَّهُمَّ حاجِتِي أَلَّقِ إِنْ أَعْطَيْتَنِي لَمْ يَضْرَنِي مَا
 مَنْعَتْنِي، وَإِنْ مَنَعْتَنِي لَمْ يَنْفَعْنِي مَا أَعْطَيْتَنِي، أَسْأَلُكَ فَكَاكَ
 رَقْبَتِي مِنَ النَّارِ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، وَحْدَكَ لَا شَيْءَ يَكُونُ لَكَ، لَكَ
 الْبُدْلُكُ، وَلَكَ الْحَمْدُ، وَأَنْتَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ عَقَدِيرٌ،

يَا رَبُّ يَا رَبُّ بِإِلَهِي أَنَا الْفَقِيرُ فِي غِنَائِي فَكَيْفَ لَا أَكُونُ قَفِيرًا فِي
 فَقْرِي، إِلَهِي أَنَا الْجَاهِلُ فِي عِلْمِي فَكَيْفَ لَا أَكُونُ جَهُولًا فِي
 جَهْلِي، إِلَهِي إِنَّ اخْتِلَافَ تَدْبِيرِكَ، وَسُرْعَةَ طَوَّاعِي مَقَادِيرِكَ،
 مَنَعَا عِبَادَكَ الْعَارِفِينَ بِكَ عَنِ السُّكُونِ إِلَى عَطَاءِ، وَالْيَأسِ
 مِنْكَ فِي بَلَاءِ، إِلَهِي مِنْيٌّ مَا يَلِيقُ بِلُؤْمِي وَمِنْكَ مَا يَلِيقُ
 بِكَرِيمِكَ، إِلَهِي وَصَفْتَ نَفْسَكَ بِاللُّطْفِ وَالرَّأْفَةِ لِي قَبْلَ وُجُودِ
 ضَعْفِي، أَفَتَبَيِّنُنِي مِنْهُمَا بَعْدَ وُجُودِ ضَعْفِي، إِلَهِي إِنْ ظَهَرَتِ

الْمَحَاسِنُ مِنِّي فِيْفَضِيلَكَ، وَلَكَ الْبِلَةُ عَلَىَّ، وَإِنْ ظَهَرْتِ
 الْمُسَاوِيُّ مِنِّي فَبِعَدْلِكَ، وَلَكَ الْحُجَّةُ عَلَىَّ إِلَهِ كَيْفَ تَكْلُنِي
 وَقَدْ تَكَفَّلْتَ لِي، وَكَيْفَ أُضَامُ وَأَنْتَ النَّاصِرُ لِي، أَمْ كَيْفَ أَخِيبُ
 وَأَنْتَ الْحَفِيْعُ بِي، هَا آنَا أَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ بِفَقْرِي إِلَيْكَ، وَكَيْفَ
 أَتَوَسَّلُ إِلَيْكَ بِسَاهُومَاحاً أَنْ يَصِلَّ إِلَيْكَ، أَمْ كَيْفَ أَشْكُو إِلَيْكَ
 حَالِي وَهُوَ لَا يَخْفِي عَلَيْكَ، أَمْ كَيْفَ أُتَرْجِمُ بِسَقَالِي وَهُوَ مِنْكَ بَرِّ
 إِلَيْكَ، أَمْ كَيْفَ تُخَيِّبُ آمَالِي وَهُنَّ قَدْ وَفَدَتُ إِلَيْكَ، أَمْ كَيْفَ لَا
 تُحْسِنُ أَحْوَالِي وَبِكَقَامَتْ،

إِلَهِي مَا الْطَّفَكَ بِمَعَ عَظِيمِ جَهْلِي، وَمَا أَرْحَمَكَ بِمَعَ قَبِيحِ
 فِعْلِي، إِلَهِي مَا أَقْرَبَكَ مِنِّي وَأَبْعَدَنَ عَنْكَ، وَمَا أَرْأَفَكَ بِفَهْما
 الَّذِي يَحْجُبُنِي عَنْكَ، إِلَهِي عَلِمْتُ بِاِختِلَافِ الاُثَارِ، وَتَنَقْلَاتِ
 الْأَطْوَارِ، أَنَّ مُرَادَكَ مِنِّي أَنْ تَتَعَرَّفَ إِلَيَّ فِي كُلِّ شَيْءٍ، حَتَّى لَا
 أَجْهَدَكَ فِي شَيْءٍ، إِلَهِي كُلُّمَا أَخْرَسَنِي لُؤْمِي أَنْجَقَنِي كَمُكَ، وَكُلُّمَا

آيَسْتُنِي أَوْ صَافِي أَطْبَعْتُنِي مِنْتُكَ، إِلَهِي مَنْ كَانَتْ مَحَاسِنُهُ
 مَسَاوِيَ، فَكَيْفَ لَا تَكُونُ مُسَاوِيَهِ مَسَاوِيَ، وَمَنْ كَانَتْ
 حَقَائِقُهُ دَعَاوِيَ، فَكَيْفَ لَا تَكُونُ دَعَاوِيَهِ دَعَاوِيَ، إِلَهِي حُكْمُكَ
 النَّافِذُ، وَمَشِيقَتُكَ الْقَاهِرَةُ لَمْ يَتَرَكَ الِذِي مَقَالَ مَقَالًاً، وَلَا لِذِي
 حَالٍ حَالًاً، إِلَهِي كُمْ مِنْ طَاعَةٍ بَنَيْتُهَا، وَحَالَةٌ شَيَّدْتُهَا، هَدَمَ
 إِعْتِيادِي عَلَيْهَا عَدْلُكَ، بَلْ أَفَالَنِي مِنْهَا فَضْلُكَ، إِلَهِي إِنَّكَ
 تَعْلَمُ أَنِّي وَإِنْ لَمْ تَدْمِرِ الطَّاعَةَ مِنِّي فِعْلًا جَزْمًا قَدْ دَامَتْ مَحَبَّةً
 وَعَزِيمًاً، إِلَهِي كَيْفَ أَعْزِمُ وَأَنْتَ الْقَاهِرُ، وَكَيْفَ لَا أَعْزِمُ وَأَنْتَ
 الْأَمْرُ، إِلَهِي تَرَدُّدِي فِي الْأُثَارِ يُوجِبُ بُعْدَ الْبَيْزَارِ، فَاجْعَنِي
 عَلَيْكَ بِخِدْمَةٍ تُوَصِّلُنِي إِلَيْكَ،

كَيْفَ يُسْتَدَالُ عَلَيْكَ بِهَا هُوَ فِي وُجُودِهِ مُفْتَقِرٌ إِلَيْكَ، أَيْكُونُ
 لِغَيْرِكَ مِنَ الظُّهُورِ مَا يُؤْسِنُكَ، حَتَّى يَكُونَ هُوَ الْمُظْهَرُ لَكَ، مَتَى
 غَبَّتْ حَتَّى تَحْتَاجَ إِلَى دَلِيلٍ يَدْلِلُ عَلَيْكَ، وَمَتَى بَعْدَتْ حَتَّى

تَكُونَ الْأُثَارُ هِيَ الَّتِي تُوَصِّلُ إِلَيْكَ، عَيْنٌ لَا تَرَاكَ عَلَيْهَا
 رَقِيبًا، وَخَسِئَتْ صَفْقَةٌ عَبْدُ لَمْ تَجْعَلْ لَهُ مِنْ حُبْكَ نَصِيبًا،
 إِلَهِي أَمْرَتِ بِالرُّجُوعِ إِلَى الْأُثَارِ فَأَرْجِعْنِي إِلَيْكَ بِكِسْوَةِ الْأَنْوَارِ،
 وَهِدَايَةِ الْأُسْتِبْصَارِ، حَتَّى أَرْجِعَ إِلَيْكَ مِنْهَا كَمَا دَخَلْتُ إِلَيْكَ
 مِنْهَا، مَصْوَنَ السِّرِّ عَنِ النَّظَرِ إِلَيْهَا، وَمَرْفُوعَ الْهِئَةِ عَنِ الْأُعْتِيَادِ
 عَلَيْهَا، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، إِلَهِي هَذَا ذُلِّ ظَاهِرٌ بَيْنَ يَدَيْكَ،
 وَهَذَا حَالٌ لَا يَخْفِي عَلَيْكَ، مِنْكَ أَطْلُبُ الْوُصُولُ إِلَيْكَ، وَبِكَ
 أَسْتَدِلُّ عَلَيْكَ، فَاهْدِنِي بِنُورِكَ إِلَيْكَ، وَأَقِنْنِي بِصِدْقِ
 الْعُبُودِيَّةِ بَيْنَ يَدَيْكَ، إِلَهِي عَلِّينِي مِنْ عَلِيْكَ الْمَخْزُونِ،
 وَصُنْقِ بِسِترِكَ الْبَصُونِ، إِلَهِي حَقِّقْنِي بِحَقَائِقِ أَهْلِ الْقُربَى،
 وَاسْلُكْ بِمَسْلَكَ أَهْلِ الْجَذْبِ،

إِلَهِي أَغْنِنِي بِتَدْبِيرِكَ لِي عَنْ تَدْبِيرِي، وَبِاُخْتِيَارِكَ عَنِ
 اخْتِيَارِي، وَأَوْقِنْنِي عَلَى مَرَاكِنِ اضْطِرَابِي، إِلَهِي أَخْرِجْنِي مِنْ

ذُلِّ نَفْسِي، وَطَهْرُنِي مِنْ شَكْيٍ وَشَهْرَنِي قَبْلَ حُلُولِ رَمْسِي، بِكَ
أَتُتَصِّمُ فَانْصَمْنِي، وَعَلَيْكَ أَتَوَكَّلُ فَلَا تَكْنُنِي، وَإِيَّاكَ أَسْأَلُ فَلَا
تُخِيبَنِي، وَفِي فَضْلِكَ أَرْغَبُ فَلَا تَحْرِمْنِي، وَبِجَنَابِكَ أَتُسْبِّبُ فَلَا
تُبْعِدْنِي، وَبِبَابِكَ أَقِفُ فَلَا تَطْرُدْنِي، إِلَهِي تَقَدَّسْ رِضاكَ أَنْ
يَكُونَ لَهُ عِلَّةٌ مِنْكَ، فَكَيْفَ يَكُونُ لَهُ عِلَّةٌ مِنْيَ، إِلَهِي أَنْتَ الْغِنْيُ
بِذاتِكَ أَنْ يَصِلَ إِلَيْكَ الْفَقْعُ مِنْكَ، فَكَيْفَ لَا تَكُونُ غَنِيًّا عَنِّي،
إِلَهِي إِنَّ الْقَضَاءَ وَالْقَدَارَ يُيَثِّنِينِي، وَإِنَّ الْهُوَى بِوَثَائِقِ الشَّهْوَةِ
أَسْهَنِي، فَكُنْ أَنْتَ النَّصِيرَ لِي، حَتَّى تَنْصَهَنِي وَتُبْصِّرَنِي، وَأَغْنِنِي
بِفَضْلِكَ حَتَّى أَسْتَغْنِي بِكَ عَنْ طَلَبِي، أَنْتَ الَّذِي أَشْرَقْتَ
الْأَنُوارَ فِي قُلُوبِ أَوْلِيَائِكَ حَتَّى عَرَفُوكَ وَوَحَدَوكَ، وَأَنْتَ الَّذِي
أَزَلْتَ الْأَغْيَارَ عَنْ قُلُوبِ أَحِبَّائِكَ حَتَّى لَمْ يُحِبُّوا سِوالَكَ، وَلَمْ
يَلْجَأُوا إِلَى غَيْرِكَ، أَنْتَ الْبُونُسُ لَهُمْ حَيْثُ أَوْحَشَتُهُمُ الْعَوَالِمُ،
وَأَنْتَ الَّذِي هَدَيْتُهُمْ حَيْثُ اسْتَبَانَتْ لَهُمُ الْبَعَالِمُ، مَاذَا وَجَدَ

مَنْ فَقَدَكَ، وَمَا الَّذِي فَقَدَ مَنْ وَجَدَكَ، لَقَدْ خَابَ مَنْ رَضِيَ
دُونَكَ بَدَلًا، وَلَقَدْ خَسَرَ مَنْ بَغَى عَنْكَ مُتَحَوِّلًا، كَيْفَ يُرْجِي
سِواكَ وَأَنْتَ مَا قَطَعْتَ الْإِحْسَانَ، وَكَيْفَ يُطَلِّبُ مِنْ غَيْرِكَ وَأَنْتَ
مَا بَدَلْتَ عادَةَ الْإِمْتِنَانِ، يَا مَنْ أَذَاقَ أَحِبَّاءَهُ حَلَوةَ
الْبُؤَانَسَةِ، فَقَامُوا بَيْنَ يَدَيْهِ مُتَنَلِّقِينَ، وَيَا مَنْ أَلْبَسَ أُولِيَاءَهُ
مَلَابِسَ هَيْبَتِهِ، فَقَامُوا بَيْنَ يَدَيْهِ مُسْتَغْفِرِينَ، أَنْتَ الَّذِي كُرِمَ
قَبْلَ الَّذِي كِرِينَ، وَأَنْتَ الْبَادِي بِالْإِحْسَانِ قَبْلَ تَوْجِهِ
الْعَابِدِينَ، وَأَنْتَ الْجَوَادُ بِالْعَطَاءِ قَبْلَ طَلَبِ الطَّالِبِينَ، وَأَنْتَ
الْوَهَابُ ثُمَّ لِيَا وَهَبْتَ لَنَا مِنَ الْمُسْتَقْرِضِينَ، إِلَهِ أُطْلُبُنِي
بِرَحْمَتِكَ حَتَّى أَصِلَّ إِلَيْكَ، وَاجْزِنْ بْنِي بِبِنْتِكَ حَتَّى أُقْبِلَ عَلَيْكَ،
إِلَهِ إِنَّ رَجَائِي لَا يَنْقِطُ عَنْكَ وَإِنْ عَصَيْتُكَ، كَمَا أَنَّ خَوفِي لَا
يُزَايِلُنِي وَإِنْ أَطَعْتُكَ، فَقَدْ دَفَعْتَنِي الْعَوَالِمُ إِلَيْكَ، وَقَدْ أُوقَعْتُنِي
عِلْمِي بِكَرِمِكَ عَلَيْكَ، إِلَهِ كَيْفَ أَخِيبُ وَأَنْتَ أَمَلِي، أَمْ كَيْفَ

أهانْ وَعَلَيْكَ مُتَّكِّلٌ،

إِلَهِي كَيْفَ أَسْتَعِرُونِي الْذِلَّةَ أَرْكَنْتَنِي، أَمْ كَيْفَ لَا أَسْتَعِرُونِي إِلَيْكَ
نَسْبَتَنِي، إِلَهِي كَيْفَ لَا أَفْتَقِرُ وَأَنْتَ الَّذِي فِي الْفُقْرِ آءِ أَفْتَنَتِي،
أَمْ كَيْفَ أَفْتَقِرُ وَأَنْتَ الَّذِي بِجُودِكَ أَغْنَيْتَنِي، وَأَنْتَ الَّذِي لَا إِلَهَ
غَيْرُكَ تَعْرَفَتْ لِكُلِّ شَيْءٍ فِيمَا جَهَلْتَ شَيْءً، وَأَنْتَ الَّذِي تَعْرَفْتَ
إِلَيْهِ فِي كُلِّ شَيْءٍ، فَرَأَيْتُكَ ظَاهِرًا فِي كُلِّ شَيْءٍ، وَأَنْتَ الظَّاهِرُ لِكُلِّ
شَيْءٍ، يَا مَنِ اسْتَوَى بِرَحْمَانِيَّتِهِ فَصَارَ الْعَرْشَ غَيْبًا فِي ذَاتِهِ،
مَحْقُوتَ الْأُثَارِ بِالْأُثَارِ، وَمَحْوَتَ الْأَغْيَارِ بِمُحِيطَاتِ أَفْلَاكِ
الْأَنُوارِ، يَا مَنِ احْتَجَبَ فِي سُرَادِقَاتِ عَرْشِهِ عَنْ أَنْ تُدْرِكَهُ
الْأَبْصَارُ، يَا مَنْ تَجَلَّ بِكَيْالِ بَهَائِهِ، فَتَحَقَّقْتُ عَظَمَتُهُ مَنْ
الْأُسْتِوَاءِ، كَيْفَ تَخْفِي وَأَنْتَ الظَّاهِرُ، أَمْ كَيْفَ تَغْيِبُ وَأَنْتَ
الرَّقِيبُ الْحَاضِرُ، إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَحْدَهُ.

“Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu Ambaye hukumu Yake haina muondoaji wala upaji wake hauna kizuizi na

wala sanaa Yake si kama sanaa za msanii, na Yeye ndiye Mkarimu Mwingi wa ukarimu. Aliumba jinsia za kuvutia, na kwa hekima Yake akaumba viumbe kwa ufanisi, havifichiki Kwake vichomozavyo na wala hazipotei Kwake amana. Ni mwenye kumlipa kila mtengenezaji na ni mwenye kumtosheleza kila aliyekinai, na ni mwenye kumrehemu kila mwenye kujinyenyeka, na ni mwenye kuteremsha manufaa na Kitabu kilichokusanya yote kwa nuru yene kung'aa. Naye ni mwenye kusikia dua na mwenye kuondoa matatizo, mwenye kunyanyua daraja na mwenye kuwango'oa majabari. Hivyo hakuna mungu asiyekuwa Yeye na wala hakuna kina kinacholingana Naye na wala hafanani na kitu chochote, Naye ni Msikivu Mwenye kuona, Mpole Mwenye habari, na ni Muweza wa kila kitu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi natamani kuja Kwako na nashahidilia Umola Wako hali ni mwenye kukiri kwamba hakika Wewe ni Mola Wangu Mlezi, na kwamba marudio yangu ni Kwako. Ulinianza kwa neema Yako kabla sijakuwa kitu chenye kutajwa, ukaniumba kutokana na udongo kisha uknipa makazi katika mifupa ya migongo, na ni mwenye kuamini hali ya kupatwa na mauti na kupishana kwa dahari na miaka, niliendelea kuhamza toka mfupa wa mgongo mpaka kwenye mfuko wa kizazi kadiri zilivyokuja siku zilizopita na karne zilizokwisha. Kwa huruma Yako kwangu, fadhila Yako kwangu na ihsani Yako kwangu hukunitoa katika dola ya viongozi wa ukafiri ambao walitengua ahadi Yako na wakawakadhibisha Mitume Wako. Lakini Wewe kwa huruma Yako na upendo Wako kwangu ulinitoa kwa ajili ya uongofu ulionitangulia, ambao umenirahisisha kwa ajili yake na humo umeniumba, na kabla ya hapo ulinihurumia kwa matendo Yako mazuri na wasaa wa neema Zako,

hivyo ukalianza umbile langu kwa tone la manii lililotonwa, na ukaniipa makazi katika giza tatu baina ya nyama, damu na ngozi, hukunishuhudilisha uumbwaji wangu na wala hujaweka kwangu chochote kutokana na amri yangu.

“Kisha ukanitoa duniani kwa ajili ya uongofu ulionitangulia na hali ni kamili niliye sawasawa, na ukanihifadhi katika mbeleko nami mtoto mdogo, ukaniruzuku chakula maziwa matamu, ukazipa huruma juu yangu nyoyo za walezi, na ukanilea kwa akina mama wenye huruma, ukaniepusha mabalaa ya majini na ukantisalimisha na ziada na upungufu, hivyo umetakasika Ewe Mwenye kurehemu Mwingi wa rehema, mpaka nilipoinua sauti hali ni mwenye kutamka maneno ulinitimizia wasaa wa neema, ukanilea hali ni mwenye kuongezeka katika kila mwaka mpaka umbile langu lilipokamilika na ukawa sawa uwezo wangu ndipo ukawajibisha hoja Yako juu yangu kwa kunipa ilhamu ya kukutambua. Ukanishtua kwa maajabu ya hekima Yako na ukaniamsha kwa yale uliyoweka katika mbingu Yako na ardhi Yako mionganoni mwa uumbaji Wako wa ajabu, ukanzindua kukushukuru Wewe na kukutaja Wewe na ukawajibisha juu yangu kukutii Wewe na kukuabudu Wewe. Ukanifahamisha yale waliyokuja nayo Mitume Wako na ukadirahisishia kukubali maridhawa Yako, na ukanineemeshya katika yote hayo kwa msaada Wako na huruma Yako.

“Kisha uliponiumba kwa udongo bora hukuridhia kunipa neema hii bila ile, na ukaniruzuku aina za maisha na aina za mavazi kwa upaji Wako mkubwa uliotukuka ulio juu yangu na ihsani Zako za tangu zilizo kwangu, hata uliponitimizia neema zote na ukaniondolea kila adhabu,

bado ujinga wangu na ujasiri wangu dhidi Yako haukukuzuia kunionyesha yale yatakayoniweka karibu Nawe, na ukaniwafikisha yale yatakayonisogeza karibu Nawe. Nikikuita unanijibu na nikikuomba unanipa, nikikutii unanishukuru na nikikushukuru unanizidishia. Hayo yote ni kukamilisha neema Zako juu yangu na ihsani Yako kwangu. Basi Umetakasika! Umetakasika! Kushinda mwanzilishi na mrudishaji, muhimidiwa na mtukuka. Na yametakasika Majina Yako na zimetukuka neema Zako, ni neema ipi Mungu Wangu nitakayohesabu kiidadi na kiutajo! Au ni upaji Wako upi nitakaoutolea shukurani! Na hali wenyewe Ewe Mola Mlezi ni mwingi na mkubwa kuliko uwezo wa kuhesabiwa na wenyе kuhesabu au kufikiwa na elimu ya wenyе kuhifadhi.

“Kisha Ewe Mwenyezi Mungu uliyoniondolea na kuniepushia mionganoni mwa madhara na maradhi ni mengi kushinda yaliyonidhihirikia mionganoni mwa afya na furaha. Na mimi nashahidilia Ewe Mungu Wangu kwa ukweli wa imani yangu, kwa kifungo cha uimara wa yakini yangu, kwa ikhlasi ya uwazi tauhidi yangu, kwa undani wa siri ya dhamiri yangu, kwa viambatishi vya mapitio ya nuru ya uoni wangu, kwa kunyanzi za ubapa wa paji langu la uso, kwa tundu la mapitio ya nafsi yangu, kwa maungio ya tundu la pua yangu, kwa njia ya tundu la sikio langu, kwa kile kilicho jumuishwa na kufunikwa na midomo yangu, kwa harakati za utamkaji wa ulimi wangu, kwa maungio ya kaakaa la kinywa changu na taya langu, kwa maoteo ya magego yangu na materemkio mazuri ya chakula changu na kinywaji changu, kwa ubebaji wa mfuko wangu wa ubongo na njia isiyo na kitu ya nyuzinyuzi za shingo yangu, kwa yale yaliyokusanywa na shimo la kifua changu, kwa vinyavyobebwa na teri ya moyo wangu, kwa kujishikiza kwa kinga ya moyo wangu, kwa vipande

vidogo nya nyama laini ya mzunguko wa ini langu.

“Na kwa yaliyokusanya na pande za mbavu zangu, kwa matundu ya maungio yangu, kwa mshiko wa vitendea kazi vyangu, kwa ncha za vidole vyangu, kwa nyama yangu, kwa damu yangu, kwa unyele wangu, kwa ngozi yangu, kwa mishipa yangu ya fahamu, kwa koromeo langu, kwa mifupa yangu, kwa ubongo wangu, kwa mishipa yangu, kwa viungo vyangu vyote na kwa yale yaliyojifuma siku za utoto wangu wa kunyonya, na kwa yale yaliyopunguzwa na ardhi toka kwangu, usingizi wangu, kuamka kwangu, utulivu wangu, harakati za kurukuu kwangu na kusujudu kwangu, kwamba lau ningejaribu na kujituma zama zote na miaka yote kama ningepewa umri huu, ili nitimize shukurani angalau ya neema Yako moja nisingeweza kufanya hivyo ila kwa neema Yako ambayo ingeniwajibisha nayo kukushukuru Wewe upya muda wote na kukutukuza upya muda wote.

“Ndio, na lau nitapupia mimi na wahasibu toka katika viumbe Wako kuhesabu kiwango cha neema Zako zilizotangulia na zilizopita hatutaweza kuifikia idadi yake wala kupata muda wake. Itawezekanaje hilo na hali Wewe umetoa habari ndani ya Kitabu Chako chenye kutamka na kilicho habari ya kweli: ‘Na kama mkihesabu neema za Mwenyezi Mungu, hamtaweba kuzihesabu.’ Kimesema kweli Kitabu Chako Ewe Mwenyezi Mungu na utoaji Wako wa habari, na wamefikisha Manabii Wako na Mitume Wako yale uliyowateremshia mionganoni mwa wahyi Wako, na ile sheria uliyowapa na dini uliyoileta kuititia kwao, isipokuwa ni kwamba mimi Ewe Mungu Wangu nashahidilia kwa juhudzi zangu, jitihada zangu, kiwango cha utii wangu na wasaa wangu, na ninasema na hali ni mwenye kuamini mwenye yakini, kila sifa njema ni

ya Mwenyezi Mungu ambaye hajajifanyia mtoto hata awe mwenye kurithiwa, na wala hana mshirika katika ufalme Wake hata awe mpinzani wake katika yale aliyoumba, wala hana rafiki kwa sababu ya udhaifu hata amsaidie katika aliyotengeneza.

“Ametakasika! Tena ametakasika! Lau kama wangelikuwako humo (mbinguni na ardhini) waungu wengine isipokuwa Mwenyezi Mungu, lazima zingeharibika na zingepasuka. Ametakasika Mwenyezi Mungu Mmoja wa pekee Mwenye kukusudiwa kwa haja, ambaye hakuzaa wala hakuzaaliwa, wala hana anayefanana Naye hata mmoja. Kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, himidi inayolingana na himidi ya Malaika Wake waliowekwa karibu ya Manabii Wake waliotumwa, na sala na salamu za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya chaguo Lake bora Muhammad hitimisho la Manabii, na juu ya aali zake wema watakasifu wenyewe ikhlasi.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie niwe nakuhofu Wewe kana kwamba mimi nakuona, na nipe furaha kwa kukuogopa Wewe na wala usinipe huzuni kwa kukuasi Wewe, niwekee heri katika maamuzi Yako na nitilie Baraka katika makadara Yako, mpaka nisipende kuharakishwa yale uliyochelewesha wala kucheleweshwa yale uliyoharakisha. Ewe Mwenyezi Mungu! Weka utajiri wangu ndani ya nafsi yangu, yakini ndani ya moyo wangu, ikhlasi katika amali yangu, nuru katika macho yangu na ujuzi katika dini yangu. Na nistareheshe kwa viungo vyangu na jaalia masikio yangu na macho yangu kuwa warithi wangu, na ninusuru dhidi ya yule aliyenidhulumu na nionyeshe mlipizaji wa kisasi changu na matakwa yangu, na yatulize macho yangu kwa hayo. Ewe Mwenyezi Mungu! Niondolee matatizo yangu, nisitiri aibu yangu,

nighufirie makosa yangu, mfukuze shetani wangu na fungua kitanzi changu, na nipe Ewe Mungu Wangu daraja la juu mno katika Akhera na dunia.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Una kila sifa njema kama ulivyonumba na ukafanya mwenye kusikia mwenye kuona, na una kila sifa njema kama ulivyonumba na ukafanya kiumbe hai niliye sawa, hiyo ni kwa kunirehemu na hali ulikuwa si muhitaji wa kuumbwa kwangu. Ewe Mola Mlezi tangu uliponumba na ukalinganisha sawa umbile langu. Ewe Mola Mlezi tangu uliponanzisha na ukapendezesha sura yangu. Ewe Mola Mlezi tangu uliponifanyia ihsani na uknipa afya njema katika nafsi yangu. Ewe Mola Mlezi tangu uliponilinda na ukaniwafikisha. Ewe Mola Mlezi tangu uliponineemesha na ukaniongoza. Ewe Mola Mlezi tangu uliponichagua na uknipa toka katika kila heri. Ewe Mola Mlezi tangu uliponilisha na ukainywesha. Ewe Mola Mlezi tangu uliponitajirisha na ukankinaisha. Ewe Mola Mlezi tangu uliponisaidia na uknipa nguvu. Ewe Mola Mlezi tangu uliponivisha kutoka katika sitara Yako safi na ukahirahisishia wema Wako wenye kutosheleza, mswalieMuhammad na aali Muhammad na nisaidie dhidi ya mabalaa ya dahari na mabalaa ya usiku na mchana. Niokoe na misukosuko ya dunia na matatizo ya Akhera, na nitosheleze shari ya yale wanayotenda madhalimu duniani.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ninalohofia nitosheleze, na ninalojihadhari nalo nikinge, na nipe ulinzi katika nafsi yangu na dini yangu na nihifadhi safarini, nirithi katika watu wangu na mali yangu na nitilie Baraka katika yale uliyoniruzuku, nipe unyenyekevu katika nafsi yangu na nipe adhama mbele ya macho ya watu, nisalimishe na shari ya majini na watu, usinifedheheshe kwa dhambi zangu na

usinifichulie siri yangu, usinipe majaribu kwa amali yangu, usinipokonye neema Zako na usinitegemeze kwa asiyekuwa Wewe. Mungu Wangu! Unaniegemeza kwa nani! Kwa mtu wa karibu ili anitenge, au kwa mtu wa mbali ili anichukie, au kwa wenyewe kuninyong'onyesha na hali Wewe ndiye Mola Wangu Mlezi na Mmiliki wa jambo langu. Nashtaki Kwako ugeni wangu, umbali wa nyumba yangu na kutezwa kwangu dhidi ya yule uliyemmilikisha jambo langu.

“Mungu Wangu! Usinishushie ghadhabu Yako kwani ukiwa hujanighadhibikia basi simjali asiyekuwa Wewe. Umetakasika! Isipokuwa ni kwamba afya Yako ni pana kwangu, hivyo nakuomba Ewe Mola Mlezi kwa nuru ya heshima Yako ambayo imeangaza mbingu na ardhi, na kwayo likaondolewa giza na kutengenezwa jambo la wale wa mwanzo na wale wa mwisho, usinifishe na hali ni mwenye kughadhibikiwa na Wewe na wala usiniteremshie adhabu Yako. Furaha ni Yako! Furaha ni Yako! Mpaka uniridhie kabla ya hiyo, hakuna mungu ila Wewe Mola Mlezi wa mji mtukufu, eneo la kumbukumbu tukufu, na Nyumba ya kale ambayo umeiwekea Baraka na umeifanya amani kwa watu.

“Ewe Ambaye alisamehe madhambi makubwa kwa uvumilivu Wake! Ewe Ambaye alimimina neema kwa fadhila Zake! Ewe Ambaye alitoa tele kwa ukarimu Wake! Ewe Uwezo wangu wakati wa shida yangu! Ewe Sahiba wangu wakati wa upweke wangu! Ewe Msaada wangu wakati wa matatizo yangu! Ewe Msimamizi wa neema yangu! Ewe Mungu Wangu na Mungu wa baba zangu Ibrahim na Ismail, Is'haqa na Ya'qub, na Mola Mlezi wa Jibril, Mikail na Israfil, na Mola Mlezi wa Muhammad mwisho wa Manabii na aali zake wateule, na Ewe

uliyeshusha Taurati na Injili, Zaburi na Furqani, na uliyeshusha Kaf, Haa, Yaa, Ain, Swad, na Twaha, Yasin na Qur’ani Tukufu, Wewe ndio kimbilio langu pindi njia zinaponisonga katika upana wake na ardhi inaponibana kwa upana wake. Na lau si rehema Yako ningekuwa mionganoni mwa walioangamia na Wewe ndiye Mwenye kufumbia macho kujikwaa kwangu. Na laiti si kunisitiri Kwako ningekuwa mionganoni mwa waliofedheheka na Wewe ni Mwenye kunipa nguvu kwa kuninusuru dhidi ya maadui zangu. Na lau si kunisaidia Kwako ningekuwa mionganoni mwa walioshindwa.

“Ewe Ambaye ameiteua nafsi Yake kwa ajili ya heshima na utukufu, hivyo mawalii Wake hutukuka kupitia utukufu Wake. Ewe Ambaye Malaika wameweka kwa ajili Yake nira ya unyenyekevu juu ya shingo zao, hivyo wao ni wenyenye kuhofu adhabu Yake. Anajua hiyana ya macho na yanayoficha vifua, na mambo ya ghaibu yanayoletwa na zama na dahari. Ewe Ambaye hakuna anayejua alivyo ila Yeye Mwenyewe! Ewe Ambaye hakuna anayejua Yeye ni nani ila Yeye Mwenyewe! Ewe Ambaye hakuna ajuaye anayoyajua ila Yeye Mwenyewe! Ewe Ambaye aliigandamiza ardhi juu ya maji na akaizua hewa kwa mbingu! Ewe Ambaye ana Majina Matukufu mno! Ewe Mwenye hisani ambayo milele haikatiki! Ewe aliyetoa kipando kwa ajili ya Yusuf katika nchi ya ukame na aliyemtoa kisimani na aliyemfanya mfalme baada ya utumwa! Ewe aliyemrudisha kwa Yaq’ub baada ya kuwa meupe macho yake kwa huzuni aliyokuwa akiizuia!

“Ewe aliyemuondolea Ayubu dhara na mtihani! Ewe alieuzuia mkono wa Ibrahimu usimchinje mwanae baada ya kuwa mtu mzima na kuisha umri wake! Ewe Ambaye alimjibu Zakariya akampa Yahya na hakumwacha peke

yake mpweke! Ewe Ambaye alimtoa Yunus toka katika tumbo la samaki! Ewe Ambaye alipasua bahari kwa ajili ya wana wa Israil na akawaokoa, na akawafanya Firaun na jeshi lake kuwa mionganini mwa waliozamishwa! Ewe Ambaye alipeleka pepo kuwa habari njema kabla ya kufika rehemaa Zake! Ewe Ambaye hana haraka na aliyemuasi kati ya viumbe Wake! Ewe Ambaye aliwaokoa wachawi baada ya upingaji wa muda mrefu, na walikuwa ndani ya neema Zake wakila riziki Zake na wakimwabudu asiyekuwa Yeye, na walikuwa wamemkataa, wamempanga na kuwakadhibisha Mitume Wake.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Mwanzilishi! Ewe Muumbaji usiye na mpinzani! Ewe wa daima usiye na mwisho! Ewe uliye hai pindi hakuna aliye hai! Ewe Mwenye kuhuisha wafu! Ewe Mwenye kusimamia kila nafsi kwa yale iliyochuma! Ewe Ambaye shukrani zangu ni chache Kwake lakini hajaninyima, makosa yangu ni makubwa lakini hajanifiedhesha na ameniona nikiwa ndani ya maasi lakini hajanitangaza. Ewe Ambaye alinihifadhi udogoni! Ewe Ambaye ameniruzuku ukubwani! Ewe Ambaye hisani Zake kwangu hazihesabiki na neema Zake hazilipiki! Ewe Ambaye amenionyesha heri na hisani nami nimemwonyesha ubaya na maasi!

“Ewe Ambaye ameniongoza kwa imani kabla sijajua kushukuru neema! Ewe Ambaye nilimwita hali mgonjwa akaniponyesha, hali mtupu akanivisha, hali mwenye njaaakanishibisha, hali mwenye kiu akanikatia kiu, hali dhalili akanitukuza, hali jahili akanifundisha, hali mmoja akanizidisha, hali sipo akanirudisha, hali mkata akanitajirisha, hali mwenye kutaka msaada akanisaidia, na hali tajiri na hajaninyang’anya, na nikajizuia na yote hayo lakini akanianzisha. Hivyo kila sifa njema na shukrani ni

Yako Ewe Ambaye alifumbia macho kujikwaa kwangu, akaondoa matatizo yangu, akajibu dua yangu, akasitiri aibu yangu, akaghufiri dhambi zangu, akanifikishia ombi langu naakanisaidia juu ya adui yangu. Na kama nitahesabu neema Zako, fadhila Zako na hisani za upaji Wako sintaweza kuzihesabu.

“Ewe Bwana Wangu! Wewe ndiye uliyefadhili, Wewe ndiye uliyeneemesha, Wewe ndiye uliyefanya hisani, Wewe ndiye uliyependezesha, Wewe ndiye uliyependelea, Wewe ndiye uliyekamilisha, Wewe ndiye uliyeruzuku, Wewe ndiye uliyewafikisha, Wewe ndiye uliyetoea, Wewe ndiye uliyetajirisha, Wewe ndiye uliyekinaisha, Wewe ndiye uliyehifadhi, Wewe ndiye uliyetosheleza, Wewe ndiye uliyetongoza, Wewe ndiye uliyekinga, Wewe ndiye uliyesitiri, Wewe ndiye uliyeghufiri, Wewe ndiye uliyepunguza, Wewe ndiye uliyemakinisha, Wewe ndiye uliyetia nguvu, Wewe ndiye uliyesaadia, Wewe ndiye uliybunga mkono, Wewe ndiye uliyetongeza nguvu, Wewe ndiye uliyenusuru, Wewe ndiye uliyeponya, Wewe ndiye uliyetoea afya njema na Wewe ndiye uliyekirimu. Umetakasika na umetukuka!

“Kila sifa njema ni Yako daima na shukurani ni Yako milele. Kisha mimi Ewe Mungu Wangu naungama dhambi zangu basi nighufirie. Mimi ndiye niliyefanya ubaya, Mimi ndiye niliyekosea, Mimi ndiye niliyekusudia, Mimi ndiye niliyehahili, Mimi ndiye niliyeghafilika, Mimi ndiye niliyesahau, Mimi ndiye niliyetegemea, Mimi ndiye niliyetenda makusudi, Mimi ndiye niliyahidi, Mimi ndiye niliyekhalifu, Mimi ndiye niliyevunja, Mimi ndiye niliyeungama, Mimi ndiye niliyekiri neema Zako zilizo juu yangu na kwangu na ninazikimbia dhambi zangu basi zighufiri. Ewe Ambaye dhambi za waja Wake hazimdhuru,

Naye si Mwenye kuhitajia utiifu wao, na ni Mwenye kumwafikisha kwa msaada Wake na rehema Zake yule atakayetenda mema mionganini mwao.

“Kila sifa njema ni Yako Mungu Wangu na Bwana Wangu, Mungu Wangu uliniamuru nami nikakuasi, ukankataza nami nikatenda katazo Lako, hivyo nimekuwa ni mtu nisiye na udhuru nitakaotoa, wala nguvu itakayonisaidia. Basi nitakupokea kwa kitu gani Ewe Bwana Wangu! Je ni kwa masikio yangu au kwa macho yangu au ulimi wangu, au ni kwa mkono wangu au mguu wangu, hivyo vyote si neema Zako zilizopo kwangu na kwa vyote hivyo nimekuasi Ewe Bwana Wangu! Una hoja na njia juu yangu.

“Ewe ambaye umenisitiri dhidi ya mababa na akina mama wasinifokee, na dhidi ya jamaa na ndugu wasiniaibishe, na dhidi ya watawala wasiniadhibu. Na lau wangeyaona Ewe Bwana Wangu yale uliyoyaona toka kwangu basi wasingenivumilia wangenikataa na kunitenga. Basi ni mimi hapa Ewe Mungu Wangu mbele Yako Ewe Bwana Wangu na hali ni mnyenyekevu dhalili, mnyonge duni, sina udhuru nitakaotoa wala nguvu itakayonisaidia, wala hoja nitakayotoa wala atakayesema: sijatenda dhambi wala sijatenda kosa.

“Hakuna upingaji utakaoninufaisha Ewe Bwana Wangu hata nikipinga, itawezekanaje hilo na hali viungo vyangu vyote vinatoa ushahidi juu yangu kwa yale niliyotenda, na nimejua kwa yakini bila shaka kwamba hakika Wewe ni Mwenye kunihoji kuhusu mambo mazito, na kwamba hakika Wewe ni hakimu mwadilifu ambaye hadhulumu, na uadilifu Wako ni wenye kuniangamiza, nami ni mwenye kuukimbia kila uadilifu Wako. Hivyo ikiwa utaniadhibu Ewe Mungu Wangu basi ni kwa sababu ya dhambi zangu baada ya hoja Yako kwangu. Na ikiwa utanisamehe basi ni

kwa sababu ya uvumilivu Wako, fadhila Yako na ukarimu Wako.

“Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa madhalimu. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekuomba maghfira. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekupwekesha. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekutetemeka. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekutaraji. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekraghba. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekufanya tahalili. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekufanya tasbih. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika hakika mimi nilikuwa mionganii mwa wenyekutoatakbira. Hakuna mungu ila Wewe, Umetakasika Mola Wangu Mlezi na Mola Mlezi wa baba zangu waliotangulia.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Huu ni wasifu wangu juu Yako na hali ni mwenye kutukuza, na ikhlasi yangu katika kukutaja Wewe na hali ni mwenye kupwekesha, na kukiri kwangu neema Zako na hali ni mwenye kuzihesabu, ijapokuwa ni mwenye kukiri kwamba hakika mimi sijazihesabu kutokana na wingi wake, utele wake, udhihirikaji wake na kutangulia kwake mpaka leo, kwani bado hujaacha kunifunika kwazo tangu uliponiumba na tangu mwanzo wa umri, kwa kuniepusha na ufakiri,

kuniondolea dhara, kunisababishia wepesi, kuniondolea zito, kuniondolea shida, kuupa afya mwili na kuwa na usalama katika dini. Na lau viumbe Wako wote wa mwanzo na wa mwisho wangenisaidia katika kiwango cha kutaja neema Zako bado nisingeweza na wala wao wasingeweza. Umetakasika na umetukuka kushinda bwana mkarimu, adhimu na mwenye huruma. Neema Zako hazihesabiki na sifa Zako hazifikiwi, na wala neema Zako hazilipwi. Msalie Muhammad na aali Muhammad na timiza juu yetu neema Zako na tupe furaha kwa kukutii Wewe.

“Umetakasika, hakuna mungu ila Wewe. Ewe Mwenyezi Mungu hakika Wewe unamjibu mwenye kudhikika na unaondoa dhiki, unamsaidia mwenye matatizo na unamponya mgonjwa, unamtajirisha fakiri na unamganga aliyeunjika, unamhurumia mdogo na kumsaidia mkubwa, na hakuna msaidizi asiyekuwa Wewe wala mwenye uwezo kuliko Wewe, na Wewe ni Mtukufu Mkuu. Ewe Mwenye kumpa uhuru mfungwa aliye katika pingu! Ewe Mwenye kumruzuku mtoto mdogo! Ewe Kinga ya mwenye hofu mwenye kuomba hifadhi! Ewe Ambaye hana mshirika wala waziri! Msalie Muhammad na aali Muhammad, na nipe jioni hii kile kilicho bora kushinda ulichotoa na kumpatia yejote kati ya waja Wako mionganoni mwa neema unayomgawia, bonasi unayompa tena, balaa unayoondoa, mateso unayoondoa, dua unayoisikia, jema unalolipokea na baya unalosamehe, hakika Wewe ni Mpole Mwenye habari wa yale unayoyataka na ni Muweza wa kila kitu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika Wewe upo karibu kushinda kila aliyeitwa, Mwepesi kushinda kila aliyejibu, Mkarimu kushinda kila aliyesamehe, Mwingi wa kutoa kushinda kila aliyetoa, na Msikivu kushinda kila

aliyeombwa. Ewe Mwingi wa rehema duniani na akhera na Mwenye kuzirehemu, hakuna muombwa mfano Wako wala mwenye kutarajiwa asiyekuwa Wewe. Nilikuita ukanijibu na nikakuomba ukaniipa, nikaja Kwako ukanirehemu na nikakutegemea Wewe ukaniokoa, na nikakimbilia Kwako ukanitosheleza. Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad mja Wako na Mtume Wako na Nabii Wako, na aali zake wote wema watakasifu, na tutimizie neema Zako na tufurahishe kwa zawadi Yako, tuandike kuwa ni wenye kukushukuru na ni wenye kutaja neema Zako, amina, amina Ewe Mola Mlezi wa viumbe wote.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Ewe Ambaye alimiliki na hatimaye akaweza, akaweza na hatimaye akatawala, akaasiwa na hatimaye akasitiri, akaombwa maghfira na hatimaye akaghufiria. Ewe lengo la wenye kutafuta walio na raghaba na uliye kilele cha matumaini ya wenye kutaraji. Ewe uliyekidhibiti kila kitu kwa elimu na akawajumuisha kwenye huruma, rehema na upole wale wenye kuomba pepo. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika sisi tunaelekea Kwako jioni hii ambayo umeipa sharafu na kuitkuza kuititia Muhammad Nabii Wako, Mtume Wako, chaguo Lako bora kati ya viumbe Wako na mwaminifu juu ya wahyi Wako, mtoa habari njema na mwonyaji, taa itoayo nuru, ambaye umewaneemesha Waislamu na umemfanya rehema kwa walimwengu wote.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Msalie Muhammad na aali Muhammad kama anavyostahiki hilo Muhammad kutoka Kwako Ewe Adhimu. Msalie yeye na aali zake wote wateule wema waliotakasika, na tufunike msamaha Wako kwani sauti kwa lugha mbalimbali zimeelekea Kwako kwa kulia. Tuwekee Ewe Mwenyezi Mungu jioni hii fungu toka katika kila heri unayoigawa baina ya waja Wako, nuru

unayoongoza kwayo, rehema unayoieneza, baraka unayoiteremsha, afya unayovisha, na riziki unayoigawa Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu. Ewe Mwenyezi Mungu! Tugeuze wakati huu tuwe wenye kufaulu, wenye kufanikiwa, wachamungu na wenye kubarikiwa. Na wala usituweke mionganoni mwa wenye kukata tamaa na wala usitukoseshe rehema Zako, wala usitunyime yale tunayotaraji toka katika fadhila Zako, wala usitufanye wenye kunyimwa rehema Zako, wala wenye kukata tamaa na yale tunayotaraji mionganoni mwa zawadi Zako, wala usiturudishe mikono mitupu na wala tusifukuzwe toka mlangoni Kwako.

“Ewe Mkarimu kushinda wakarimu wote na Mfadhili kushinda wafadhili wote, tumegeukia Kwako na hali ni wenye yakini, na ni wenye kuizuru na kuiendea Nyumba Yako Tukufu, basi tusaidie kutekeleza ibada zetu, tukamilishie Hijja yetu na tusamehe na utupe afya njema, kwani tumenyoosha Kwako mikono yetu nayo ina alama ya udhalili wa kuungama. Ewe Mwenyezi Mungu! Tupe jioni hii yale tuliyokuomba na tutosheleze yale tuliyokuomba ututoshleze, kwani hatuna wa kututoshleza asiyekuwa Wewe na wala hatuna Mola Mlezi asiyekuwa Wewe, hukumu Yako ni yenye kufanya kazi kwetu, elimu Yako ni yenye kutuzunguka, majaaliwa Yako ni adilifu kwetu, basi tukidhie heri na tujaalie mionganoni mwa watu wa heri. Ewe Mwenyezi Mungu! Tujazie kwa ukarimu Wako malipo makubwa, dafina ya thamani na wepesi wa kudumu, tughufirie dhambi zetu zote na wala usituhilikishe pamoja na wenye kuhiliki, wala usituondolee huruma Yako na rehema Yako Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Tujaalie katika wakati huu

miongoni mwa aliyekuomba Nawe ukampa, akakushukuru Nawe ukamwongeza, akakimbilia Kwako Nawe ukampokea, na akajitoa katika dhambi zake zote kwa kukimbilia Kwako Nawe ukamghufiria, Ewe Mwenye utukufu na ukarimu. Ewe Mwenyezi Mungu! Tuwafikishe, tuongoze njia na pokea maombi yetu, Ewe uliye bora kushinda kila aliyeombwa na Ewe aliye Mrehemevu kushinda kila aliyeombwa rehema. Ewe Ambaye haufichiki Kwake mpepeso wa macho wala mtupo wa macho, wala yale yaliyotulia mafichoni wala yale yaliyokusanywa na dhamira za nyoyo, yote hayo yamehesabiwa na elimu Yako na yamefikiwa na uvumilivu Wako. Umetakasika na umeepukana na hayo wayasemayo kwa uepukano mkubwa. Zinakutukuza Wewe mbingu saba na ardhi na vilivyomo ndani yake, na hakuna chochote isipokuwa kinakusabihii kwa sifa Zako njema.

“Una kila sifa njema, utukufu na uadhama wa juu, Ewe Mwenye utukufu na ukarimu, fadhila na uneemeshaji na neema kubwa, na Wewe ni Mkarimu Mfadhilli, Mpole, Mwenye huruma. Ewe Mwenyezi Mungu! Nipanulie riziki Yako ya halali, nipe afya katika mwili wangu na dini yangu, niondolee hofu na ikomboe shingo yangu na moto. Ewe Mwenyezi Mungu! Usifanyie hila na wala usinivute kidogo kidogo na wala usinidanganye, na niondolee shari za mafasiki wa kijini na wa kibinadamu.

“Ewe Msikivu kushinda wote wenyewe kusikia! Ewe Mwenye kuona kushinda wote wenyewe kuona! Ewe Mwepesi kushinda wote wenyewe kuhesabu! Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenyewe kurehemu! Msalie Muhammad na aali Muhammad mabwana wema. Na ninakuomba Ewe Mwenyezi Mungu haja yangu ambayo iwapo utanipa hayatonidhuru yale uliyoninyima, na iwapo

utaninyima hayatoninufaisha yale uliyonipa, nakuomba ukombozi wa shingo yangu dhidi ya moto, hakuna mungu ila Wewe, peke Yako huna mshirika. Ufalme ni Wako na kila sifa njema ni Yako na Wewe ni Muweza wa kila kitu. Ewe Mola Mlezi! Ewe Mola Mlezi! Ewe Mola Mlezi!

“Mungu Wangu mimi ni fakiri katika utajiri wangu ni vipi nisiwe fakiri katika ufkiri wangu! Mungu Wangu mimi ni jahili katika elimu yangu vipi nisiwe jahili katika ujahili wangu! Mungu Wangu hakika kupishana kwa tadbirdi Yako na wepesi wa kuzama makadara Yako vimewazuia waja Wako wenye kukujuu kutegemea kupewa na kukata tamaa na Wewe wakati wa balaa. Mungu Wangu kwangu yanatoka yanayolingana na uduni wangu na Kwako yanatoka yanayolingana na ukarimu Wako. Mungu Wangu umejisifu kwa upole na huruma kwangu kabla ya kuwepo udhaifu wangu, je sasa waninyima hivyo viwili (upole na huruma) baada ya kuwepo udhaifu wangu? Mungu Wangu iwapo mema yatadhiihiri kutoka kwangu basi ni kwa fadhila Zako na una neema juu yangu, na iwapo mabaya yatadhiihiri toka kwangu basi ni kwa uadilifu Wako na una hoja juu yangu.

“Mungu Wangu, vipi unaniacha nijitegemee na hali Wewe umechukua dhamana yangu, na ni vipi nidhulumiwe na hali Wewe ndiye Mwenye kulinusuru, au vipi nisifanikiwe na hali Wewe ndiye mwenye kunikirimu. Ni mimi hapa natawassali Kwako kuititia uhitaji wangu Kwako, na ni vipi nitawassali Kwako kuititia kilicho muhali kufika Kwako, au ni vipi nilalamike Kwako hali yangu na hali yenyewe haifichikani Kwako, au vipi nifafanue kauli yangu na hali yenyewe iko wazi Kwako, au vipi ufelishe matumaini yangu na hali yenyewe yamefika Kwako, au vipi hali zangu zisiwe nzuri na hali zimesimama kuititia Kwako. Mungu

Wangu, ni Mpole kwangu uliyoje pamoja na ujinga wangu mkubwa!

“Ni Mwenye rehema kwangu uliyoje pamoja na ubaya wa vitendo vyangu. Mungu Wangu, ni uliye karibu kwangu kiasi gani nami niko mbali na Wewe kiasi gani! Ni Mwenye huruma kwangu uliyoje basi ni kitu gani kitakachonizua Nawe. Mungu Wangu, nimejua kupitia tofauti ya athari na mihamo ya aina mbalimbali kwamba unachokitaka kutoka kwangu ni kujitambulisha kwangu katika kila kitu mpaka nisikose kukujua katika kila kitu. Mungu Wangu, kila uduni wangu unaponiziba mdomo basi ukaribu Wako hunitamkisha, na kila sifa zangu zinaponikatisha tamaa neema Zako hunitamanisha. Mungu Wangu, yule ambaye mazuri yake ni mabaya ni vipi mabaya yake yasiwe mabaya, na yule ambaye ukweli wake ni madai vipi madai yake yasiwe madai. Mungu Wangu, hukumu Yako ni yenye kufanya kazi na utashi Wako ni wenye kutiisha, havijamwachia mwenye la kusema chochote cha kusema wala mwenye hali yoyote.

“Mungu Wangu, ni twaa ngapi nimezijenga na hali ngapi nimeziimarisha lakini uadilifu Wako umebomoa utegemezi wangu kwazo bali fadhila Zako zimeninyanya tokwa kwenye mbomoko wake. Mungu Wangu, hakika Wewe unajua kwamba ijapokuwa utiifu wangu haujadumisha kitendo yakini lakini mapenzi na azma vimedumu. Mungu Wangu, vipi nitaazimia na hali Wewe ni Kahari, na ni vipi nisiazimie na hali Wewe ni mwamrishaji. Mungu Wangu, kutaradadi kwangu katika athari kunawajibisha umbali wa eneo la kuzuru basi nikusanye Kwako kupitia utumishi utakaonifikisha Kwako. Vipi Wewe huthibitishwa kupitia kile ambacho uwepo wake unakuhitajia Wewe, hivi kisichokua Wewe kina mdhihiriko usiokuwa nao Wewe

hata ipelekee chenyewe kukudhihirisha Wewe! Kwani ni lini ulijificha hata uhitaji dalili itakayokuthibitisha Wewe, na ni lini ulijitenga mbali mpaka athari ziwe ndizo zinazofikisha Kwako. Limepofuka jicho lisilokuona kwamba ni mwenye kulifuatilia, na imepata hasara bishara ya mja ambaye hajakuwekea fungu la mapenzi Yako.

“Mungu Wangu, umeamuru kurejea kwenye athari basi nirejeshe Kwako kwa vazi la nuru na uongofu wa ujuzi, mpaka nirejee Kwako toka kwenye athari kama nilivyoingia Kwako toka humo, na hali ni mwenye kuhifadhiwa nisizione na ni mwenye hima ya juu isiyozitegemea, hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu. Mungu Wangu, huu ni udhalili wangu uliyo dhahiri mbele Yako na hii ni hali yangu haifichiki Kwako, kutoka Kwako naomba kufika Kwako na kupitia Kwako nakuthibitisha Wewe basi niongoze kwa nuru Yako nifike Kwako, na nisimamishe mbele Yako kwa utumwa wa kweli. Mungu Wangu, nielimishe toka katika elimu Yako iliyohifadhiwa na nikinge kwa sitara Yako iliyokingwa. Mungu Wangu, nipe uhakika kupitia uhakika wa watu wa karibu na nipitishe mapito ya watu wenye mvuto. Mungu Wangu, nitosheleze kwa tadbiri Yako kwangu dhidi ya tadbiri yangu na kwa chaguo Lako dhidi ya chaguo langu, na nisimamishe juu ya vituo vyta dharura. Mungu Wangu, nitoe kwenye udhalili wa nafsi yangu, nitakase na shaka yangu na shirki yangu kabla ya kuingia (mazamio yangu)kaburini kwangu.

“Nataka msaada Kwako basi nisaidie, natawakali Kwako basi usiniache mwenyewe, Wewe tu nakuomba basi usinirudishe mikono mitupu, natamani fadhila Zako basi usininyime, najinasibisha na heshima Yako basi usinitenge na ninasimama mlangoni Kwako basi usinifukuze. Mungu

Wangu, ridhaa Yako imeepukana na sababu toka Kwako
vipi sasa itakuwa na sababu toka kwangu! Mungu Wangu,
Wewe kwa asili Yako hauhitaji manufaa yafike Kwako
toka Kwako vipi sasa usiwe usiyenihitajia mimi! Mungu
Wangu, hakika majaliwa na makadara yananitia tamaa na
hakika hawaa kwa kamba za matamanio imeniteka basi
kuwa mwenye kuninusuru mpaka uninusuru na unifumbue
macho, na nitosheleze kwa fadhila Zako mpaka nitosheke
Nawe dhidi ya utafutaji wangu.

“Wewe Ndiye uliyeangaza nuru ndani ya nyoyo za mawalii
Wako mpaka wakakujua na wakakupwekesha. Na Wewe
Ndiye uliyewatoa wengine ndani ya nyoyo za vipedzi
Vyako mpaka wakawa hawajampenda asiyekuwa Wewe na
wala hawajakimbilia kwa mwингine asiyekuwa Wewe.
Wewe Ndiye Mwenye kuwaliwaza pale walimwengu
walipowatia woga. Wewe Ndiye uliyewaongoza pale dalili
zilipowabainikia. Amepata nini aliyekukosa na amekosa
nini aliyekupata, bila shaka amefeli yule aliyeridhia
mbadala asiyekuwa Wewe, na bila shaka amepata hasara
aliyejitenga Nawe na hali ni mwenye kugeuka. Vipi
atarajiwe asiyekuwa Wewe na hali Wewe hukukata hisani,
na vipi itafutwe toka kwa mwингine asiyekuwa Wewe na
hali hukubadili ada ya kufanya hisani.

“Ewe Ambaye amewaonjesha vipedzi Vyake utamu wa
maliwazo nao wakasimama mbele Yake na hali ni wenye
kuomba dua. Ewe Ambaye amewavisha mawalii Wake
mavazi ya haiba Yake nao wakasimama mbele Yake na
hali ni wenye kuomba maghfira. Wewe ni Mwenye
Kukumbuka kabla ya wakumbukaji na Wewe ni Mwenye
kuonyesha hisani kabla ya mwelekeo wa wenye kuabudu.
Wewe ni Mkarimu wa kutoa kabla ya ombi la waombaji na
Wewe ni Mpaji kisha ni mionganoni mwa wakopaji wa yale

uliyotupa. Mungu Wangu nitafute kwa rehema Zako mpaka nifike Kwako, na nivute kwa neema Yako mpaka nikuelekee Wewe. Mungu Wangu, hakika matarajio yangu Kwako hayakatiki hata kama nikikuasi, kama ambavyo hofu yangu hainitengi hata kama nikikutii, Na bila shaka malimwengu yamenisukuma kuja Kwako na kujuua kwangu ukarimu Wako kumenifikasiha Kwako.

“Mungu Wangu, vipi nifeli na hali Wewe ndio matumaini yangu, au vipi nidhalilishwe na hali mategemeo yangu ni juu Yako. Mungu Wangu, vipi naomba utukufu na hali umeniiamarisha katika udhalili, au vipi nisiombe utukufu na hali umeninasibisha Kwako. Mungu Wangu, vipi nisifikirike na hali Wewe ndiye uliyenisimamisha ndani ya mafakiri, au vipi nafakirika na hali Wewe ndiye uliyenitosheleza kwa ukarimu Wako na Wewe Ndiye Ambaye hakuna mungu mwingine asiyekuwa Wewe. Umejitambulisha kwenye kila kitu hivyo hakuna chochote kisichokujua, na Wewe Ndiye ulijejtambulisha kwangu katika kila kitu, basi nikakuona Mwenye kudhihirika katika kila kitu na Wewe ni dhahiri kwenye kila kitu.

“Ewe Ambaye amejitegemea kwa rehema Zake basi Arshi ikawa ghaibu katika dhati Yake, umefuta athari kwa athari na umewafuta wasiokuwa Wewe kwa vinavyozizunguka falaki za nuru. Ewe Ambaye amejificha katika mahema ya Arshi Yake macho yasimdiriki. Ewe Ambaye amejidhihirisha kwa uzuri Wake wote na hatimaye adhama Yake ikatimia toka kwenye kujitegemea, vipi ukichike na hali Wewe ni dhahiri, au vipi usiwepo na hali Wewe ni mfuatiliaji uliyopo, hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu, na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu peke Yake.”

Sema mwishoni mwa mchana wa siku ya Arafa:

يَا رَبِّ انْ ذُنُوبِي لَا تَضْرِبَكَ، وَإِنَّ مَغْفِرَتَكَ لِي لَا تَنْقُصُكَ، فَاعْطِنِي
مَا لَا يَنْقُصُكَ، وَاغْفِرْ لِي مَا لَا يَضْرِبَكَ

“Ewe Mola Mlezi! Hakika dhambi zangu hazikudhuru, na hakika maghfira Yako kwangu hayakupunguzii chochote, basi nipe yale yasiyokupunguzia chochote na nighufirie yale yasiyokudhuru chochote.”

Pia sema:

اللّٰهُمَّ لَا تَحِرِّ مُنْيٍ خَيْرًا مَا عِنْدَكَ لِشَّرٍّ مَا عِنْدِي فَإِنْ أَنْتَ لَمْ
تَرْحَمْنِي بِتَعْبِي وَنَصَبِي فَلَا تَرْحِمْنِي أَجْرَ الْبُصَابِ عَلَى مُصِيبَتِهِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Usininyime heri iliyoko Kwako kwa sababu ya shari iliyoko kwangu, kwani ikiwa Wewe hujanirehemu kwa mchoko wangu na taabu zangu basi usininyime malipo ya msiba ya aliyepatwa na msiba.”

Na kwa mujibu wa riwaya ya Sayyid Ibnu Tawus ni mustahabu itakapokaribia kuzama jua la siku ya Arafa kusoma dua Asharati.

Ziyaratul-Jami'a:

Na katika siku hii soma Ziyaratul-Jami'a ya tatu, nayo ni:

السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا رَسُولَ اللَّهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا نَبِيَّ اللَّهِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا خَيْرَةَ اللَّهِ مِنْ خَلْقِهِ وَأَمِينَهُ عَلَى وَحْيِهِ، السَّلَامُ عَلَيْكَ
يَا مَوْلَايَ يَا أَمِيرَ الْمُؤْمِنِينَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ، أَنْتَ حَجَّةُ
اللَّهِ عَلَى خَلْقِهِ وَبَابُ عِلْمِهِ وَوَصِّيُّ نَبِيِّهِ وَالْخَلِيفَةُ مِنْ بَعْدِهِ فِي
أُمَّتِهِ، لَعَنَ اللَّهِ أُمَّةً غَصَبْتُكَ حَقًّا وَقَعَدْتُ مَقْعَدَكَ، أَنَا بَرِّيُّ
مِنْهُمْ وَمِنْ شَيْعَتِهِمْ إِلَيْكَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا فَاطِمَةَ الْبَتُولُ،
السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا زَيْنَ نِسَاءِ الْعَالَمَيْنَ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا بَنْتَ
رَسُولِ اللَّهِ رَبِّ الْعَالَمَيْنَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَيْهِ، السَّلَامُ
عَلَيْكَ يَا أُمَّةَ الْحَسَنِ وَالْحُسَيْنِ،
لَعَنَ اللَّهِ أُمَّةً غَصَبْتُكَ حَقًّا وَمَنَعْتُكَ مَا جَعَلَهُ اللَّهُ لَكِ حَلَالًا،
أَنَا بَرِّيُّ إِلَيْكَ مِنْهُمْ وَمِنْ شَيْعَتِهِمْ، السَّلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا

آبَا مُحَمَّدَ الْحَسَنِ الرَّكِنِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ لَعْنَ اللَّهِ أُمَّةً
قَتَلَتْكَ وَبَا يَعْتُ فِي أَمْرِكَ وَشَايَعَتْ أَنَا بَرْئٌ إِلَيْكَ مِنْهُمْ وَمِنْ
شِيعَتِهِمْ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا عَبْدِ اللَّهِ الْحُسَيْنَ بْنَ
عَلِيٍّ صَلَواتُ اللَّهِ عَلَيْكَ وَعَلَى آبَيكَ وَجَدِّكَ مُحَمَّدَ صَلَّى اللَّهُ
عَلَيْهِ وَآلِهِ، لَعْنَ اللَّهِ أُمَّةً اسْتَحْلَتْ دَمَكَ، وَلَعْنَ اللَّهِ أُمَّةً
قَتَلَتْكَ وَاسْتَبَاحَتْ حَرَبَيْكَ، وَلَعْنَ اللَّهِ أَشْيَاعَهُمْ وَأَتْبَاعَهُمْ،
وَلَعْنَ اللَّهِ الْبُهَيْدِينَ لَهُمْ بِالْتَّكِينِ مِنْ قِتَالِكُمْ، أَنَا بَرْئٌ إِلَى اللَّهِ
وَإِلَيْكَ مِنْهُمْ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا مُحَمَّدَ عَلِيَّ بْنَ
الْحُسَيْنِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا جَعْفَرَ مُحَمَّدَ بْنَ عَلِيٍّ،
أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا عَبْدِ اللَّهِ جَعْفَرَ بْنَ مُحَمَّدَ،

أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا الْحَسَنِ مُوسَى بْنَ جَعْفَرَ، أَلْسَلَامُ
عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا آبَا الْحَسَنِ عَلِيَّ بْنَ مُوسَى، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا
مَوْلَايَ يَا آبَا جَعْفَرَ مُحَمَّدَ بْنَ عَلِيٍّ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَايَ يَا

أَبَا الْحَسَنِ عَلَيْهِ بُنَّ مُحَمَّدٍ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَانِي يَا أَبَا
 مُحَمَّدَ الْحَسَنَ بْنَ عَلَيْهِ، أَلْسَلَامُ عَلَيْكَ يَا مَوْلَانِي يَا أَبَا الْقَاسِمِ
 مُحَمَّدَ بْنَ الْحَسَنِ صَاحِبَ الزَّمَانِ، صَلَّى اللَّهُ عَلَيْكَ وَعَلَى
 عِتْرَتِكَ الطَّاهِرَةِ الطَّيِّبَةِ، يَا مَوَالِيَ كُونُوا شُفَعَاءِ فِي حَطَّ وِزْرِي
 وَخَطَلِيَّاَيِ، آمَنْتُ بِاللَّهِ وَبِإِيمَانِكُمْ، وَأَتَوْالِيَ آخِرَكُمْ بِإِيمَانِ
 أَتَوْالِيَ أَوَّلَكُمْ، وَبَرِئْتُ مِنَ الْجِبْتِ وَالْطَّاغُوتِ وَاللَّاتِ وَالْعَزْزِيِّ، يَا
 مَوَالِيَ أَنَا سِلْمُ لِيَنْ سَالِيَكُمْ، وَحَرَبُ لِيَنْ حَارَبَكُمْ، وَعَدُوُ لِيَنْ
 عَادَكُمْ، وَوَلِيَ لِيَنْ وَالاَكْمُ إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ وَلَعْنَ اللَّهُ ظَالِيَكُمْ
 وَغَاصِبِيَكُمْ، وَلَعْنَ اللَّهِ أَشْيَاعَهُمْ وَاتْبَاعَهُمْ وَأَهْلَ مَذْهِبِهِمْ،
 وَآبُرَأُ إِلَى اللَّهِ وَإِلَيْكُمْ مِنْهُمْ.

“Amani iwe juu yako ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yako ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu!
 Amani iwe juu yako ewe chaguo bora la Mwenyezi Mungu
 kati ya viumbe Wake na ewe mwaminifu wa wahyi Wake.
 Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu kiongozi wa
 waumini! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu! Wewe
 ndiye hoja wa Mwenyezi Mungu juu ya viumbe Wake,
 mlango wa elimu Yake, Wasii wa Nabii Wake na khalifa

wake kwa umma wake baada yake. Mwenyezi Mungu aulaani umma uliokupora haki yako na ukakaa nafasi yako, mimi ni mwenye kujitenga nao wao na wafuasi wao kwa kujielekeza kwako.

“Amani iwe juu yako Fatima al-Batul! Amani iwe juu yako ewe pambo la wanawake wa ulimwenguni! Amani iwe juu yako ewe binti ya Mtume wa Mola Mlezi wa viumbe wote! Sala ya Mwenyezi Mungu iwe juu yako na juu yake. Amani iwe juu yako ewe mama wa Hasan na Husein! Mwenyezi Mungu aulaani umma uliokupora haki yako na ukakuzuia yale aliyoyafanya Mwenyezi Mungu halali kwako, mimi ni mwenye kujitenga nao wao na wafuasi wao kwa kujielekeza kwako. Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Muhammad Hasan az-Zakiyyu! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu, Mwenyezi Mungu aulaani umma uliokuwa na ukatoa kiapo katika jambo lako na ukaandamana, mimi ni mwenye kujitenga nao wao na wafuasi wao kwa kujielekeza kwako.

“Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Abdillah Husain bin Ali! Sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya baba yako na babu yako Muhammad (s.a.w.w.), Mwenyezi Mungu aulaani umma uliohalalisha damu yako, na Mwenyezi Mungu aulaani umma uliokuuwa na ukavunja utukufu wako, na Mwenyezi Mungu awalaani wafuasi wao na wapambe wao, na Mwenyezi Mungu awalaani wale waliowaandalia mazingira kwa kuwapa nafasi ya kuwauweni nyinyi, mimi ni mwenye kujitenga nao kwa kujielekeza kwa Mwenyezi Mungu na kwako.

“Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Muhammad Ali bin Husein! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Ja’far Muhammad bin Ali! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Abdillah Ja’far

bin Muhammad! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Hasan Musa bin Ja'far! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Hasan Ali bin Musa! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Ja'far Muhammad bin Ali! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Hasan Ali bin Muhammad! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Muhammad Hasan bin Ali! Amani iwe juu yako Ewe Bwana Wangu ewe Abu Qasim Muhammad bin Hasan Imam wa zama hizi! Sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yako na juu ya kizazi chako chema kitakasifu.

“Enyi mabwana zangu kuweni waombezi wangu katika kufuta mzigo wangu na makosa yangu. Nimemwamini Mwenyezi Mungu na yale yaliyoteremshwa kwenu. Namtawalisha wa mwisho wenu kama ninavyomtawalisha wa kwanza wenu. Na nimejitenga na sanamu na shetani, Lata na Uzza. Enyi mabwana zangu mimi ni mwenye amani na yule mwenye amani nanyi, na ni mwenye vita na yule mwenye vita nanyi, na ni adui wa yule mwenye uadui nanyi na ni mwenye mapenzi na yule mwenye mapenzi nanyi, mpaka Siku ya Kiyama. Mwenyezi Mungu awalaani waliokudhulumuni nyinyi na wakawaporeni nyinyi, na Mwenyezi Mungu awalaani wafuasi wao na wapambe wao na watu wa madhehebu yao, na ninajitenga nao kwa kujielekeza kwa Mwenyezi Mungu na kwenu nyinyi.”

Fadhila za kumzuru Husain (a.s.):

Miongoni mwa amali zilizopatikana katika siku hii ni kumzuru Husain (a.s.), nayo inalingana na Hijja elfu moja na Umra elfu moja na Jihadi mara elfu moja, bali ni zaidi ya hapo. Tambua kwamba kumzuru Husein na hali ukiwa mbali na Karbala kuna fadhila nyingi.

Ziyara ya Husein siku ya Arafa:

سُبْحَانَ اللَّهِ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ وَلَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَاللَّهُ أَكْبَرُ وَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيمِ، سُبْحَانَ اللَّهِ آنَاءَ اللَّيْلِ وَأَطْرَافَ النَّهَارِ، سُبْحَانَ اللَّهِ بِالْغُدُوِّ وَالاِصَالِ، سُبْحَانَ اللَّهِ بِالْعَشِيِّ وَالْأَبْكَارِ، سُبْحَانَ اللَّهِ حِينَ تُمْسُونَ وَحِينَ تُصْبِحُونَ وَلَهُ الْحَمْدُ فِي السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ وَعَشِيًّا وَحِينَ تُظْهِرُونَ، يُخْرِجُ الْحَمَّ مِنَ الْبَيْتِ وَيُخْرِجُ الْبَيْتَ مِنَ الْحَمَّ وَيُحْيِي الْأَرْضَ بَعْدَ مَوْتِهَا وَكَذِلِكَ تُخْرِجُونَ، سُبْحَانَ رَبِّكَ رَبِّ الْعِزَّةِ عَمَّا يَصِفُونَ وَسَلَامٌ عَلَى الْبُرْسَلِينَ وَالْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ، سُبْحَانَ ذِي الْبُلْكِ وَالْمَلَكُوتِ، سُبْحَانَ ذِي الْعِزَّةِ وَالْجَبَرُوتِ، سُبْحَانَ ذِي الْكِبْرِيَاءِ وَالْعَظَمَةِ الْمُلِكِ الْحَقِّ الْمُهَمَّينِ (الْمُبَيِّنِ) الْقُدُّوسِ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْمَلِكِ الْحَمِّ الَّذِي لَا يَمُوتُ، سُبْحَانَ اللَّهِ الْمَلِكِ

الْحَمْدُ لِلّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيمِ، سُبْحَانَ الْقَائِمِ الْدَّاعِمِ، سُبْحَانَ الدَّائِمِ الْقائمِ،
سُبْحَانَ رَبِّ الْعَظِيمِ، سُبْحَانَ رَبِّ الْأَعْلَى، سُبْحَانَ الْحَقِّ الْقَيُّومِ،
سُبْحَانَ الْعَلِيِّ الْأَعْلَى، سُبْحَانَهُ وَتَعَالٰى، سُبُّوْحٌ قُدُّوسٌ رَبُّنَا
وَرَبُّ الْبَلَائِكَةِ وَالرُّوحِ، سُبْحَانَ الدَّائِمِ غَيْرِ الْغَافِلِ، سُبْحَانَ
الْعَالَمِ بِغَيْرِ تَغْلِيمِ، سُبْحَانَ خالِقِ مَا يُرِيَ، وَمَا لَا يُرِي سُبْحَانَ
الَّذِي يُدْرِكُ الْأَبْصَارُ وَلَا تُدْرِكُهُ الْأَبْصَارُ وَهُوَ اللَّطِيفُ
الْخَبِيرُ، أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَصْبَحْتُ مِنْكَ فِي نِعْمَةٍ وَخَيْرٍ وَبَرَكَةٍ وَعَافِيَةٍ
فَصَلِّ عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ وَاتِّهِمْ عَلَى نِعْمَتِكَ وَخَيْرِكَ وَبَرَكَاتِكَ
وَعَافِيَاتِكَ بِنَجَاةٍ مِنَ النَّارِ، وَارْزُقْنِي شُكْرَكَ وَعَافِيَاتِكَ
وَفَضْلَكَ وَكَرَامَتِكَ أَبْدًا مَا أَبْغَيْتُنِي، أَللّٰهُمَّ بِنُورِكَ اهْتَدِيْتُ
وَبِفَضْلِكَ اسْتَغْنَيْتُ وَبِنِعْمَتِكَ أَصْبَحْتُ وَأَمْسَيْتُ، أَللّٰهُمَّ إِنِّي
أُشْهِدُكَ وَكَفِيْ بِكَ شَهِيدًا وَأُشْهِدُ مَلَائِكَتِكَ وَأَنْبِياءَكَ
وَرُسُلَكَ وَحَمَلَةَ عَرْشِكَ وَسُكَّانَ سَمَاوَاتِكَ وَأَرْضِكَ

(وَأَرْضِيكَ) وَجَيْعَ خَلْقِكَ بِأَنَّكَ أَنْتَ اللَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ وَحْدَكَ لَا
شَرِيكَ لَكَ وَأَنَّ مُحَمَّداً صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ عَبْدُكَ وَرَسُولُكَ
وَأَنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ، تُحْيِي وَتُمْيِتْ وَتُتَبَّعُ وَتُحْيَى وَآشَهَدُ
أَنَّ الْجَنَّةَ حَقٌّ وَأَنَّ النَّارَ حَقٌّ، وَ(أَنَّ) الْتُّشُورَ حَقٌّ، وَالسَّاعَةَ
اتِّيَّةً لَا رَيْبَ فِيهَا، وَأَنَّ اللَّهَ يَنْبَغِي مَنْ فِي الْقُبُورِ، وَآشَهُدُ أَنَّ عَلَيَّ
بْنَ آبِي طَالِبٍ أَمِيرِ الْمُؤْمِنِينَ حَقًا حَقًا، وَأَنَّ الْأُنْيَةَ مِنْ وُلْدَةِ هُمْ
الْأُنْيَةُ الْهُدَاةُ الْمَهْدِيُّونَ غَيْرُ الضَّالِّينَ وَلَا الْبُصِّلِينَ وَأَنَّهُمْ
أَوْلِيَاؤُكَ الْمُصْطَفَوْنَ وَحِزْبُكَ الْغَالِبُونَ وَصِفْوَتُكَ وَخِيرَتُكَ مِنْ
خَلْقِكَ وَنُجْبَاؤُكَ الَّذِينَ اتَّسْجَبْتَهُمْ لِدِينِكَ وَاخْتَصَصْتَهُمْ مِنْ
خَلْقِكَ، وَاصْطَفَيْتَهُمْ عَلَى عِبَادِكَ، وَجَعَلْتَهُمْ حُجَّةً عَلَى
الْعَالَمَيْنَ صَلَوَاتُكَ عَلَيْهِمْ وَالسَّلَامُ وَرَحْمَةُ اللَّهِ وَبَرَكَاتُهُ، أَللَّهُمَّ
اکْتُبْ لِي هَذِهِ الشَّهَادَةِ عِنْدَكَ حَتَّى تُلَقِّنِي هَا يَوْمَ الْقِيَامَةِ وَإِنَّ
عَنِّي راضٌ إِنَّكَ عَلَى مَا تَشَاءُ قَدِيرٌ، أَللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا

يَصْعُدُ أَوْلُهُ وَلَا يَنْفَدُ اخِرُهُ، أَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا تَضَعُ لَكَ
السَّمَاءُ كَنْفِيهَا (كَتْفِيهَا) وَتُسَبِّحُ لَكَ الْأَرْضُ وَمَنْ عَلَيْهَا،
أَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا سَمِّ مَدًّا أَبَدًا لَا انْقِطَاعَ لَهُ وَلَا نَفَادَ وَلَكَ
يَنْبَغِي وَإِلَيْكَ يَنْتَهِ فِي وَعَلَى وَلَدَى وَمَعِي وَقَبْلِي وَبَعْدِي
وَأَمَامِي وَفَوْقِي وَتَحْتِي وَإِذَا مِتْ وَبَقِيتُ فَرْدًا وَحِيدًا ثُمَّ فَنِيتُ،
وَلَكَ الْحَمْدُ إِذَا نُشِرتُ وَبُعْثِتُ يَا مَوْلَاي. أَللّٰهُمَّ وَلَكَ الْحَمْدُ
وَلَكَ الشُّكْرُ بِجَيِيعِ مَحَامِدِكَ كُلُّهَا عَلَى جَيِيعِ نَعْبَائِكَ كُلُّهَا
حَتَّى يَنْتَهِ الْحَمْدُ إِلَى مَا تُحِبُّ رَبَّنَا وَتَرْضَى، أَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ
عَلَى كُلِّ أَكْلَةٍ وَشِرَابَةٍ وَبَطْشَةٍ وَقَبْضَةٍ وَبَسْطَةٍ وَفِي كُلِّ مَوْضِعٍ
شَعْرَةٍ، أَللّٰهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا خَالِدًا مَعَ خُلُودِكَ وَلَكَ الْحَمْدُ
حَمْدًا لَا مُنْتَهِي لَهُ دُونَ عِلْمِكَ وَلَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا أَمْدَلَهُ دُونَ
مُشِيَّتِكَ، وَلَكَ الْحَمْدُ حَمْدًا لَا أَخْرَ لِقَاءِلِهِ إِلَّا رِضَاكَ وَلَكَ
الْحَمْدُ عَلَى حِلْمِكَ بَعْدَ عِلْمِكَ وَلَكَ الْحَمْدُ عَلَى عَفْكَ بَعْدَ

قُدْرَتِكَ وَلَكَ الْحَمْدُ بَايِعُثُ الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ وَارِثُ الْحَمْدُ
وَلَكَ الْحَمْدُ بَدِيعَ الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ مُنْتَهَى الْحَمْدِ وَلَكَ
الْحَمْدُ مُبْتَدِعَ الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ مُشْتَرِى الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ
وَلِيَّ الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ قَدِيمَ الْحَمْدِ وَلَكَ الْحَمْدُ صَادِقَ الْوَعْدِ
وَفِيَّ الْعَهْدِ عَزِيزَ الْجُنْدِيَّ قَائِمٌ إِلَّا مَجِيدٌ وَلَكَ الْحَمْدُ رَفِيعَ
الدَّرَجَاتِ مُجِيبَ الدَّعَوَاتِ مُنْزِلَ (مُنْزَلٍ) الْأَيَّاتِ مِنْ فَوْقِ
سَبْعِ سَيَّاَتِ عَظِيمَ الْبَرَكَاتِ مُخْرِجَ النُّورِ مِنَ الْطُّلُمَاتِ مَنِ فِي
الْطُّلُمَاتِ وَمُخْرِجٌ إِلَى النُّورِ، مُبَدِّلٌ السَّيِّئَاتِ حَسَنَاتِ، وَجَاعِلٌ
الْحَسَنَاتِ دَرَجَاتِ، أَللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ غَافِرُ الذَّنْبِ وَقَابِلُ
الْتَّوْبِ شَدِيدُ الْعِقَابِ ذَا الصَّوْلِ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ إِلَيْكَ الْبَصِيرُ،
أَللَّهُمَّ لَكَ الْحَمْدُ فِي الْلَّيْلِ إِذَا يَغْشَى، وَلَكَ الْحَمْدُ فِي النَّهَارِ إِذَا
تَجَلَّ، وَلَكَ الْحَمْدُ فِي الْأَخْرَى وَالْأُولَى، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ كُلِّ نَجْمٍ
وَمَلَكٍ فِي السَّمَاوَاتِ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ الْثَّرَى وَالْحَصَى وَالثَّوَى،

وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ مَا فِي جَوَافِ السَّمَاءِ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ مَا فِي جَوْفِ
 الْأَرْضِ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ أَوْزَانِ مِياهِ الْبِحَارِ، وَلَكَ الْحَمْدُ
 عَدَدَ أُوراقِ الْأَشْجَارِ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ مَا عَلَى وَجْهِ الْأَرْضِ،
 وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ مَا أَحْصَى كِتَابُكَ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ مَا أَحَاطَ
 بِهِ عِلْمُكَ، وَلَكَ الْحَمْدُ عَدَدَ الْإِنْسِينَ وَالْجِنِّ وَالْهَوَامِ وَالْطَّيْرِ
 وَالْبَهَائِمِ وَالسَّبَاعِ، حَمْدًا كَثِيرًا طَيْبًا مُبَارِكًا فِيهِ كَمَا تُحِبُّ
 رَبَّنَا وَتَرْضِي، وَكَمَا يُبَغِّنِي لِكَمِ وَجْهُكَ وَعِزِّ جَلَالِكَ.

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu. Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu, kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, na hakuna mungu ila Allah, Mwenyezi Mungu Mkubwa na hakuna hila wala nguvu ila kwa msada wa Mwenyezi Mungu Aali Adhimu. Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu nyakati za usiku na katikati ya mchana. Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu asubuhi na jioni. Utukufu ni wa Mwenyezi Mungu jioni na asubuhi. Basi mtukuzeni Mwenyezi Mungu mnapoingia usiku na mnapoingia asubuhi. Na sifa zote njema ni Zake mbinguni na ardhini, na wakati wa alasiri na mnapoingia adhuhuri. Hukitoa kilicho hai kutokana na kilicho kufa, na hukitoa kilichokufa kutokana na kilicho hai, na huhuisha ardhii baada ya kufa kwake na hivyo ndivyo mtakavyotolewa. Ametakasika Mola Wako Mlezi, Mola Mlezi Mwenye enzi na yale wanayomsifu. Na amani juu ya

wale waliotumwa. Na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa walimwengu. Utukufu ni wa Mwenye umiliki na ufalme. Utakatifu ni wa Mwenye nguvu na ujabari.

“Utakatifu ni wa Mwenye kiburi na uadhama. Mfalme Haki iliyo wazi, Mwangalizi, Mwenye nguvu, Mtakatifu. Utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu Mfalme Mzima wa milele asiyekufa. Utakatifu ni wa Mwenyezi Mungu, Mfalme, Mzima wa milele Mtakatifu. Utakatifu ni wa Msimamizi Mwenye kudumu. Utakatifu ni wa Mwenye kudumu aliye Msimamizi. Utakatifu ni wa Mola Wangu Mlezi Adhimu. Utakatifu ni wa Mola Wangu Mlezi Mtukufu. Utakatifu ni wa aliye Mzima wa milele Mwenye kusimamia mambo. Utakatifu ni wa Aliye juu, Mtukufu. Utakatifu ni Wake na ametakasika. Mtakatifu Mtukufu, Mola Wetu Mlezi na Mola Mlezi wa Malaika na roho. Utakatifu ni wa Mwenye kudumu asiyeghafilika. Utakatifu ni wa Mjuzi bila kufundishwa. Utakatifu ni wa Muumba wa vinavyoonekana na visivyoonekana. Utakatifu ni wa Ambaye huyafikia macho wala macho hayamfikii, Naye ni Mpole, Mwenye habari.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi nimeamka katika hali ya neema, heri, baraka na afya toka Kwako, basi mswalie Muhammad na aali Muhammad na nitimizie neema Yako, heri Yako, Baraka Yako na afya Yako kwa kuniokoa na moto. Na niruzuku shukrani Yako, afya Yako, fadhila Yako na heshima Yako muda wote utakaonibakisha hai. Ewe Mwenyezi Mungu! Nimeongoka kuitia nuru Yako, nimetosheka kuitia fadhila Yako na kwa kuitia neema Yako nimeingia asubuhi na machana.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Mimi nakushahidilisha Wewe na unatosha kuwa shahidi, na nawashahidilisha Malaika

Wako, Manabii Wako, Mitume Wako, wabebaji wa Arshi Yako, wakazi wa mbingu Zako na ardhi Zako, na viumbe Wako wote, kwamba hakika Wewe ndiye Mwenyezi Mungu ambaye hakuna mungu ila Wewe Mmoja peke Yako hauna mshirika, na kwamba hakika Muhammad (s.a.w.w.) ni mja Wako na Mtume Wako, na kwamba hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu. Unahuisha na unafisha, unafisha na unahuisha. Na ninakiri kwamba hakika pepo ni haki na hakika moto ni haki, na hakika ufufuo ni haki, na kwamba hakuna shaka Kiyama ni chenye kuja, na kwamba hakika Mwenyezi Mungu atawafufua waliyomo makaburini.

“Na ninakiri kwamba ni haki kabisa kuwa Ali bin Abu Talib (a.s.) ni jemedari wa waumini, na kwamba hakika maimamu toka katika kizazi chake ndio Maimamu waongofu wenyе kuongoa, si wenyе kupotea wala kupoteza. Na kwamba hakika wao ndio mawalii wako wateule na kundi Lako lenye kushinda, wateule Wako na chaguo Lako bora toka kati ya viumbe Wako, na wateule Wako ambaо umewateua kwa ajili ya dini Yako na ukawafanya makhsusi kati ya viumbe Wako, na ukawachagua juu ya waja Wako na ukawafanya hoja juu ya walimwengu, sala na salamu Zako viwe juu yao, na pia rehemza Mwenyezi Mungu na Baraka Zake.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Niandikie shahada hii Kwako mpaka utakaponitamkisha siku ya Kiyama na hali Wewe u radhi nami. Hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya lile utakalo. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema, sifa njema ambayo mwanzo wake unapanda wala mwisho wake hauishi. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema, sifa njema ambayo mbingu inashusha mbawa zake kwa ajili Yako, na ardhi na vilivyo juu yake vinasabihi kwa ajili

Yako.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema, sifa njema ya daima milele, haina kukatika wala kwisha na inakupasa Wewe. Na Kwako ndiko kinakokomea kile kilicho kwangu, juu yangu, katika miliki yangu, pamoja nami, kabla yangu, baada yangu, mbele yangu, juu yangu, chini yangu, nitakapokufa na nitakapoingizwa kaburini na kubaki mpweke peke yangu kisha nikaisha. Na una sifa njema pale nitakapofufuliwa Ewe Bwana Wangu. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema na shukurani ni Yako kwa himidi Zako zote juu ya neema Zako zote mpaka himidi ikomee kwenye yale unayoyapenda Ewe Mola Wetu Mlezi na unayoyeridhia. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema juu ya kila chakula na kinywaji, nguvu, ufumbaji na uumbuaji wa mkono na katika kila eneo lenye unywele.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema, sifa njema yenye kudumu pamoja na kudumu Kwako. Na Una sifa njema, sifa njema haina mwisho bila elimu Yako. Na Una sifa njema, sifa njema isiyo na muda bila utashi Wako. Na Una sifa njema, sifa njema isiyo na malipo ya kukutana nayo ila ridhaa Yako. Una sifa njema juu ya uvumilivu Wako baada ya elimu Yako. Una sifa njema juu ya msamaha Wako baada ya uwezo Wako. Una sifa njema Mwenye kuleta himidi. Una sifa njema Mwenye kurithisha himidi. Una sifa njema Mwenye kuumba himidi. Una sifa njema kikomo cha sifa njema.

“Una sifa njema mwenye kuanzisha himidi. Una sifa njema Mwenye kununua himidi. Una sifa njema Mmiliki wa himidi. Una sifa njema Mwenye himidi tangu kale. Una sifa njema Mkweli wa ahadi na Mtekelezaji wa ahadi, Mwenye jeshi lenye nguvu na Mwenye utukufu wenye kuendelea. Una sifa njema Mwenye daraja za juu, Mwenye

kujibu maombi, Mwenye kuteremsha aya toka juu ya mbingu saba, Mwenye Baraka kubwa, Mwenye kutoa nuru toka kwenye giza na Mwenye kumtoa aliye katika giza na kumpekeka kwenye nuru, Mwenye kuyabadili maovu kuwa mema na kuyaweka mema katika daraja mbalimbali.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema, Mwenye kughufiri dhambi, Mwenye kupokea toba, Mkali wa adhabu, Mwenye nguvu, hakuna mungu ila Wewe, mafikio ni Kwako. Ewe Mwenyezi Mungu! Una sifa njema usiku unapofunika na una sifa njema mchana unapoangaza. Una sifa njema Akhera na duniani. Una sifa njema kwa idadi ya kila nyota na malaika aliyopo mbinguni. Una sifa njema kwa idadi ya udongo na changarawe na kokwa. Una sifa njema kwa idadi ya vilivyomo katika angahewa la mbingu. Una sifa njema kwa idadi ya vilivyomo ndani ya tumbo la ardhi.

“Una sifa njema kwa idadi ya ujazo wa maji ya bahari. Una sifa njema kwa idadi ya majani ya miti. Una sifa njema kwa idadi ya vile vilivyopo juu ya uso wa ardhi. Sifa njema kwa idadi ya vile vilivyo hesabiwa na Kitabu Chako. Una sifa njema kwa idadi ya vile vilivyzungukwa na elimu Yako. Una sifa njema kwa idadi ya watu na majini, wadudu, ndege, wanyama howa na wanyama wakali, sifa njema nyingi nzuri zeny Baraka, kama upendavyo Ewe Mola Wetu Mlezi na uridhiavyo, na kama inavyolingana na heshima ya utukufu Wako na utukufu wa utakatifu Wako.”

Kisha utasema mara kumi:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْحُكْمُ وَهُوَ

اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ

“Hakuna mungu ila Allah peke Yake hana mshirika, ana ufalme na himidi na Yeye ni Mpole Mwenye khabari.”

Mara kumi:

لَا إِلَهَ إِلَّا اللَّهُ وَحْدَهُ لَا شَرِيكَ لَهُ، لَهُ الْمُلْكُ وَلَهُ الْحَمْدُ يُحْيِي
وَيُمْتَنِعُ وَيُبَيِّنُ وَيُحْيِي وَهُوَ حَقٌّ لَا يَمُوتُ بِيَدِهِ الْخَيْرُ وَهُوَ عَلَى كُلِّ
شَيْءٍ قَدِيرٌ

“Hakuna mungu ila Allah peke Yake hana mshirika, ana ufalme na himidi, huhuisha na kufisha, hufisha na kuhuisha, Naye ni Mzima wa milele asiyekufa, heri imo mikononi Mwake na Yeye ni Mwenye uwezo juu ya kila kitu.”

Mara kumi:

أَسْتَغْفِرُ اللَّهَ الَّذِي لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ الْحَمْدُ لِلْقَيْوَمِ وَأَتُوبُ إِلَيْهِ

Namuomba maghfira Mwenyezi Mungu ambaye hakuna mungu ila Yeye Mzima wa milele Mwenye kusimamia mambo, na ninatubu Kwake.

Mara kumi:

يَا أَللّٰهُ يَا أَللّٰهُ،

“Ewe Mwenyezi Mungu. Ewe Mwenyezi Mungu.”

Mara kumi:

يَا رَحْمٌ يَا رَحْمٌ

“Ewe Mwingi wa rehema. Ewe Mwingi wa rehema.”.

Mara kumi:

يَا رَحِيمٌ يَا رَحِيمٌ

“Ewe Mwenye kurehemu. Ewe Mwenye kurehemu.”

Mara kumi:

يَا بَدِيعُ السَّمَاوَاتِ وَالْأَرْضِ

“Ewe Muumba wa mbingu na ardhi.”

Mara kumi:

يَا ذَا الْجَلَلِ وَالْكَرَمِ

“Ewe Mwenye utukufu na ukarimu.”

Mara kumi:

يَا حَنَانُ يَا مَنَانُ

“Ewe Mwenye huruma, ewe Mwenye hisani.”

Mara kumi:

يَا حَمْ يَا قَيْوُمْ

“Ewe Mzima wa milele, ewe Mwenye kusimamia mambo.”

Mara kumi:

يَا حَمْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

“Ewe Mzima wa milele, hakuna mungu ila Wewe.”

Mara kumi:

يَا أَللَّهُ يَا لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ

“Ewe Mwenyezi Mungu, hakuna mungu ila Wewe.”

Mara kumi:

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema Mwenye kurehemu.”

Mara kumi:

اللّٰهُمَّ صَلِّ عَلٰى مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ

“Ewe Mwenyezi Mungu mswalie Muhammad na aali Muhammad.”

Mara kumi:

اللّٰهُمَّ اغْفِلْ بِي مَا أَنْتَ أَهْلُهُ

“Ewe Mwenyezi Mungu nifanyie yale unayoyataka.”

Mara kumi:

آمِينَ آمِينَ

“Amina. Amina.”

Mara kumi:

قُلْ هُوَ اللّٰهُ أَحَدٌ

“Sema Yeye Mwenyezi Mungu ni Mmoja.”

Baada ya hapo sema:

أَللّٰهُمَّ اصْنَعْ بِي مَا أَنْتَ أَهْلُهُ وَلَا تَصْنَعْ بِي مَا أَنَا أَهْلُهُ فَإِنَّكَ أَهْلُ
 التَّقْوٰ وَأَهْلُ الْغُفْرٰةِ، وَأَنَا أَهْلُ الذُّنُوبِ وَالْخَطَايا فَارْحَنْي يَا
 مَوْلَائِي وَأَنْتَ أَرْحَمُ الرَّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nifanyie yale ambayo Wewe unataka na wala usinifanyie yale niyatakayo mimi, kwani hakika Wewe ndiye unayestahiki uchaji na ndiye Mmiliki wa maghfira, na mimi ndiye mwenye madhambi na makosa, basi nirehemu Ewe Bwana Wangu na Wewe ni Mwenye kurehemu kushinda wote wenyе kurehemu.”

Kisha sema mara kumi:

لَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللّٰهِ تَوَكَّلْتُ عَلَى الْحَمِّ الَّذِي لَا يَءُوتُ وَالْحَمْدُ
 لِلّٰهِ الَّذِي لَمْ يَتَخَذْ وَلَدًا وَلَمْ يَكُنْ لَهُ شَيْئٌ فِي الْبُلْكِ وَلَمْ يَكُنْ لَهُ
 وَلِيًّا مِنَ الدُّلُّ وَكَبِيرٌ تَكْبِيرًا

“Hakuna hila wala nguvu ila kwa msaada wa Mwenyezi Mungu. Nimetawakali juu ya Mzima wa milele ambaye hafi, na kila sifa njema ni ya Mwenyezi Mungu ambaye hakujifanya mtoto wala hana mshirika katika ufalme, wala hana rafiki kwa sababu ya udhaifu, na mtukuze kwa matukuzo makubwa.””

Ziyara ya Imam wa Zama hizi:

Ibnu Tawus amesema: Maulana Imam wa zama hizi hufanyiwa ziara kwa ziyara hii kila siku ya Ijumaa baada ya sala ya alfajiri:

اللَّهُمَّ بِدِلْغٍ مَوْلَائِي صَاحِبَ الزَّمَانِ صَلَوَاتُ اللَّهِ عَلَيْهِ عَنْ جَمِيعِ
الْبُؤْمِنِينَ وَالْبُؤْمِنَاتِ فِي مَشَارِقِ الْأَرْضِ وَمَعَارِبِهَا وَبَرِّهَا وَ
بَحْرِهَا وَسَهْلِهَا وَجَبَلِهَا حَيْثِمْ وَمَيْتِهِمْ وَعَنْ وَالِدَائِي وَوُلْدِي وَ
عَنِّي مِنَ الصَّلَواتِ وَالشَّهِيَّاتِ زِنَةَ عَرْشِ اللَّهِ وَمِدَادَ كَلِمَاتِهِ وَ
مُنْتَهَى رِضَاهُ وَعَدَدَ مَا أَحْصَاهُ كِتَابُهُ وَأَحَاطَ بِهِ عِلْمُهُ اللَّهُمَّ
(إِنِّي) أُجَدِّدُ لَهُ فِي هَذَا الْيَوْمِ وَفِي كُلِّ يَوْمٍ عَهْدًا وَعَقْدًا وَبِيَعْتَةً فِي
رَقْبَتِي اللَّهُمَّ كَمَا شَرَّفْتِنِي بِهَذَا الشَّهِيْفِ وَفَضَّلْتِنِي بِهَذِهِ
الْفَضِيلَةِ وَخَصَّصْتِنِي بِهَذِهِ النِّعْمَةِ فَصَلَّى عَلَى مَوْلَائِي وَسَيِّدِي
صَاحِبِ الزَّمَانِ وَاجْعَلْنِي مِنْ أَنْصَارِهِ وَأَشْيَاعِهِ وَالْذَّاهِبِينَ عَنْهُ
وَاجْعَلْنِي مِنَ الْمُسْتَشْهَدِينَ بَيْنَ يَدِيهِ طَائِعاً غَيْرَ مُكْرِهٍ فِي
الصَّفِ الَّذِي نَعْتَ أَهْلَهُ فِي كِتَابِكَ فَقُلْتَ صَفَّاً كَأَنَّهُمْ بِنِيَّانٍ

مَرْسُومٌ عَلَى طَاعَتِكَ وَ طَاعَةِ رَسُولِكَ وَ آلِهِ عَلَيْهِمُ السَّلَامُ

اللَّهُمَّ هَذِهِ بَيْعَةٌ لَهُ فِي عُنْقِي إِلَى يَوْمِ الْقِيَامَةِ

“Ewe Mwenyezi Mungu! Mfikishie bwana wangu Imam wa zama hizi, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake, kutoka kwa waumini wote wa kiume na waumini wote wa kike, walio Mashariki ya ardhi na Magharibi yake, bara yake na bahari yake, katika tambarare yake na milima yake, kutoka kwa aliye hai kati yao na aliye mfu kati yao, kutoka kwa wazazi wangu na kizazi changu na kutoka kwangu, sala na maamkizi sawa na uzito wa Arshi ya Mwenyezi Mungu, wino wa maneno Yake na ukomo wa ridhaa Yake, na sawa na idadi ya vile vilivyohesabiwa na Kitabu Chake na kudhibitiwa na elimu Yake. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi narudia tena katika siku hii na katika kila siku ahadi, mkataba na kiapo cha utii katika shingo yangu.

Ewe Mwenyezi Mungu! Kama ulivyonipa heshima kwa heshima hii na ukani fadhilisha kwa fadhila hii na ukani husisha na neema hii, basi mswalie kiongozi wangu na bwana wangu Imam wa zama hizi, na unijaalie niwe mionganoni mwa wasaidizi wake, wafuasi wake na wenye kumuhami yeye. Na nijaalie niwe mionganoni mwa wenye kufa kishahidi mbele yake, mwenye kutii asiyelazimishwa, katika safu ambayo umewasifu watu wake katika Kitabu Chako, ukasema: Safu kama jengo lililokamatana, katika kukutii Wewe na kumtii Mtume Wako na aali zake (a.s.). Ewe Mwenyezi Mungu! Hiki ni kiapo changu cha utii kwake katika shingo yangu mpaka Siku ya Kiyama.”

DUA AL-'AHAD

Imepokewa kutoka kwa Imam as-Sadiq (a.s.) kwamba alisema: "Atakayemuomba Mwenyezi Mungu kwa Ahadi hii kwa muda wa siku arobaini basi atakuwa mionganoni mwa watetezi wa Mahdi wetu, na iwapo atakuufa kabla yake basi Mwenyezi Mungu atamtoa ndani ya kaburi lake na kumpa kwa kila neno moja mema elfu moja na atamfutia mabaya elfu moja." Dua yenyewe ni hii:

أَللّٰهُمَّ رَبَّ الْعُوْدِ الْعَظِيْمِ، وَرَبَّ الْكُنْسِيِّ الرَّفِيْعِ، وَرَبَّ الْبَحْرِ
الْمُسْجُورِ، وَمُنْزِلِ التَّوْرَاةِ وَالْإِنْجِيلِ وَالرَّبُورِ، وَرَبَّ الظَّلِّ
وَالْحَمْوَرِ، وَمُنْزِلِ الْقُرْآنِ الْعَظِيْمِ، وَرَبَّ الْمَلَائِكَةِ الْمُقَرَّبِيْنَ
وَالْأَنْبِيَاءِ وَالرُّسُلِيْنَ، أَللّٰهُمَّ إِنِّي أَسْأَلُكَ بِإِسْمِكَ الْكَرِيمِ،
وَبِنُورِ وَجْهِكَ الْمُنْيِرِ وَمُلْكِكَ الْقَدِيمِ، يَا حَمْ يَا قَيْوُمْ أَسْأَلُكَ
بِإِسْمِكَ الَّذِي أَشَرَّقْتُ بِهِ السَّيَاوَاتْ وَالْأَرْضُونَ، وَبِإِسْمِكَ
الَّذِي يَصْلَحُ بِهِ الْأَكْلُونَ وَالْأَخْرُونَ، يَا حَيَا قَبْلَ كُلِّ حَيٍّ وَيَا حَيَا
بَعْدَ كُلِّ حَيٍّ وَيَا حَيَا حِينَ لَا حَيٍّ يَا مُحْيِي الْمَوْتَى وَمُمِيتِ الْأَحْيَاءِ،
يَا حَمْ لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ، أَللّٰهُمَّ بَلِّغْ مَوْلَانَا الْأَمَامَ الْهَادِي الْمَهْدِيَّ

الْقَائِمِ بِأَمْرِكَ صَلَواتُ اللَّهِ عَلَيْهِ وَعَلَى آبَائِهِ الظَّاهِرِينَ عَنْ
جَمِيعِ الْمُؤْمِنِينَ وَالْمُؤْمِنَاتِ فِي مَشَارِقِ الْأَرْضِ
وَمَغَارِبِهَا سَهْلَهَا وَجَبَلَهَا وَبَرِّهَا، وَعَنِّي وَعَنْ وَالدَّى
مِنَ الصَّلَواتِ زِنَةَ عَرْشِ اللَّهِ وَمِدَادَ كَلِباتِهِ، وَمَا أَحْصَاهُ عَلَيْهِ
وَاحْاطَ بِهِ كِتَابُهُ، أَللَّهُمَّ إِنِّي أَجَدِدُ لَهُ فِي صَبِيحةِ يَوْمِ هَذَا وَمَا
عَشْتُ مِنْ آيَاتِكَ عَهْدًا وَعَقْدًا وَبَيْعَةً لَهُ فِي عُنْقِي، لَا أَحُولُ عَنْهَا
وَلَا أَزُولُ أَبَدًا، أَللَّهُمَّ اجْعَلْنِي مِنْ أَنْصَارِهِ وَأَعْوَانِهِ وَالْذَّابِيْنَ
عَنْهُ وَالْمُسَارِعِينَ إِلَيْهِ فِي قَضَاءِ حَوَائِجهِ، وَالْمُسْتَشِدِينَ لِأَوْامِرِهِ
وَالْمُحَامِيْنَ عَنْهُ، وَالسَّابِقِيْنَ إِلَى إِرَادَتِهِ وَالْمُسْتَشْهِدِيْنَ
بَيْنَ يَدِيْهِ، أَللَّهُمَّ إِنْ حَالَ بَيْنِي وَبَيْنَهُ الْبُوتُ الَّذِي جَعَلْتَهُ عَلَى
عِبَادِكَ حَثِيًّا مَقْضِيًّا فَأَخْرِجْنِي مِنْ قَبْرِي مُؤْتَزِرًا كَفَنِي شَاهِرًا
سَيْفِي مُجَرِّدًا قَنَاقِي مُلَبِّيًّا دَعْوَةَ الدَّاعِ فِي الْحَاضِرِ وَالْبَادِي،
أَللَّهُمَّ أَرِنِي الطَّلْعَةَ الرَّشِيدَةَ، وَالْغُرَّةَ الْحَبِيدَةَ، وَأَكْحُلْ نَاظِرِي

بِنَظْرَةٍ مِنْ إِلَيْهِ، وَعَجِّلُ فَرَجَهُ وَسَهَّلُ مَحْرَجَهُ، وَأُوْسِعْ مَنْهَاجَهُ
وَاسْلُكْ بِمَحَجَّتَهُ، وَانْفُدْ أَمْرَهُ وَاشْدُدْ أَزْرَهُ،
وَاعْمِرِ اللَّهُمَّ بِهِ بِلَادَكَ، وَأَحْبِي بِهِ عِبَادَكَ، فَإِنَّكَ قُلْتَ وَقَوْلُكَ
الْحَقُّ : ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ أَيْدِي النَّاسِ،
فَأَظْهِرِ اللَّهُمَّ لَنَا وَلِيَّكَ وَابْنَ بِنْتِ نَبِيِّكَ الْمُسَيْبِيِّ بِاسْمِ رَسُولِكَ
حَتَّى لا يَظْفَرَ بِشَيْءٍ مِنَ الْبَاطِلِ إِلَّا مَزَقَهُ، وَيُحَقَّ الْحَقُّ
وَيُحَقِّقَهُ، وَاجْعَلْهُ اللَّهُمَّ مَفْرَعًا لِيَظْلُومِ عِبَادَكَ، وَنَاصِرًا لِمَنْ لَا
يَجِدُ لَهُ نَاصِرًا غَيْرِكَ، وَمُجَدِّدًا لِهَا عُطَّلَ مِنْ أَحْكَامِ كِتابِكَ،
وَمُشَيْدًا لِهَا وَرَدَ مِنْ أَعْلَامِ دِينِكَ وَسُنْنَ نَبِيِّكَ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ
وَآلِهِ، وَاجْعَلْهُ اللَّهُمَّ مِنْ حَصَنَتَهُ مِنْ بَأْسِ الْمُعْتَدِينَ،
اللَّهُمَّ وَسَرِّ نَبِيِّكَ مُحَمَّدًا صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَآلِهِ بِرُوْتَتِهِ وَمَنْ
تَبِعَهُ عَلَى دَعْوَتِهِ، وَارْحِمْ اسْتِكَانَتَنا بَعْدَهُ، أَلَّهُمَّ اكْشِفْ
هَذِهِ الْغُبَّةَ عَنْ هَذِهِ الْأُمَّةِ بِحُضُورِهِ، وَعَجِّلْ لَنَا ظُهُورَهُ، إِنَّهُمْ

يَرَوْنَهُ بَعِيدًا وَنَرَاهُ قَرِيبًا، بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرّاحِمِينَ

“Ewe Mwenyezi Mungu Mola Mlezi wa nuru adhimu na Mola Mlezi wa elimu ya juu na Mola Mlezi wa bahari iliojazwa. Uliyeiteremsha Taurati na Injili na Zaburi na Mola Mlezi wa kivuli na joto. Uliyeiteremsha Qur’ani tukufu na Mola Mlezi wa Malaika waliowekwa karibu na wa Manabii na Mitume. Ewe Mwenyezi Mungu hakika mimi nakuomba kwa heshima Yako tukufu na kwa nuru ya heshima Yako itowayo nuru na ufalme wa tangu kale, Ewe Mzima wa milele! Ewe Mwenyekusimamia mambo! Nakuomba kwa jina Lako ambalo umeangaza kwalo mbingu na ardhi, na kwa jina Lako ambalo kwalo wanatengemaa wale wa mwanzo na wale wa mwisho. Ewe Uliyekuwa Mzima wa milele kabla ya kila aliye hai! Na Ewe utakayeendelea kuwa Mzima wa milele baada ya kila aliye hai! Ewe Mzima wa milele pasipo na aliye hai! Ewe Mwenye kuwapa uzima wafu na kuwafisha walio hai! Ewe Mzima wa milele hakuna mungu ila Wewe.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Mfikishie kiongozi wetu Imam mwenye kuongoza aliye mwongozo, mwenye kusimamia jambo Lako, sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu yake na juu ya baba zake watakasifu, kutoka kwa waumini wote wa kiume na waumini wote wa kike, walio Mashariki ya ardhi na Magharibi yake, katika tambarare yake na milima yake, bara yake na bahari yake, kutoka kwangu na kwa wazazi wangu, sala na maamkizi sawa na uzito wa Arshi ya Mwenyezi Mungu na wino wa maneno Yake, na sawa na idadi ya vile vilivyohesabiwa na elimu Yake na kudhibitiwa na Kitabu Chake. Ewe Mwenyezi Mungu! Hakika mimi narudia tena katika asubuhi ya siku hii na katika siku zote za maisha yangu, ahadi, mkataba na kiapo

cha utii katika shingo yangu, sijitengi navyo wala siviachi milele.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nijaalie niwe mionganini mwa wasaidizi wake, wafuasi wake, wenyenye kumhami yeye na wenyenye kuharakisha kwenda kwake kumtimizia haja yake, na niwe mionganini mwa wenyenye kutekeleza amri yake, wenyenye kumhami yeye, wenyenye kutangulia katika muradi wake na wenyenye kufa kishahidi mbele yake. Ewe Mwenyezi Mungu! Ikiwa kifo ambacho umekifanya kuwa ni hatima yenye kutimia kitazuia kati yangu na yeye, basi unitoe kaburini mwangu hali ni mwenye kujifunika sanda yangu, mwenye kuchomoa upanga wangu, mwenye kuchomoa mkuki wangu na mwenye kuitikia wito wa mwenye kuita mjini na jangwani.

“Ewe Mwenyezi Mungu! Nionyeshe paji la uso wenyenye kuongoza, na mwezi wenyenye utukufu, na yang’arishe macho yangu kwa mtazamo wangu kwake, iharakishe faraja yake na mrahisishie matokeo yake, panua njia yake na nipiitishe njia yake, tekeleza jambo lake na mtie nguvu. Na amirisha Ewe Mwenyezi Mungu nchi Yako kupidia kwake na wahuishe waja Wako, kwani hakika Wewe umesema na kauli Yako ni haki tupu: Uharibifu umedhihiri barani na baharini kwa sababu ya yale iliyoyafanya mikono ya watu. Basi tudhihirishe Walii Wako na mwana wa binti ya Nabii Wako anayeitwa kwa jina la Mtume Wako, mpaka asikute kitu cha batili ila akichanechane, ahakikishe haki na kuitimiza.

“Na mjaalie Ewe Mwenyezi Mungu awe kimbilio la mwenye kudhulumiwa na waja Wako, mtetezi wa asiye na mtetezi mwininge asiyekuwa Wewe, mwenye kuhuisha zile hukumu za Kitabu Chako zilizotelekezwa, na mwenye kuimarisha zile sayansi za dini Yako zilizofundishwa na

zile Sunnah za Nabii Wako (s.a.w.w.). Na mjaalie Ewe Mwenyezi Mungu awe mionganini mwa uliowalinda na ubaya wa wapinduka mipaka. Ewe Mwenyezi Mungu! Mfurahishe Nabii Wako Muhammad (s.a.w.w.) kwa kumuona yeye na yule aliyefuata wito wake, na urehemu umasikini wetu baada yake. Ewe Mwenyezi Mungu! Ondo simanzi hii toka katika umma huu kwa kuhudhuria kwake, na tuharakishie kudhihiri kwake, hakika wao wanakuona uko mbali nasi tunakuona uko karibu. Kwa rehema Zako Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu.”

Kisha piga mara tatu juu ya paja lako la kulia kwa mkono wako, na katika kila mara sema:

الْعَجَلُ الْعَجَلُ يَا مَوْلَايَ يَا صَاحِبَ الزَّمَانِ

“Fanya haraka, fanya haraka Ewe Bwana Wangu Imam wa zama hizi.”

DUA YA ASUBUHI YA AMIRUL-MUUMININA (A.S.)

اللَّهُمَّ يَا مَنْ دَلَعَ لِسَانَ الصَّبَاحِ بِنُطْقٍ تَبَلُّجِهِ، وَسَرَّأَ حَقِطَاعَ
اللَّيْلِ الْمُظْلِمِ بِغَيَاهِ تَلَجُّلِهِ، وَأَتْقَنَ صُنْعَ الْفَلَكِ الدَّوَارِ
فِي مَقَادِيرِ تَبَرُّجِهِ، وَشَعْشَعَ ضِيَاءَ الشَّمْسِ بِنُورِ تَاجِجِهِ، يَا مَنْ
دَلَّ عَلَى ذَاتِهِ بِذَاتِهِ وَتَنَزَّأَ عَنْ مُجَانَسَةِ مَخْلُوقَاتِهِ وَجَلَّ عَنْ

مُلَاءَمَةٌ كَيْفِيَّاتِهِ، يَا مَنْ قَرِبَ مِنْ خَطَّارَتِ الظُّنُونِ وَبَعْدَ عَنْ
لَحَظَاتِ الْعَيْنِ وَعِلْمِ بِسَاكَانَ قَبْلَ أَنْ يَكُونَ، يَا مَنْ أَرْقَدَنِ فِي
مِهَادِ أَمْنِيهِ وَأَمَايِهِ وَأَيْقَظَنِي إِلَى مَا مَنَحَنِي بِهِ مِنْ مَنِيَّهِ
وَإِحْسَانِهِ وَكَفَ أَكْفَ السُّوءَ عَنِي بِيَدِهِ وَسُلْطَانِهِ، صَلِّ اللَّهُمَّ
عَلَى الدَّلِيلِ إِلَيْكَ فِي اللَّيْلِ الْأَلَيْلِ، وَالْمَاسِكِ مِنْ آسِبَابِكَ
بِحَبْلِ الشَّرَفِ الْأَطْوَلِ، وَالنَّاصِعِ الْحَسِبِ فِي ذُرُورَةِ الْكَاهِلِ
الْأَعْبَلِ، وَالثَّابِتِ الْقَدَمِ عَلَى زَحَالِيفِهَا فِي الزَّمَنِ الْأَوَّلِ، وَعَلَى
آلِهِ الْأَخْيَارِ الْمُصْطَفَيْنِ الْأَبْرَارِ، وَافْتَحْ اللَّهُمَّ لَنَا مَصَارِيعَ
الصَّبَاحِ بِسَفَاتِيْحِ الرَّحْمَةِ وَالْفَلَاحِ، وَأَلْبِسْنِي اللَّهُمَّ مِنْ أَفْضَلِ
خِلْعِ الْهِدَايَةِ وَالصَّلَاحِ، وَأَغْرِسِ اللَّهُمَّ بِعَظَمَتِكَ فِي شَرْبِ جَنَانِ
يَنَابِيعِ الْخُشُوعِ، وَأَجْرِ اللَّهُمَّ لِهَيْبَتِكَ مِنْ امْرَاقِ زَفَرَاتِ
الدُّمُوعِ، وَأَدِبِ اللَّهُمَّ نَزَقَ الْخُنُقَ مِنِّي بِأَزْمَمَةِ الْقُنُوْعِ، إِلَهِي
إِنْ لَمْ تَبْتَدِئْنِي الرَّحْمَةُ مِنْكَ بِحُسْنِ التَّوْفِيقِ فَمَنِ السَّالِكُ بِ

إِلَيْكَ فِي وَاضِحِ الطَّرِيقِ، وَإِنْ أَسْلَمْتُنِي أَنَا تُكَلِّفُ لِقَاءِ الْأَمْلِ
 وَالْمُنْفِي فَسِنِ الْبُقِيلُ عَثَرَاتِي مِنْ كَبُوْا الْهَوَى، وَإِنْ خَدَلَنِي
 نَصْرَكَ عِنْدَ مُحَارَبَةِ النَّفْسِ وَالشَّيْطَانِ فَقَدْ وَكَنِي خِذْلَانِكَ
 إِلَى حَيْثُ النَّصْبُ وَالْحِرْمَانُ، إِلَهِ آتَرَانِ ما آتَيْتُكَ إِلَّا مِنْ
 حَيْثُ الْأُمَالِ أَمْ عَلِقْتُ بِأَطْرَافِ حِبَالِكَ إِلَّا حِينَ بَاعَدْتُنِي ذُنُوبِي
 عَنْ دَارِ الْوِصَالِ، فَبِئْسَ الْبِطِيْهُ الَّتِي امْتَظَثَتْ نَفْسِي مِنْ هَوَاهَا
 فَوَاهَا لَهَا لِبَا سَوَّلَتْ لَهَا ظُنُونُهَا وَمُنْهَا، وَتَبَّأَلَهَا لِجُرَأَتِهَا عَلَى
 سَيِّدِهَا وَمَوْلَاهَا إِلَهِ قَرْعَتْ بَابَ رَحْمَتِكَ بِيَدِ رَجَائِي وَهَرَبَتْ
 إِلَيْكَ لاجِئًا مِنْ فَرَطِ أَهْوَائِي، وَعَلِقْتُ بِأَطْرَافِ حِبَالِكَ أَنَامِلَ
 وَلَائِي، فَاصْفَحِ اللَّهُمَّ عَمَّا كُنْتُ (كَانَ) أَجْرَمُتْهُ مِنْ زَلَّى
 وَخَطَائِي، وَأَقْلَنِي مِنْ صَرْعَةِ رِدَائِي فِيَكَ سَيِّدِي وَمَوْلَايِ
 وَمُعْتَبِدِي وَرَجَائِي وَأَنْتَ غَايَةُ مَطْلُوبِي وَمُنْتَابِي فِي مُنْقَلَبِي
 وَمَثْوَايِ، إِلَهِ كَيْفَ تَطْرُدُ مِسْكِينَاً التَّجَأَ إِلَيْكَ مِنَ الدُّنُوبِ

هارِبًا، أَمْ كَيْفَ تُخِيبُ مُسْتَرِشِدًا قَصَدَ إِلَى جَنَابِكَ سَاعِيًّا، أَمْ
 كَيْفَ تَرُدُّ ظَبَانًا وَرَدًا إِلَى حِيَاضِكَ شَارِبًا كَلًا وَحِيَاضُكَ مُتَرَعِّةً فِي
 ضَنْكِ الْمُحْوِلِ، وَبَابِكَ مَفْتُوحٌ لِلَّطَبِ وَالْوَغْوِلِ، وَأَنْتَ غَايَةُ
 الْبَسْوَولِ (السُّؤُلِ) وَنِهَايَةُ الْأَمْوَلِ، إِلَهِ هَذِهِ آزِمَّةُ نَفْسِي
 عَقْلُتُهَا بِعِقَالٍ مَشِيشِتَكَ وَهَذِهِ أَعْبَاءُ ذُنُوبِي دَرَأْتُهَا بِعَفْوِكَ
 وَرَحْمَتِكَ وَهَذِهِ أَهْوَائِي الْبِضْلَةُ وَكَلَّتُهَا إِلَى جَنَابِ لُطِفَكَ
 وَرَأْفَتِكَ، فَاجْعَلْ اللَّهُمَّ صَبَاحِي هَذَا نِازِلًا عَلَى بِضِياءِ الْهُدَى
 وَبِالسَّلَامَةِ بِالسَّلَامِ فِي الدِّينِ وَالدُّنْيَا، وَمَسَائِي جُنَاحَةِ مِنْ كَيْدِ
 الْعِدَى (الْأَعْدَاءِ) وَوِقَايَةِ مِنْ مُرْدِيَاتِ الْهَوَى إِنَّكَ قَادِرٌ عَلَى مَا
 تَشَاءُ تُؤْتِ الْمُلْكَ مَنْ تَشَاءُ وَتَنْزِعُ الْمُلْكَ مِنْ تَشَاءُ وَتَعْرِزُ
 مَنْ تَشَاءُ وَتُنْذِلُ مَنْ تَشَاءُ، يَسِيرْكَ الْخَيْرُ إِنَّكَ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ
 قَدِيرٌ، تُولِجُ اللَّيْلَ فِي النَّهَارِ وَتُولِجُ النَّهَارَ فِي اللَّيْلِ وَتُخْرِجُ الْحَمَّ
 مِنَ الْبَيْتِ وَتُخْرِجُ الْبَيْتَ مِنَ الْحَمَّ وَتَرْزُقُ مَنْ تَشَاءُ بِغَيْرِ

حِسَابٌ، لَا إِلَهَ إِلَّا أَنْتَ سُبْحَانَكَ اللَّهُمَّ وَبِحَمْدِكَ مَنْ ذَا يَعْرِفُ
 قَدْرَكَ فَلَا يَخَافُكَ، وَمَنْ ذَا يَعْلَمُ مَا أَنْتَ فَلَا يَهَا بُكَ، أَلَّا
 بِقُدْرَتِكَ الْفِرَقَ، وَفَلَقْتَ بِلُطْفِكَ الْفَلَقَ، وَأَنْزَلْتَ بِكَرَمِكَ
 دِيَاجِي الْغَسَقِ، وَأَنْهَرْتَ الْبِيَاهَ مِنَ الصُّمِّ الصَّيَاخِيدِ عَذْبَاً
 وَأَجَاجَاً، وَأَنْزَلْتَ مِنَ الْبُعْصِرَاتِ مَاءً ثَجَاجَاً، وَجَعَلْتَ الشَّسْوَسَ
 وَالْقَمَرَ لِلْبَرِّيَّةِ سِرَاجاً وَهَا جَا مِنْ غَيْرِ أَنْ تُسَارِسَ فِيهَا ابْتَدَأْتَ بِهِ
 لُغُوبَاً وَلَا عِلاجاً، فَيَا مَنْ تَوَحَّدَ بِالْعِزِّ وَالْبَقَاءِ، وَقَهَرَ عِبَادَةَ
 بِالْمَوْتِ وَالْفَنَاءِ صَلَّى عَلَى مُحَمَّدٍ وَآلِهِ الْأَتْقِيَاءِ، وَاسْتَعِنْدِي
 وَاسْتَجِبْ دُعَائِي وَحَقِّقْ بِفَضْلِكَ أَمَلِي وَرَجَائِي يَا خَيْرَ مَنْ دُعِيَ
 لِكَشْفِ الضَّرِّ وَالْمَأْمُولِ لِكُلِّ عُسْرَ وَيُسْرٍ بِكَ أَنْزَلْتُ حَاجَتِي فَلَا
 تَرْدَنِي مِنْ سَقِّي مَوَاهِبِكَ خَائِبًا يَا كَرِيمُ يَا كَرِيمُ بِرَحْمَتِكَ
 يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ وَصَلَّى اللَّهُ عَلَى خَيْرِ خَلْقِهِ مُحَمَّدَ وَآلِهِ
 أَجْمَعِينَ.

“Kwa jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa rehema

Mwenye kurehemu. Ewe Mwenyezi Mungu ewe Ambaye aliutoa ulimi wa asubuhi kwa utamkaji wa mapambazuko yake, na akavifisha vipande vyta usiku wenyewe giza kwa utusitusi wa kigugumizi chake, akatengeneza sanaa ya falaki zenyet kuzunguka katika vipimo vyta mwonekano wake, akatoa mwale wa juu kwa nuru ya mwako wake. Ewe Ambaye alionyesha dhati Yake kuitia dhati Yake, akatakasika dhidi ya kufanana na viumbwe Wake, na ametukuka dhidi ya kuoana na aina zake. Ewe Ambaye yuko karibu na mawazo ya dhana na yuko mbali na mitupo ya macho, na akajua yatakayokuwa kabla hayajakuwa. Ewe Ambaye ameniweka katika utulivu wa kisusu cha ulinzi Wake na amani Yake, akaniamsha kwenda kwenye yale aliyonitunuku mionganoni mwa neema Zake na hisani Yake, na akazuia dhidi yangu makucha ya ubaya kwa mkono Wake na uwezo Wake .

“Msalie Ewe Mwenyezi Mungu mwonyeshaji Kwako katika usiku wa giza kali, mwenye kushikilia njia Zako kwa kamba za utukufu mrefu, ambaye utukufu wake unaonekana katika kilele madhubuti kilicho waziwazi, aliyesimama imara kwa nyayo zake sehemu za utelezi zama za mwanzo, ziwe juu yake na juu ya aali zake wabora wateule wema. Na tufungulie Ewe Mwenyezi Mungu milango ya asubuhi kwa funguo za rehema na kufaulu. Na nivishe Ewe Mwenyezi Mungu joho bora la uongofu na wema kushinda yote. Na toboa Ewe Mwenyezi Mungu kwa adhama Yako chemchem ya unyenyekevu katika manywesheo ya moyo wangu. Na bubujisha Ewe Mwenyezi Mungu mbubujiko mkubwa wa machozi toka kwenye ncha za macho yangu. Utie adabu Ewe Mwenyezi Mungu uzembe wa ujinga wangu kwa hatamu ya ukinaifu .

“Mungu Wangu, ikiwa hutanianza kwa rehema toka

Kwako kwa taufiki nzuri ni nani atakayenipitisha njia ya kuja Kwako katika njia ya wazi, na ikiwa uvumilivu Wako unanikabidhi kwenye hatamu ya matumaini na matamano ni nani atakayesamehe kujikwaa kwangu toka kwenye visiki nya hawaa. Na iwapo msaada Wako utanitelekeza wakati wa kupambana na nafsi na shetani, bila shaka utelekezaji Wako utakuwa umeniegemeza kwenye shida na unyimwaji. Mungu Wangu, hivi unaniaona sijakujia ila kwa kadiri ya matumaini, au sikung'ang'ania ncha za kamba Zako ila pale dhambi zangu ziliponitenga mbali na nyumba ya muungano. Basi ni kipando kibaya kilioje! Ambacho nafsi yangu imekipanda kutokana na hawaa yake. Ole wake kwa udanganyifu uliyofanywa na dhana zake na matumaini yake, na imeangamia kwa ujasiri wake dhidi ya bwana wake na mkuu wake .

“Mungu Wangu, nimegonga mlango wa rehema Zako kwa mkono wa matarajio yangu, na nimekimbilia Kwako hali ni mwenye kutaka hifadhi dhidi ya upindukiaji wa hawaa zangu, nimetundika vichwa nya vidole nya mapenzi yangu kwenye kamba Zako. Basi nisamehe Ewe Mwenyezi Mungu yale niliyokuwa nimetenda mionganoni mwa kuteleza kwangu na makosa yangu, na niinue toka kwenye mwangusho wa joho langu, kwani hakika Wewe ni Bwana Wangu, kiongozi Wangu, tegemeo Langu na matarajio Yangu, na Wewe ndiye hatima ya maombi yangu na matumaini yangu katika mgeuko wangu na mafikio yangu .

“Mungu Wangu, vipi utamfukuza masikini aliyekimbilia Kwako dhidi ya dhambi na hali ni mwenye kukimbia, au vipi utavunja matumaini ya mwenye kuomba uongofu aliyejuka kwenye kizingiti Chako na hali ni mwenye kutembea haraka, au vipi utamzuia mwenye kiu aliyefika kwenye hodhi Yako na hali ni mwenye kutaka kunywa,

hapana haiwezekani kwani hodhi Zako ni zeny e kububujika katika taabu za ukame, na mlango Wako uko wazi kwa maombi na kuperanya (kuingia), na Wewe ndiye hatima ya kiombwacho na kilele cha matumaini .

“Mungu Wangu hizi ni hatamu za nafsi yangu nimezifunga kwa kitanzi cha matakwa Yako, na haya ni majoho ya dhambi zangu nimeyawekea kinga kwa msamaha Wako na rehema Zako, na hizi ni hawaa zangu zeny e kupoteza nimeziegemeza kwenye kizingiti cha upole Wako na huruma Yako. Jaalia Ewe Mwenyezi Mungu asubuhi yangu hii iwe ni yeny e kunishukia na mwangaza wa uongofu na usalama katika dini na dunia, na jioni yangu iwe ngome dhidi ya vitimbi vy a maadui na kinga dhidi ya maangamizi ya hawaa, kwani hakika Wewe ni Mwenye uwezo juu ya kile utakacho, humpa ufalme umtakaye na humnyang’anya ufalme umtakaye, na humtukuza umtakaye na kumdhali lisha umtakaye. Heri imo mikononi Mwako, hakika Wewe ni Muweza wa kila kitu. Huutia usiku katika mchana na ukautia mchana katika usiku na ukakitoa kilicho hai katika kilicho maiti, na ukakitoa kilicho maiti katika kilicho hai, na ukamruzuku umtakaye pasi na hesabu .

Hakuna mungu ila Wewe. Umetakasika Ewe Mwenyezi na kila sifa njema ni Yako, ni nani anayejua uwezo Wako kisha hakuogopi, na ni nani anayejua Wewe ni nani kisha asiku heshimu. Umeunganisha tofauti kwa uwezo Wako, na kwa huruma Yako umeipambazua asubuhi. Kwa ukarimu Wako umeng’arisha giza la usiku, na umeleta maji baridi na maji chumvi toka kwenye mawe magumu. Na ukateremsha maji yaangukayo kwa kasi kutoka mawinguni, na ukafanya jua na mwezi taa ing’ aayo na yeny e joto sana kwa viumbe, bila ya kutumia uchovu wala juhud i katika kile ulichokianzisha. Basi Ewe Ambaye amejitenga peke

Yake kwa utukufu na kubaki, na ukawatiisha waja Wake kwa kifo na kutoweka, mswalie Muhammad na aali zake wachamungu, sikia wito wangu na jibu dua yangu na timiza kwa fadhila Yako matumaini yangu na matarajio yangu. Ewe Ambaye aliitwa kuondoa dhara na ni Mwenye kutumainiwa katika kila zito na jepesi, nimeteremsha haja yangu Kwako hivyo usinirudishe mikono mitupu toka kwenye mlango wa zawadi Zako tukufu. Ewe Mkarimu! Ewe Mkarimu! Ewe Mkarimu! Kwa rehema Yako Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenye kurehemu. Na sala za Mwenyezi Mungu ziwe juu ya mbora kati ya viumbe Wake Muhammad na juu ya aali zake wote.”

Kisha nenda sijida na useme katika sijda yako:

إِلَهِي قَلْبِي مَحْجُوبٌ، وَنَفْسِي مَعْيُوبٌ، وَعَقْلِي مَغْلُوبٌ، وَهَوَانِي
غَالِبٌ، وَطَاعَتِي قَلِيلٌ، وَمَعْصِيَتِي كَثِيرٌ، وَلِسَانِي مُقْرَّبٌ إِلَى الْذُنُوبِ
فَكَيْفَ حِيلَتِي يَا سَتَارَ الْعَيْوِبِ وَيَا عَلَامَ الْغُيُوبِ وَيَا كَاشِفَ
الْكُرُوبِ، إِغْفِرْ ذُنُوبِ كُلَّهَا بِحُرْمَةِ مُحَمَّدٍ وَآلِ مُحَمَّدٍ يَا غَافِرِ
غَفَارِ يَا غَافِرِ بِرَحْمَتِكَ يَا أَرْحَمَ الرَّاحِمِينَ

“Mungu Wangu moyo wangu ni wenye kufunikwa, nafsi yangu ni yenye kuaibishwa, akili yangu ni yenye kushindwa, hawaaz zangu ni zenye kushinda, utii wangu ni mchache, maasi yangu ni mengi, na ulimi wangu ni wenye kuungama dhambi, basi nifanye nini Ewe Mwenye kusitiri aibu, Ewe Mjuzi wa mambo ya ghaibu, na Ewe Mwenye

kuondoa matatizo! Nighufirie dhambi zangu zote kwa utukufu wa Muhammad na aali Muhammad. Ewe Mwenye kughufiri! Ewe Mwenye kughufiri! Ewe Mwenye kughufiri! Kwa rehema Zako Ewe Mwenye kurehemu kushinda wote wenyewe kurehemu.”

Tunakutakia Hijja yenyewe kukubaliwa, juhudini zenyewe kuthaminiwa na amali zenyewe kupokewa.

تَتَبَّنِي لَكُمْ حَجَّاً مَقْبُولاً وَسَعْيَاً مَشْكُوراً وَعَيْلًا مُتَقَبِّلاً

ORODHA YA VITABU VILIVYO CHAPISHWA NA AL-ITRAH FOUNDATION

1. Qur'an Al-Kariim - Tafsir Al-Kashif Juzuuy ya kwanza mpaka Thalathini
2. Uharamisho wa Riba
3. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Kwanza
4. Uharamisho wa uwongo Juzuuy ya Pili
5. Hekaya za Bahlul
6. Muhanga wa Imamu Husein (A.S.)
7. Mikingamo iliyomzunguka Imamu Ali (A.S.)
8. Hijab vazi Bora
9. Ukweli wa Shia Ithnaashari
10. Madhambi Makuu
11. Mbingu imenikirimu
12. Abdallah Ibn Saba
13. Khadijatul Kubra
14. Utumwa
15. Umakini katika Swalaa
16. Misingi ya Maarifa

17. Kanuni za Ndoa na maadili ya Familia
18. Bilal wa Afrika
19. Abudharr
20. Usahihi wa Historia ya Uislamu na Waislamu
21. Salman Farsi
22. Ammar Yasir
23. Qur'an na Hadithi
24. Elimu ya Nafsi
25. Yajue Madhehebu ya Shia
26. Ukusanyaji na Uhifadhi wa Qur'an Tukufu
27. Al-Wahda
28. Ponyo kutoka katika Qur'an.
29. Uislamu mfumo kamili wa maisha ya kijamii
30. Mashukio ya Akhera
31. Al Amali
32. Dua Indal Ahlul Bayt
33. Udhuu kwa mujibu wa Kitabu na Sunna.
34. Haki za wanawake katika Uislamu

35. Mwenyeesi Mungu na sifa zake
36. Kumswalia Mtume (s)
37. Nafasi za Ahlul Bayt (a.s)
38. Adhana.
- 39 Upendo katika Ukristo na Uislamu
40. Tiba ya Maradhi ya Kimaadili
41. Maana ya laana na kutukana katika Qur'ani Tukufu
42. Kupaka juu ya khofu
43. Kukusanya swala mbili
44. Bismillah ni sehemu ya Qur'ani na husomwa kwa Jahara
45. Kuwaongoza vijana wa kizazi kipya
46. Kusujudu juu ya udongo
47. Kusheherekea Maulidi Ya Mtume (s)
48. Tarawehe
49. Malumbano baina ya Sunni na Shia
50. Kupunguza Swala safarini
51. Kufungua safarini
52. Umaasumu wa Manabii

53. Qur'an inatoa changamoto
54. as-Salaatu Khayrun Mina -'n Nawm
55. Uadilifu wa Masahaba
56. Dua e Kumayl
57. Sauti Ya Uadilifu wa Binadamu
58. Umaasumu wa Mitume - Faida Zake Na Lengo Lake
59. Umaasumu wa Mitume - Majibu Ya Aya Zenye Utata
60. Umaasumu wa Mitume - Umaasumu wa Mitume Muhammad (s)
61. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Kwanza
62. Nahju'l-Balaghah - Juzu ya Pili
63. Kuzuru Makaburi
64. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Kwanza
65. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Pili
66. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tatu
67. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Nne
68. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Tano
69. Maswali Na Mishkili Elfu - Sehemu ya Sita

70. Tujifunze Misingi Ya Dini
71. Sala ni Nguzo ya Dini
72. Mikesha Ya Peshawar
73. Malezi Ya Mtoto Katika Uislamu
74. Ubora wa Imam ‘Ali Juu ya Maswahaba Na Ushia
ndio njia iliyonyooka
75. Hukumu za Kifikihi zinazowahusu Wanawake
76. Liqaa-u-llaah
77. Muhammad (s) Mtume wa Allah
78. Amani na Jihadi Katika Uislamu
79. Uislamu Ulienea Vipi?
80. Uadilifu, Amani na Mtume Muhammad (s)
81. Mitala na Ndoa za Mtume Muhammad (s)
82. Urejeo (al-Raja’ a)
83. Mazingira
84. Utokezo (al - Badau)
85. Hukumu ya kujenga juu ya makaburi
86. Swala ya maiti na kumlilia maiti
87. Uislamu na Uwingi wa Dini

88. Mtoto mwema
89. Adabu za Sokoni
90. Johari za hekima kwa vijana
91. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Kwanza
92. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Pili
93. Maalimul Madrasatain Sehemu ya Tatu
94. Tawasali
95. Imam Mahdi katika Usunni na Ushia
96. Hukumu za Mgonjwa
97. Sadaka yenyе kuendelea
98. Msahafu wa Imam Ali
99. Ngano ya kwamba Qur'ani imebadilishwa
100. Idil Ghadiri
101. Kusoma sura zenyе Sijda ya wajibu
102. Hukumu zinazomuhusu mkuu wa kazi na Mfanyakazi
103. Huduma ya Afya katika Uislamu
104. Sunan an-Nabii
105. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya

Kwanza)

106. Historia na sera ya viongozi wema (Sehemu ya Pili)
107. Shahiid Mfiadini
108. Kusalia Nabii (s.a.w)
109. Ujumbe -Sehemu ya Kwanza
110. Ujumbe - Sehemu ya Pili
111. Ujumbe - Sehemu ya Tatu
112. Ujumbe - Sehemu ya Nne
113. Mariamu, Yesu na Ukristo kwa mtazamo wa Kiislamu
114. Hadithi ya Thaqalain
115. Maarifa ya Kiislamu
116. Ukweli uliopotea sehemu ya Kwanza
117. Ukweli uliopotea sehemu ya Pili
118. Ukweli uliopotea sehemu ya Tatu
119. Ukweli uliopotea sehemu ya Nne
120. Ukweli uliopotea sehemu ya Tano
121. Johari zenyе hekima kwa vijana
122. Safari ya kuifuata Nuru

123. Fatima al-Zahra
124. Myahudi wa Kimataifa
125. Kuanzia ndoa hadi kuwa Wazazi
126. Visa vyta kweli sehemu ya Kwanza
127. Visa vyta kweli sehemu ya Pili
128. Muhadhara wa Maulamaa
129. Mwanadamu na Mustakabali wake
130. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Kwanza)
131. Imam Ali ('a) Ndugu wa Mtume Muhammad (s)
(Sehemu ya Pili)
132. Khairul Bariyyah
133. Uislamu na mafunzo ya kimalezi
134. Vijana ni Hazina ya Uislamu.
135. Yafaayo kijamii
136. Tabaruku
137. Taqiyya
138. Vikao vyta furaha
139. Shia asema haya Sunni asema haya Wewe wasemaje?

140. Visa vya wachamungu
141. Falsafa ya Dini
142. Azadari-Kuhuzunika na Kuomboleza
143. Sunna katika Kitabu Fiqhi al-Sunnah
144. Mtazamo Mpya - Wanawake katika Uislamu
145. Kuonekana kwa Allah
146. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Kwanza)
147. Tabia njema kwa Mujibu wa Ahlul-Bayt (Sehemu ya Pili)
148. Ndugu na Jirani
149. Ushia ndani ya Usunni
150. Maswali na Majibu
151. Mafunzo ya hukmu za ibada
152. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 1
- 153 Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 2
154. Ahlul Bayt ndani ya tafsiri za Kisusunni No 3
155. Abu Huraira
156. Vipengee kadhaa katika Swala ya Jamaa na Msikiti.

157. Mazingatio kutoka katika Qur'an - Sehemu ya Kwanza
158. Mazingatio kutoka kaitka Qur'an - Sehemu ya Pili
159. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya kwanza
160. Mazingatio kutoka katika Uislamu - Sehemu ya Pili
161. Qur'ani Tukufu – Pamoja na Tarjuma ya Kiswahili
162. Falsafa ya Mageuzi ya Imam Husein (a.s)
163. Amali za Mwezi Mtukufu wa Ramadhani
164. Elimu ya Tiba za Kiislamu - Matibabu ya Maimamu
165. Uislamu Safi
166. Majlisi za Imam Husein Majumbani
167. Mshumaa.
168. Uislam wa Shia
169. Amali za Makka
170. Amali za Madina
171. Asili ya Madhehebu katika Uislamu
172. Sira ya Imam Ali kuhusu Waasi
173. Ukweli uliofichika katika neno la Allah

174. Uislamu na Mifumo ya Uchumi
175. Umoja wa Kiislamu na Furaha
176. Mas’ala ya Kifiqhi
177. Jifunze kusoma Qur’ani
178. As-Sahifatul Kamilah as-Sajjadiyyah
179. Hayya ‘Alaa Khayri’l-’Amal Katika Adhana
180. Ukweli kuhusu Funga ya Siku ya Ashura
181. Dua za Miezi Mitatu Mitukufu (Rajabu, Shaabani na Ramadhan)
182. Uadilifu katika Uislamu
183. Mahdi katika Sunna
184. Jihadi ya Imam Hussein (‘as)
185. Kazi na Bidii ni njia ya maendeleo
186. Abu Talib – Jabali Imara la Imani
187. Ujenzi na Utakaso wa Nafsi
188. Vijana na Matarajio ya Baadaye
189. Usalafi – Historia yake, maana yake na lengo lake
190. Ushia – Hoja na Majibu
191. Mateso ya Dhuria wa Mtume (saww)

192. Maombolezo – Msiba wa Bwana wa Mashahidi (a.s.)
193. Shahidi kwa Ajili ya Ubinadamu
194. Takwa
195. Mwonekano wa Upotoshaji katika Hazina ya Kiislamu
196. Amirul Muuminina ('as) na Makhalifa
197. Uongozi na Utawala katika Mwanendo wa Imam 'Ali ('a)
198. Kuelewa Rehma ya Mwenyezi Mungu

KOPI NNE ZIFUATAZO ZIMETAFSIRIWA KWA LUGHA KINYARWANDA

1. Amateka Na Aba' Khalifa
2. Nyuma yaho naje kuyoboka
3. Amavu n'amavuko by'ubushiya
4. Shiya na Hadithi

BACK COVER

Hija ni fursa ya Ummah wa Kiislamu kufikia hali ya Kiibrahim katika sekta ya kisiasa, kijamii, kitamaduni na kiroho. Mwenyezi Mungu amesema: "*Hakika Nyumba ya kwanza waliyowekewa watu ni ile iliyoko Makka yenyekubarikiwa na mwongozo kwa walimwengu.*" (Sura Aali Imran: 96).

Watu wamezoea zaidi kutimiza Hija yao kwa mwonekano wa nje katika siku za mukutano huu wa kimungu ambao huwaleta pamoja Waislamu toka pande zote za dunia bila kujali rangi zao, makabila wala mataifa na tamaduni za asili. Kwa kuwa Hija ni mkusanyiko wa kiroho wenyewe kulenga kuchanua na kustawi katika nyanja zote za maisha ya mwanadamu, ni vizuri mahujaji wetu wakaelewa kwamba ibada hii ni kama ibada nyingine katika kuilea jamii katika sekta zote za maisha ya kisiasa, kitamaduni na kijamii, na hivyo ni lazima tuitumie fursa hii kama Bunge la Waislamu la Kimataifa na Baraza Kuu la Waislamu duniani kupanga mikakati yao ya kiroho, kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni, ili kwamba lengo la Nabii Ibrahim (a.s.) lidhihirike ndani ya maisha yetu ya kila siku.

Ni juu ya Waislamu ambao hubeba ujumbe wa Mungu Mwenyezi, kufaidika kisiasa na kijamii na maudhui ya Hija, na kamwe wasiridhike na mwonekano wa nje. Lakini ni lazima watambue kwamba ibada ya kisiasa na kijamii ya Hija inaweza kupatikana iwapo tu tutatimiza na kufikia ibada ya kimaadili na kiroho.

Kimetolewa na kuchapishwa na:
Alitrah Foundation
S.L.P. 19701 Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 2110640

Simu/Nukushi: +255 22 2127555

Barua Pepe: alitrah@yahoo.com

Tovuti: www.ibn-tv.com

Katika mtandao: www.alitrah.info